
## Mwongozo Wa Mwalimu

1

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

### Kuendeleza mahusiano binafsi na Mungu



MVMM

Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

## Kuendeleza mahusiano binafsi na Mungu

Kimeandikwa Na David Batty Pamoja Na Sally Girgis

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la tano

MVWW

Mafunzo Ya Vikundi Kwa Wakristo Wapya

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

**Kuendeleza mahusiano binafsi na Mungu**

Kimeandikwa Na David Batty Pamoja Na Sally Girgis

Mwongozo Wa Mwalimu

Toleo la tano

Maandiko Yanayotumiwa Katika Kitabu Hiki Yametoka Katika:

MAANDIKO: Biblia Takatifu (Union Version). Toleo La 1952, 1974, 1976, 1978. BST, BSK. Yametumiwa Kwa Ruhusa Maalum.

Tafsiri Ya Lugha Rahisi (TLR) itakayofanywa na mtafsiri ili kuleta maana halisi kama inavyosomeka katika lugha ya Kiingereza.

HakiMiliki © 2023, Teen Challenge USA.

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi vinavyohusiana na masomo haya ya *Mafunzo Ya Vikundi Kwa Wakristo Wapya* yanatawaliwa na Sheria za HakiMiliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka Global Teen Challenge.

Kwa mara ya kwanza, somo hili lilichapishwa kwa Kiingereza kwa jina lifuatalo: *How Can I Know I am a Christian? 5th edition*

Somo hili ni sehemu ya mfululizo wa masomo yaitwayo *Mafunzo Ya Vikundi Kwa Wakristo Wapya* yaliyotayarishwa ili kutumiwa makanisani, mashuleni, katika huduma gerezani, huduma za Changamoto Kwa Vijana, na huduma zingine kama hizo zinazofanya kazi na Wakristo Wapya. Vile vile kuna vifaa vingine vinavyopatikana kwa ajili ya mafunzo haya, kama kitabu cha kumwongoza mwalimu, cha kumwongoza mwanafunzi, Mwongozo Wa Somo cha mwanafunzi, mtihani, na cheti. Ukitaka habari zaidi juu ya masomo haya, wasiliana na:

Global Teen Challenge
PO Box 511
Columbus, GA, 31902 USA
Barua Pepe:gtc@globaltc.org
Tovuti: www.globaltc.org na
www.iTeenChallenge.org

MVMM
Mafunzo ya Vikundi
Yanayohusu Maisha Mapya

Mwaka wa Mwisho Kuhakikiwa: 06-2023

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

Hili somo linatoa mtazamo wa jumla kuhusu maana ya mtu kuwa Mkristo, na jinsi unavoweza kujua kwa uhakika kwamba kweli wewe ni mtoto wa Mungu. Somo kwa ufupi ni kama ifuatavyo:

1

**Sura Ya Kwanza. Je, ni vipi mtu huwa Mkristo?**

Katika sehemu hii ya somo, tunajifunza jinsi akili, nia na hisia zinavyohusika wakati mtu anapokuwa Mkristo.

2

**Sura Ya Pili. Nitazame Wapi Kupata Ushahidi Kwamba Mimi Ni Mkristo?**

Katika sura hii tunachunguza mahali unapoweza kutazama ili kupata ushahidi wa kuthibitisha ikiwa wewe ni Mkristo. Biblia, Roho Mtakatifu, na mabadiliko katika maisha ya mtu ndiyo mambo makuu yanayojadiliwa.

3

**Sura Ya Tatu. Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu Kristo**

Kukuza na kuendeleza uhusiano na Yesu, wa karibu sana na wa kina, ni eneo gumu la ukuaji kwa baadhi ya Wakristo wapya. Tunatazama njia chache za vitendo kabisa za kujenga urafiki wa karibu sana na Yesu.

4

**Sura Ya Nne. Nifanye Nini Na Mashaka Yangu Kuhusu Kuwa Mkristo?**

Wakristo wengi wapya hupitia kipindi cha kuwa na mashaka kama kweli wao ni Wakristo. Tunazungumza mahali mashaka yanakotoka, na kinachoyasababisha. Pia tunatazama jinsi mtu anavyoweza kuyaondoa mashaka hayo.

Kitabu hiki cha *Nanawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?* Kinaweza kutumiwa kama somo tangulizi kwa ajili ya mengine yote katika mfululizo huu wa *Mafunzo Ya Vikundi Kwa Wakristo Wapya*. Tutafurahi sana kukutumia habari zaidi jinsi ya kupanga vizuri masomo yenyewe. Andika maombi yako na uyatume kwa anwani iliyoko mbele ya kitabu hiki.

## Yaliyomo Katika Mwongozo Huu Wa Mwalimu

Kitabu hiki kina sehemu nne. Kila sehemu imeanza kwa ukurasa wenye rangi ya njano, ambao ni ukurasa wenye jina la mada.

1. Mipango Ya Mwalimu Kufundishia Somo
2. Mwongozo Wa Mwanafunzi
3. Mwongozo Wa Somo
4. Mtihani Wa Mwanafunzi Na Cheti Cha Somo

Maelezo juu ya jinsi ya kutumia kila sehemu yanapatikana mara tu baada ya utangulizi wa ukurasa unaofuata.

# Utangulizi

Hili ni somo moja katika mfululizo wa masomo ulioandaliwa kwa ajili ya kuwafundisha Wakristo wapya. Tunaamini kwamba lipo hitaji kubwa sana siku hizi la kuwasaidia Wakristo wapya ili wahusishe mafundisho ya Kristo na maisha yao ya kila siku kwa vitendo. Mafundisho haya pia yanaweza kutumiwa vizuri sana kwa ajili ya huduma kwa vijana kanisani na watu wazima wanaotamani kufanya Ukristo kuwa sehemu ya maisha yao kila siku.

Kusudi kubwa la somo hili na mfululizo mzima wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* ni kuwatambulisha Wakristo wapya kwa maswali muhimu yanayohusu maisha. Hatujaribu kuwapa mafundisho yatakayokuwa ndiyo mwisho kuhusu mada husika.

Kamati ya Mtaala ya Huduma ya Teen Challenge Marekani ina mpango wa kuendelea kupitia upya na kufanya marekebisho kwa masomo haya. Tunakaribisha mawazo yoyote au hoja za kutusaidia kuyaboresha.

## Jinsi ya kutumia huu Mwongozo Wa Mwalimu

### 1. Mipango Ya Mwalimu ya Kufundishia Somo

Kurasa za kwanza katika sehemu hii zinatoa mtazamo wa somo zima kwa kifupi.

Ukurasa unaofuata utakuwa ni nakala ya ***Orodha Ya Kazi Za Darasani***. Hii orodha inaonyesha wakati ambapo kila zoezi katika Mwongozo wa Somo linatakiwa kukamilishwa, na wakati kila chemsha bongo na mtihani vitakapotolewa. Kila mwanafunzi anapaswa kupewa habari stahiki kwa ajili ya ukurasa huo mwanzoni mwa kila somo. Kitabu hiki cha Mwongozo wa Somo tayari kina nakala isiyoandikwa chochote ya fomu hiyo, kwenye jalada la nyuma upande wa ndani.

Kitakachofuata ni mipango kwa ajili ya kufundishia kila somo. Hiyo yote ina kitu kinachoitwa Kweli Kuu ya Kibiblia pamoja na Mstari Mkuu. Hivyo vitu viwili vinaweza kutolewa mwanzoni mwa kipindi cha darasa. Pia vinasaidia kufanya mjadala ulenge yanayotakiwa kwa wakati wote.

Chini ya Kweli Kuu ya Kibiblia na Mstari Mkuu, kuna maelezo machache jinsi ya kufundisha somo lenyewe. Mara nyingi, marejeo yanaelekezwa kwenye Mwongozo wa Mwanafunzi au kwenye Zoezi linalopatikana katika Mwongozo wa Somo.

Kila somo humalizika kwa shughuli ya kufanya katika "Kufanyia Kazi Somo Maishani." Umuhimu wa kipengele hiki hauelezeki. Wakristo wapya wanahitaji mwongozo ulio wazi kuhusu jinsi ya kuanza kufanyia kazi mafundisho haya katika maisha yao ya kila siku. Hakikisha kwamba una toa nafasi ya kutosha ili kuwasaidia wanafunzi wako kuanzisha shughuli hii.

Mwisho wa kila mpango wa kufundishia somo kuna orodha ya kazi za wanafunzi kufanya.

Mengi katika masomo haya yalikusudiwa kuwa na vipindi vitano vya darasa, kila kimoja kikidumu kwa saa moja. Kipindi cha mwisho darasani ni kwa ajili ya mtihani. Masomo yote 14 katika mfululizo huu yanaweza kukamilishwa katika kipindi cha miezi kati ya mitatu hadi

minne, kama darasa litakutana kwa siku tano katika wiki. Ikiwa unafanya darasa kwa saa moja tu kwa juma, unaweza kukamilisha somo moja kwa mwezi – na mfululizo wote kwa kama mwaka mmoja. Mengi katika haya masomo yanaweza kupanuliwa na kufundishwa kwa muda mrefu, au kwa madarasa zaidi.

## 2. Mwongozo Wa Mwanafunzi

Hiki kitabu cha Mwongozo wa Mwanafunzi chaweza kutimiza makusudi mawili. Unaweza kutaka wanafunzi wasome kurasa husika katika kujiandaa kwa ajili ya somo linalokuja. Au, unaweza kuwataka wakisome baada ya wewe kufundisha somo, ili kufanya kama marudio na kuwa kama njia ya kusisitiza na kukazia kilichofundishwa darasani.

Tunakutia moyo uwaambie wanafunzi wajiandikie notsi darasani, hata ingawa utawapa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanayojiandikia wenyewe pamoja na mazungumzo na mijadala darasani vitawasaidia sana kuelewa vizuri baadhi ya mada zinazoshughulikiwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## 3. Mwongozo Wa Somo

Mazoezi yaliyo katika Mwongozo wa Somo yameandaliwa ili kumpa mwanafunzi kazi ya kufanya nje ya darasa. Baadhi ya kazi-mradi hizo zinasaidia kumwandaa mwanafunzi kwa ajili ya somo la darasa linalofuata.

Mengi ya mazoezi haya yamekusudiwa kuwasaidia wanafunzi wajikite ndani zaidi na kutazama baadhi ya maswala yanayojadiliwa darasani kwa kina. Lengo kuu la kazi hizo nyingi ni kuwaasaidia wanafunzi wagundue njia za kufanyia kazi hizo za kweli za Biblia katika maisha yao ya kila siku.

## 4. Mtihani Wa Mwanafunzi na Funguo la Majibu ya Mtihani

Mitihani hii imeandaliwa ili kutoa kipimo rahisi tu cha maendeleo ambayo kila mwanafunzi alipata katika uelewa wa kweli za Biblia zinazoshughulikiwa katika somo hili. Karatasi ya Majibu kwa ajili ya mtihani husika iko mara tu baada ya ukurasa wa mwisho wa ile nakala mfano ya mtihani wa mwanafunzi, katika Mwongozo huu wa Mwalimu.

## 5. Cheti Cha Somo

Cheti cha somo ni kwa ajili ya kuwatambua wale wanaomaliza kazi yote inayotakiwa kwa ajili ya somo hili na kufaulu mtihani. Mfano wa cheti hicho cha somo upo katika ukurasa wa mwisho wa kitabu hiki cha Mwongozo wa Mwalimu. Cheti cha Kufuzu pia kinapatikana kwa wale wanafunzi wanaomaliza masomo yote 14 katika mfululizo huu wa *Mafunzo ya Vikundi Ya Maisha Mapya*. Pia, mfano upo katika kile kitabu kinachoitwa ***Kuwatambulisha waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***.

# Jinsi Masomo Haya Yalivyotokea

Sulemani alisema, hakuna kitu kipya chini ya jua. Maneno hayo yanaweza kufaa hata kuhusu masomo haya. Mawazo yake mengi si mapya. Tunataka kutoa shukrani zetu maalum kwa Institute in Life Principles (Taasisi Ya Kanuni Za Maisha) kwa ushawishi mkubwa katika maisha ya watu waliotayarisha masomo haya. Masomo mengi yana alama za huduma hiyo ya Institue in Life Principles.

Nataka pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa waalimu wengi sana na maelfu ya Wakristo wapya ambao wametumia masomo haya katika kipindi cha miaka kadhaa iliyopita. Mawazo yao yamekuwa na mchango mkubwa sana katika maandalizi ya masomo haya. Pia ninamshukuru sana Ndugu Don Wilkerson kwa kunipa nafasi ya kufanya kazi katika kituo cha huduma ya Teen Challenge pale Brooklyn, New York, tokea mwaka wa 1971 hadi 1975. Katika miaka hiyo ndipo matayarisho yalipoanza ya masomo haya yaitwayo *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*.

Toleo la tano la *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* lilitayarishwa kwa msaada wa kamati ya Mitaala ya huduma ya Teen Challenge Marekani. Natoa shukrani maalum kwa wote waliosaidia katika mapitio na marekebisho hayo.

# Sera Kuhusu Kunakili Machapisho Haya

Vitabu vya Mwalimu na kila kitu cha mwanafunzi kinachohusiana na masomo haya ya *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya* kinalindwa na Sheria za Haki Miliki. Mpango maalum umefanywa ili kufasiri masomo haya kwa lugha hii ya Kiswahili. Masomo haya yanaweza kuchapwa na kugawanywa kwa ajili ya matumizi katika huduma za Teen Challenge na zinazofanana nazo, katika makanisa ya mahali, shule na mashirika mengine na hata watu binafsi. Pia, yanaweza kupatikana kutoka kwenye mtandao kwenye tovuti hii: www.iTeenChallenge.org Lakini, yasiuzwe. Yatolewe bure. Kwa wanaotaka kuchapisha na kuuza, wapate ruhusa kwa maandishi kutoka kwa Global Teen Challenge.

Dave Batty

# Pendekezo Kuhusu Mpangilio Wa Kufundisha

Somo hili ni moja kati ya 14 katika mfululizo wa *Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya*. Masomo yote 14 yameorodheshwa hapa kama pendekezo la jinsi ya kuyafundisha. Mfuatano huu ulitayarishwa kwa ajili ya ufundishaji endelevu wa masomo haya. Tunaweza kuutazama kama picha ya gudurumu lenye vichuma kumi na vinne. Masomo haya hayategemei linalotangulia. Kila somo linasimama lenyewe. Basi, mwanafunzi anaweza kujiunga na madarasa wakati wowote na akaingia tu vizuri kwenye mfumo.

1. Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
2. Kuitazama Biblia Kwa Haraka
3. Mtazamo
4. Majaribu
5. Maisha Ya Kikristo Yenye Mafanikio (ni pamoja na mafunzo juu ya huduma ya Roho Mtakatifu.)
6. Kukua kupitia kufeli
7. Matendo Ya Kikristo (Mahusiano Katika Kanisa La Mahali)
8. Utiifu kwa Mungu
9. Utiifu kwa Mwanadamu
10. Hasira na Haki za Kibinafsi
11. Jinsi Ya Kujifunza Biblia
12. Kujipenda na Kujikubali Mwenyewe
13. Mahusiano yako wewe Binafsi na Wengine
14. Nguvu Ya Kiroho na Mambo Yasio Ya Kawaida

Tazama kitabu kiitwacho, ***Kuwatanguliza waalimu kwa Mafunzo ya Vikundi Yanayohusu Maisha Mapya***, ili kupata maelezo zaidi juu ya kufundisha hayo masomo.

# Mipangilio ya Masomo

# Kwa Mwalimu

Angalia ukurasa wa 4 wa Mwongozo wa Mwalimu kwa habari zaidi
kuhusu matumizi ya mipangilio hii ya masomo

# Maelezo ya Jumla ya Somo

1. Siku moja au mbili kabla ya kukutana na wanafunzi katika kipindi cha kwanza, pengine ni vizuri kutambulisha somo hili kwa wanafunzi na kuwapa baadhi ya kazi zao za kwanza za kufanya. Ikiwezekana, gawa Mwongozo Wa Somo siku moja au mbili kabla hujaanza kufundisha somo lenyewe. Mwongozo wa Mwanafunzi unaweza kutolewa kwa wanafunzi wakati huu pia. Waambie wasome kurasa zile ambazo zitashughulikiwa katika kipindi cha kwanza cha somo.

2. Kwenye ukurasa wa 12 utakutana na nakala ya *Orodha Ya Kazi Za Darasani* inayotoa tarehe ambayo kila kazi inapaswa kukamilishwa. Waambie wanafunzi wajaze tarehe husika wakitumia ile nakala tupu iliyoko kwa ukurasa wa nyuma wa Mwongozo Wa Somo.

3. Wajulishe wanafunzi kwamba itabidi wawe wamemaliza Zoeli la 1 iliyoko katika Mwongozo Wa Somo watakapokuja darasani kw kipindi cha kwanza.

4. Kila mpango w a kufundishia somo unatoa *Shughuli Zinazotangulia Somo Za Kuchangamsha Wanafunzi* ili kutumiwa kuanzisha somo husika. Kusudi kuu la shughuli hizo ni kuwasaidia wanafunzi kuweka usikivu wao kwenye mada kuu ya hilo somo. Tunataka kutayarisha mazingira ya kukubalika na uwazi, mahali ambapo wanafunzi wote wanahisi huru kushiriki katika kipindi darasani.

5. Hebu fikiri kidogo juu ya uelewa wa wanafunzi wako kuhusu neno “Mkristo”. Waandishi wa somo hili wanatambua kabisa kwamba neno hili halina maana moja nyepesi. Lakini, ni neno la kiBiblia ambalo linaweza kuelezwa vizuri darasani kwa kiasi cha wanafunzi wako kutokuwa na mkanganyiko juu ya kile unachomaanisha wewe unapolitumia.

   Waandishi wana shauku ya dhahiri kabisa ya kujiepusha na maneno ambayo yanaeleweka na watu ambao wamekuwa Wakristo kwa miaka mingi. Somo hili kimsingi limetayarishwa kwa ajili ya Wakristo wapya na wanaotarajiwa, ambao wanaweza wasiwe na uzoefu sana wa maneno mengi maalum yanayotumiwa na Wakristo wa siku nyingi.

   Wakati neno “Mkristo” linapotumika katika somo hili, tunamaanisha juu ya wale ambao wana uhusiano halisi wa kibinafsi na Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao – au, waaminio wa kweli.

6. Itakubidi uamue ungependa kutumia vipindi vingapi vya darasa kufundisha somo hili. Kuna mipango ya kusaidia mwalimu kufundisha kwa ajili ya vipindi kumi katika kurasa zifuatazo. Lakini, ni rahisi sana somo hili kupanuka na kufikia vipindi 14 vya darasa. Majina ya masomo hayo 10 yameorodheshwa katika ukurasa unaofuata wa kitabu hiki cha mwalimu.

# Je, utatumia vipindi vingapi vya darasa kufundisha somo hili?

Utahitaji kuamua ni vipindi vingapi utakavyohitaji kufundishia somo hili. Mipango ya mwalimu kufundishia somo ni ya kutosha vipindi kumi, kwenye kurasa zinazofuata. Lakini, ni rahisi tu somo hili kuongezeka na kufikia vipindi 14. Majina ya masomo hayo kumi yameorodheshwa hapo chini. Yale yenye alama ya nyota (*) mbele yake yanaweza kugawanywa na kuwa masomo mawili. Mawazo yanatolewa katika mipango ya kufundishia masomo hayo jinsi unavyoweza kugawa vilivyomo ili vitoshe madarasa mawili.

**Sura ya 1: Je, ni vipi mtu huwa Mkristo?**

*Somo La 1: Kujitolea kwa akili na nia

*Somo La 2: Kujitolea kwa hisia

**Sura ya 2: Nitazame Wapi Kupata Ushahidi Kwamba Mimi Ni Mkristo?**

*Somo La 3: Biblia, Na Roho Mtakatifu

Somo La 4: Mabadiliko katika maisha yako

**Sura ya 3: Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu Kristo**

*Somo La 5: Uhusiano wangu binafsi na Yesu Kristo

Somo La 6: Kujenga Urafiki Na Yesu

**Sura ya 4: Nifanye Nini Na Mashaka Yangu Kuhusu Kuwa Mkristo?**

Somo La 7: Sababu za mashaka

Somo La 8: Kuyaondoa mashaka – sehemu ya 1

Somo La 9: Kuyaondoa mashaka – sehemu ya 2

Somo La 10: Mtihani

# Orodha ya Kazi za Darasani

**Jina La Somo** Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

| **Chemsha Bongo** | Maandiko Ya Kukariri | Tarehe |
|---|---|---|
| 1 | Kweli 8, Uk. 5 Mwongozo Wa Mwanafunzi | Somo La 2 |
| 2 | Warumi 8:16 | Somo La 3 |
| 3 | Yohana 1:12 | Somo La 4 |
| 4 | Yakobo 1:5-6 | Somo La 7 |

| **Zoezi la** | Tarehe Ya Kukabidhi |
|---|---|
| 1 | Somo La 1 |
| 2 | Somo La 2 |
| 3 | Somo La 3 |
| 4 | Somo La 3 au La 4 |
| 5 | Somo La 8 |
| 6 | Somo La 4 |
| 7 | Somo La 4 au La 5 |
| 8 | Somo La 5 au La 6 |
| 9 | Somo La 7 au La 8 |
| 10 | Somo La7 au La 8 |
| 11 | Somo La 7 |
| 12 | Somo La 9 |

**Mtihani** Tarehe Somo La 10

# Somo La 1
## Kujitoa Kiakili
## Kujitoa Nia

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Nikishaelewa kweli kutoka Biblia jinsi ya kuwa Mkristo, ninahitaji kuchukua hatua za kuwa Mkristo.

**2. Mstari Mkuu: Yohana 1:12, TLR**

Yeye alitoa haki na uwezo wa kuwa watoto wa Mungu kwa wale waliompokea. Aliwapa wale wenye kuliamini jina Lake.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa wa 4 hadi 8 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi huendana na sehemu hii ya somo. Tutatumia Mwongozo wa Somo Zoezi la 1, *"Kuwa Mkristo"* katika darasa la leo.

**4. Maandalizi Mapema Ya Mwalimu**

**A. Mahojiano na Mkristo**

Kwa ajili ya shughuli #17 katika mpango huu wa somo, utahitaji kufanya mahojiano na Mkristo. Pengine utapendelea kumpa mhusika huyo Mwongozo Wa Mwanafunzi asome sura ya kwanza kabla hujafanya mahojiano yenyewe. Ikiwezekana, mwambie mhusika aje kufanyiwa mahojiano ya ana kwa ana mbele ya darasa. Kama hiyo haiwezekani, basi fanya mahojiano hayo na uyarekodi au uyapige picha ya video. Hakikisha kwamba kinasa sauti kinanasa vizuri sana maswali yako na majibu anayotoa huyo mwenzako. Jaribu kutumia Dakika kumi hadi kumi na tano kwa ajili ya mahojiano hayo. Kama haiwezekani, basi chagua vipengele vichache vya mahojiano hayo na kuyawasilisha darasani kwa kutumia mashine.

Unaweza kutoa nakala zaidi za maswali yatolewayo katika shughuli #17 ili uwape wanafunzi. Wanaweza kulinganisha uzoefu wao na habari itakayotokana na mahojiano.

**B. Jedwali La Zile Kweli Nane**

Kweli nane ambazo mtu anahitaji kuzijua na kuamini ili awe Mkristo ni mojawapo wa jambo muhimu sana tunalotaka kushughulikia katika kipindi hiki cha kwanza cha darasa. Itakusaidia kwa ajili ya mjadala darasani kunakili kweli hizo nane kwenye karatasi kubwa ili kulionyesha darasani. Hii itafaa zaidi ikiwa utaendesha mahojiano ya ana kwa ana kwa ajili ya shughuli #17 katika mpango wa kufundishia somo.
Hizo kweli nane zimeorodhesha kwa ukurasa wa 5 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

**5. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)**

Chagua moja katika shughuli zifuatazo ili kuanzisha kipindi cha darasa leo.

**A. Mara ya kwanza mtu alipokuuliza kama wewe ni Mkristo**

Waulize wanafunzi kadhaa wawasilishe kwa darasa tukio la wao kuulizwa na mtu kwa mara ya kwanza ikiwa ni Wakristo. Je, waliitikiaje? Kama wengi katika wanafunzi wako wamelelewa katika nyumba za Kikristo, wanaweza wasikumbuke kuulizwa swali hili. Pengine utataka kuzungumza na mtu ambaye amefanya ushuhudiaji sana na kupata habari kadhaa za jinsi watu walivyojibu baada ya kuulizwa swali hilo.

**B. Je, kwa mawazo yako, ni nini kinachomfanya mtu kuwa Mkristo?**

Toa nafasi kwa wanafunzi kusoma majibu waliyotoa kwa swali #1 kwenye kazi-mradi namba 1 katika Mwongozo Wa Somo, linalouliza hivi: ***"Je, unafikiri ni kitu gani kinachomfanya mtu kuwa Mkristo?"*** Unaweza kutamani kutumia muda mfupi ili kujadili kidogo majibu watakayotoa, lakini msiingie kwenye mjadala mrefu sana hapa. Halafu, usitake sana majibu ya wanafunzi kuwa sahihi. Unaweza kurekebisha mawazo yoyote yasiyo sahihi katika mafundisho na majadiliano ya baadaye wakati wa kipindi.

**6. Toa Utangulizi wa Sura ya 1. Mtu Huwaje Mkristo?**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5**

Ukomavu wa kiroho wa wanafunzi wako utakuwa na mguso mkubwa jinsi utakavyofundisha somo hili. Ikiwa wengi katika wanafunzi wako hawajafanya bado uamuzi wa kuwa Wakristo, itakubidi uwe makini kutoa muda utakaotosha kwako kujibu maswali wanayoweza kuwa nayo. Usifikiri kwamba kila mtu aliye darasani mwako ni Mkristo.

Ukiwa na uhakika kwamba wengi wa wanafunzi darasani mwako wamekwishafanya uamuzi wa kumfuata Kristo, basi watie moyo kujifunza sehemu hii ya somo ili kuwaandaa kwa ajili ya kushuhudia. Wanapopitia mada hizi wanaweza kutafuta njia za kuzitumia ili kuzungumza na wasiokuwa Wakristo.

Unaweza kutamani kuanzisha mjadala kwa kuwapa nafasi wanafunzi wachache wahusishe darasa kwa majibu yao kwa swali #3 kutoka Zoezi la 1 katika Mwongozo wa Somo, linalosema hivi: "***Unaamini nini kuhusu Yesu Kristo?"*** Hii inaweza kukupa mtazamo kuhusu maudhui yakupasayo kutoa wakati wa kujadiliana juu ya kweli za kiBiblia zinazohusiana na sehemu hii ya somo. Usiingie katika mjadala mrefu wakati huu kuhusu swali hili. Ikiwa mwanafunzi mmoja au wawili watakuwa na maswali mazito hapa, weka mpango wa kuzungumza nao kwa undani zaidi baada ya kipindi.

Tunashauri **usiwaulize** wanafunzi kunyosha mikono yao ili kuonyesha jibu walilotoa kwa swali #2 katika Zoezi la 1 katika Mwongozo wa Somo, linalouliza, ***"Je, wewe ni Mkristo?"*** Hili ni swali binafsi, na linaweza kumweka mtu mahali pagumu. Tunataka wawe huru kutazama hoja zilizoko kwa somo hili bila ya kubanwa na sababu ya kufikiri kwamba wana shida kwa wao kuwa si Wakristo.

Sisitiza mada kuu katika fungu la maneno mwanzoni mwa Sura ya Kwanza katika ukurasa wa 5 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Mungu hatamdanganya mtu yeyote aingie kwa Ukristo. Onyesha kwamba kuna maeneo matatu ya kujiondoa kwayo mtu anapokuwa Mkristo.

> Kabla ya kuwa na uhakika kwamba wewe ni Mkristo ni lazima ujue jinsi ya kuwa Mkristo. Hakuna anayekuwa Mkristo kwa bahati mbaya. Mungu hamdanganyi mtu ili amfuate. Ukitaka kuwa Mkristo, lazima ufanye uamuzi na kujitolea kwa Kristo. Mambo haya matatu yafuatayo yanahusika katika hatua hii:
>
> Kujitolea kwa akili yako
>
> Kujitolea kwa nia/hiari yako
>
> Kujitolea kwa hisia zako
>
> *Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?, Mwongozo Wa Mwanafunzi, uku. wa 5*

**7. Kujitoa ni nini? (Dakika 3-5)**

Katika masomo mawili ya kwanza hapa, tutazungumzia kwamba kuwa Mkristo ni kujitolea kwa Kristo katika akili yako, nia yako na hisia zako. Hebu tumia muda mfupi kuzungumzia swala la kujitoa. Kwa baadhi ya watu, hili ni eneo lisilo na kina katika maisha yao. Hawafikiri kitu wanapovunja ahadi na kama watajikuta mahali pagumu. Kwa kifupi zungumzia kile ambacho Mungu anatafuta wakati tunaposema habari za kujitolea Kwake maisha yetu.

Wanafunzi wengine wanaweza kuibua maswali juu ya jinsi hisia zetu zinavyohusika katika kuwa Mkristo. Eleza kwamba swala hilo litashughulikiwa katika kipindi kijacho cha darasa.

**8. Jadili Hoja A-2. Zifuatazo ni kweli unazohitaji kujua na kuziamini ili uwe Mkristo (Dakika 10 hadi 15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5-6**

Pitia ile orodha ya kweli 8 zitolewazo ukurasa wa 5 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Hebu toa nafasi kwa wanafunzi kutafuta na kusoma Maandiko yanayokwenda na kila hatua. Hakikisha wanaelewa kweli kuu katika kila sentensi zifuatazo.

> **Hizi ndizo kweli unazohitaji kujua na kuziamini ili uwe Mkristo**
>
> 1. Mungu yupo. Waebrania 11:6
> 2. Biblia ni ya kweli. 2 Timoteo 3:16
> 3. Nimetenda dhambi kwa kutotii sheria za Mungu. Warumi 3:23
> 4. Mungu ananipenda, na alimtuma Yesu Mwanaye wa pekee, aishi na kufa kwa ajili yangu. Yohana 3:16
> 5. Yesu peke Yake ndiye anayeweza kusamehe dhambi zangu. Matendo 4:12
> 6. Adhabu ya dhambi ni kifo (kifo cha milele). Warumi 6:23
> 7. Ni naweza kuokolewa kutokana na adhabu ya dhambi kwa kutubu dhambi zangu kwa Yesu na kumwomba anisamehe. 1 Yohana 1:9
> 8. Ni naweza kuwa Mkristo kwa kumruhusu Yesu awe Kiongozi wa maisha yangu sasa. Warumi 10:9-10
>
> *Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5*

Yafuatayo ni maswali mengine ya ziada unayoweza kutumia katika mazungumzo yanayohusu sehemu hii ya somo:

1. Ni nini maana ya kujitolea kwa akili yako?
2. Je, unaona kwamba kuna kweli yoyote kati ya hizo kweli 8 ambayo haihitajiki kwa mtu kuwa Mkristo? Kama ni ndiyo, ni zipi? Eleza jibu lako.
3. Ni nini maana ya "kurukia gizani, kwa imani"?
4. Ile kanuni ya kiBiblia ya kuwa Mkristo inakuwaje tofauti na "kurukia gizani, kwa imani"?

**9. Je, Biblia ni sahihi? (Dakika 3-5)**

Wanafunzi wengine wanaweza kupata shida kidogo kukubaliana na hizo kweli 8 kwa sababu ya imani walizonazo kuhusu Biblia. Toa nafasi kwa wanafunzi kusoma majibu yao kwa swali #4 kutoka Zoezi la 1 katika Mwongozo Wa Somo linalosema, "***Je, ulipata shida au ilikuwa rahisi kwako kuamini kwamba Biblia ni ya kweli?"*** Ikiwa baadhi ya wanafunzi wana maswali mazito kuhusu jambo hili, unaweza kutumia muda mwingi kuzungumzia jinsi tunavyoweza kujua kwamba Biblia ni sahihi.

Mada hii itashughulikiwa kwa upana zaidi katika somo liitwalo ***Kuitazama Biblia Kwa Haraka***, ambalo ndilo somo lifuatalo ikiwa unafuata ule mpangilio wa masomo uliopendekezwa wa kufundisha masomo haya. Ikiwa swala hili ni sababu kubwa ya wanafunzi wako kusita kuwa Wakristo, basi tumia muda mrefu wakati huu kulishughulikia, hata kama itamaanisha kuongeza kipindi.

Ikiwa wanafunzi wanaamini kwamba Biblia si sahihi, wape uhuru wa kueleza ni kwa nini wanahisi hivyo. Wakati mwingine tatizo ni zile tafsiri mbalimbali za Biblia. Onyesha upesi sana kwamba hakuna tafsiri yoyote iliyo "kamilifu". Tafsiri nyingi tulizo nazo siku hizi ni nzuri, lakini zote zina udhaifu wake. Hatuna haja ya kuogopa kwamba mpango wa wokovu umepotoshwa katika tafsiri za Biblia. Mimi wakati wote huwapa changamoto wafikiri jinsi Mungu alivyo mkuu. Kama Yeye hawezi kutunza Maandiko yasipotoshwe kabisa na watafsiri, basi tatizo lililopo ni Mungu ambaye ni mdogo na aliye dhaifu.

Hapa pia ndipo mahali tunapoweza kujadili swala la imani na kumtumaini Mungu. Tunahitaji kuchunguza kwa makini kweli zote na kutumia akili zetu. Lakini kuna mahali ambapo hoja na fikra dhahiri zinashindwa kumfikisha mtu kwenye mahali pa kuokoka. Lazima tuwe tayari kuchukua hatua ya imani, bila ya kuelewa kwa ukamilifu kabisa ni nini kinahusika. Huku si "kurukia gizani, kwa imani", bali ni hatua ya imani iliyojengwa kwenye mafundisho yaliyo wazi kabisa ya kiBiblia. Kama mtu anapata shida kuiamini Biblia, mtie moyo kukiri hilo mbele za Mungu na kumwomba msaada.

**10. Unahitaji kujua kiasi gani ili uweze kuwa Mkristo?**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5-6**

Lazima tuwe makini tusiweke sheria kwamba mtu lazima ajue kiasi fulani juu ya mpango wa wokovu ndipo awe Mkristo. Zile kweli 8 zinazotolewa hapa ni kama mwongozo wa jumla. Mtu anaweza kutoelewa moja au zaidi ya kweli hizo mpaka baada ya kuwa Mkristo. Mungu yuko huru kumwokoa mtu yeyote anayetaka, akimwendea kwa moyo wa dhati.

Lakini, kuna watu ambao "wamepata dini" kwa namna ambayo walihisi kwamba kuna kitu kilichotokea ndani yao, na wakadhani kwamba hii inathibitisha wamekuwa Wakristo wakati huo. Eleza kwamba mtu huwa Mkristo, si kwa sababu tu ya maombi anayofanya. Wokovu wa kweli unatokea wakati Mungu anapomsamehe mtu dhambi yake na kuingia ndani yake ili kukaa katika roho yake. Jambo hili pia linazungumzwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 6.

**11. Tambulisha wa Hoja ya B. Kujitolea kwa nia au hiari yako**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 6-8**

Hakikisha wanafunzi wako wanaelewa tunamaanisha nini tunaposema "nia". Hii ndiyo ile sehemu inayofanya maamuzi katika haiba yako. Unaweza kutumia mfano wa kuzaliwa kwa mtoto ili kutofautisha tendo hilo na tendo la "kuzaliwa mara ya pili" wakati huu katika familia ya Mungu. Tazama mwisho wa ukurasa wa 6 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili upate maelezo zaidi juu ya mfano huo.

**12. Lazima ujue unachofanya kabla ya kufanya uamuzi**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 6-7**

Hebu eleza kwa kifupi mambo yanayotajwa kwenye ukurasa wa 6 na 7 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi chini ya kipengele #1, kwamba "*Lazima uelewe maana ya kuwa Mkristo*". Hayo yanaendana na yale tuliyokwishataja katika sehemu ya kwanza ya somo hili juu ya kujitolea akili yako. Jambo la kusisitiza hapa ni kwamba Mungu hataheshimu uamuzi utakaofanywa kwa ujinga – yaani, bila ya kujua chochote.

**13. Unafanyaje maamuzi muhimu? (Dakika 5)**

Swali #5 katika Zoezi la 1 kwenye Mwongozo Wa Somo ni shughuli ya kuwasaidia wanafunzi watambue ni utaratibu gani wanautumia wakati wanapofanya maamuzi muhimu. Waambie wanafunzi washirikishe majibu yao kuhusu shughuli hiyo. Onyesha umuhimu wa jambo hili jinsi ilivyo rahisi au vigumu kwa watu wengine kufanya maamuzi, na jinsi hilo linavyohusiana na kujitolea kwa ajili ya Kristo.

Kama mwalimu, unahitaji kuwa tayari kukubali ukweli kwamba wengi katika wanafunzi wako hawatumii utaratibu au mpango unaotumia wewe kufanya maamuzi. Hebu fikiri juu ya matokeo ya kutumia mitindo mbalimbali ya kufanya maamuzi, katika swala la kujitoa kwa ajili ya Kristo. Tazama matokeo mazuri na mabaya ya kila utaratibu au kila njia.

Kwa mfano: Yule mtu mwenye harara anaweza kushawishiwa kwa urahisi kujitoa kwa Kristo. Lakini, kujitoa huko kutadumu muda gani? Je, watapata mashaka upesi sana juu ya busara ya kufanya walichofanya? Je, yule "anayejali maelezo" atakaribia kukufanya uvurugikiwe kutokana na maswali yake mengi? Kama una mwanafunzi wa aina hiyo, fikiri matokeo ya uamuzi mzuri atakaofanya. Yawezekana kabisa kwamba mtu huyo hataachana na uamuzi wake, atakapokuwa ameufanya.

Ukiwa na muda mwishoni mwa kipindi, ni vizuri uzungumzie jambo hilo kwa upana zaidi. Swali #7 na 8 katika Zoezi la 1 kwenye Mwongozo Wa Somo linashughulikia hilo kwa kibinafsi zaidi. Hakikisha unapitia maswali hayo wakati unaposahihisha Kazi-Mradi namba 1 ili kuamua ni wanafunzi gani wanaohitaji kushughulikiwa kibinafsi ili kusaidia kuweka wazi zaidi jambo hilo.

**14. Jadili Hoja B-2. Lazima uamue kuwa Mkristo**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7**

Onyesha kwamba hawawezi tu kujifunza kweli za Biblia na kudhani kwamba kujua kweli ni ndio mwisho. Ni lazima wafanye uamuzi kwamba nani atakayekuwa kiongozi wa maisha yao – Mungu au Shetani. Hili jambo linashughulikiwa kwenye ukurasa wa 7 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi chini ya kipengele kidogo 2, *"Lazima uamue kuwa Mkristo"*.

**15. Jadili Hoja B-3. Kwa msaada wa Mungu, inakubidi utekeleze na kufanya kile ulichoamua (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 7-8**

Unaweza kutaka kutumia mfano kwamba ni rahisi sana kuweka ahadi, na jinsi ambavyo wakati mwingine inakuwa vigumu kushika, kutunza na kutimiza ahadi hiyo – kufanya ulichoahidi kufanya. Mtu anaposema, "Ninataka kuwa Mkristo," ni jambo rahisi hilo – ni maneno machache tu. Lakini kila mmoja wetu ni lazima kutekeleza na kufanya tulichoamua kufanya.

Eleza kila kinachohusika katika kutekeleza uamuzi huu.

1. Lazima ukiri dhambi zako mbele za Mungu, na kumwomba akusamehe.
2. Ni lazima umkaribishe Yesu awe kiongozi wa maisha yako.
   Maana yake ni kwamba unakabidhi maisha yako yote Kwake.
3. Ni lazima ugeuke kutoka njia zako za dhambi na uanze kutii sheria za Mungu na mafundisho Yake.

Zungumzia hoja itolewayo katika Yakobo 2:24 kwamba wokovu ni zaidi ya kusema maneno tu, bali huhusisha na matendo yetu.

Unaweza kutaka kutumia habari ya Biblia ya yule kijana tajiri aliyekuja kwa Yesu akiuliza jinsi anavyoweza kupata uzima wa milele. Tazama Luka 18:23-30; Mathayo 19:16-30; Marko 10:17-31. Onyesha kwamba Yesu hakumwambia mhusika aseme sala tu. Yesu alitaka kitendo, "Achana na utajiri wako uje unifuate." Yule mtu hakuwa tayari kutekeleza tendo lililotakiwa ili athibitishe kwamba kweli alimaanisha hilo katika uamuzi wake wa kutoa maisha yake kwa Kristo.

**16. Itakuwaje ukishindwa na ukatenda dhambi? (Dakika 3-5)**

Onyesha kwamba kujitoa kwako kwa Kristo hakukupi uhuru wa kutoka na kwenda kuvunja sheria za Mungu wakati wowote utakaotaka. Kwa upande mwingine, mtu hana haja ya kuokoka tena na tena kila wakati anapotenda dhambi. Zungumzia umuhimu wa kujitahidi kutimiza wajibu wako katika huku kujitoa kwako kwa Kristo. Mungu aliahidi atatupa nguvu za kupinga majaribu ili tumwishie Yeye. Lakini, onyesha kwamba kufanya uamuzi wa kuwa Mkristo hakupelekei kuwa na ukamilifu wa papo kwa papo.Sote tunashindwa, lakini pia tuna nafasi ya kujifunza kutokana na makosa yetu na kumkaribia Mungu zaidi.

**17. Mahojiano Na Mkristo (Dakika 10-15)**

Tungependa habari hiyo yote ifikie mahali pa kufanyiwa kazi katika kipindi hiki. Kumhoji Mkristo kwaweza kuwa njia bora ya kuwasaidia wanafunzi kuelewa jinsi ya kujitoa kwa akili na nia vinavyofanya kazi katika maisha ya mtu. Angalizo lililokuwepo mwanzo wa mpango huu wa kufundishia somo lilishauri kwamba ufanye maandalizi mapema kwamba utamhoji nani.

Ikiwezekana, fanya mahojiano ya ana kwa ana, mbele ya darasa. Kwa njia hiyo unaweza kutawala muda utakaotumia kwenye mahojiano hayo kutegemeana na jinsi wewe ulivyopanga wakati wa shughuli hiyo. Hakikisha unaendesha vizuri mahojiano hayo. Mwambie mhusika ajibu kwa kifupi – zisizidi Dakika 2 hadi 3 kwa kila jibu. Ukitaka maelezo zaidi, unaweza kuuliza swali lingine, hivi: “Je, unaweza kufafanua hilo kidogo zaidi?”

**Maswali Kwa Ajili Ya Mahojiano**

1. Ulizihisi vipi kweli za msingi kuhusu jinsi ya kuwa Mkristo kwa mara ya kwanza?
2. Ni kweli zipi kati ya zile 8 (za ukurasa wa 5 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi) zilizofafanuliwa kwako kwa uwazi *kabla* hujawa Mkristo?
3. Ni kweli zipi kati ya hizo 8 ambazo hazikufafanuliwa kwako kwa uwazi, mpaka ulipokuja kuwa Mkristo? Je, hiyo ilisababisha wewe kuchanganyikiwa akilini mwako juu ya ni nini hasa maana ya kuwa Mkristo?

   Maswali haya yafuatayo yanaweza kusaidia kuweka wazi tofauti kati ya kujitoa kwa akili zako na kujitoa kwa nia yako:

4. Ilikuwa vigumu kiasi gani kwako kuamini kwamba ulikuwa mwenye dhambi na mwenye kuhitaji msaada wa Mungu kuwa Mkristo?
5. Je, ilikuwa vigumu kwako kukubali kwamba Biblia ni ya kweli? Hebu eleza jibu lako – kama ilikuwa vigumu au haikuwa vigumu.
6. Ulipokuja kujua kwamba wewe ni mwenye dhambi, na kujua jinsi ya kuwa Mkristo, ulipita muda gani ndipo ukafikia mahali pa kusema, “Ndiyo! *Ninataka* kuwa Mkristo”?
7. Je, ulimwomba Mungu papo hapo akuokoe, uliposema, “Ndiyo! Ninataka kuwa Mkristo”? Kama hapana, ilikuchukua muda gani mpaka ukaomba sala hiyo?
8. Baada ya sala hiyo, ulipata maswali au mashaka kama kweli wewe umekuwa Mkristo?
9. Baada ya sala hiyo, ulipata wakati mgumu kusimamia uamuzi wako wa kuwa Mkristo?
10. Je, ulijihisi tofauti yoyote mara tu baada ya kusali na kumwambia Yesu awe Kiongozi wa maisha yako? Kama ulijihisi vizuri sana, hisia hizo zilidumu kwa muda gani?

Unaweza kuwauliza wanafunzi wa darasa lako walinganishe yaliyotokea kwao na hayo anayosimulia huyo mtu mnayemhoji. Unaruhusiwa kutoa nakala za maswali haya kwa ajili ya wanafunzi wako ukitaka.

Ukiwa na muda, waruhusu wanafunzi kumwuliza huyo mtu unayemhoji maswali waliyo nayo. Hakikisha kwamba unamalizia mahojiano hayo kwa wakati ili uweze kufunga darasa kwa shughuli yako uliyoandaa ya kufanyia kazi waliyojifunza.

Mazungumzo bila shaka yameweka wazi kabisa kwamba sote tuna aina tofauti za yanayotupata katika utaratibu wa kuwa Mkristo. Kila mmoja wetu amejifunza kwa namna fulani zile kweli kuhusu jinsi ya kuwa Mkristo. Sote tumekabiliana na uamuzi kwamba – *Sasa, nitafanya nini na mpango wa Mungu wa wokovu?* Akili yetu na nia yetu vinahusika katika kuwa Mkristo.

**18. Kutendea Somo Kazi Maishani (Dakika 5-10)**

Waambie wanafunzi wanakili zile kweli nane kutoka kwa ukurasa wa 5 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi na kuitikia kwa kuandika maneno yafuatayo pembeni ya kila kweli:

- Hii ninaiamini
- Hii siiamini
- Kwa hii sina uhakika

Shughuli hii itawasaidia wanafunzi kujitathmini kama wametoa akili zao kwa ajili ya imani hizo za Kikristo au hapana.

**19. Kazi Za Kufanya**

A. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 1, *“Kuwa Mkristo”*.

B. Waambie wakariri hizo kweli 8 na kuwa tayari kuziwasilisha kwenye chemsha bongo katika kipindi kinachofuata (za ukurasa wa 5 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi).

C. Wanafunzi wasome Sura ya 1 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kufanya marudio ya mazungumzo ya darasani leo, na kujiandaa kwa ajili ya kipindi kitakachofuata cha darasa.

**20. Tathmini ya mwalimu baada ya darasa**

Kwa kifupi, andika maelezo juu ya sehemu za somo ambazo zilisaidia.
Je, ulikaribia kiasi gani vile viwango vya muda ulivyopanga kwa ajili ya kila shughuli?

Unahitaji kufanya mabadiliko gani katika ile shughuli ya mahojiano (#17 katika mpango wa kufundishia)? Ni maswali gani utakayoondoa au kuongeza ili kuboresha wakati utakapofundisha darasa hili tena?

# Somo La 2
## Kujitoa Kihisia



**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Nahitaji kuelewa vizuri jinsi hisia zangu zinavyohusika katika kuwa Mkristo.

**2. Mstari Mkuu: Yakobo 1:9 TLR**

Ndugu Mkristo asiyekuwa na utajiri mwingi wa dunia hii anapaswa kufurahi kwa alicho nacho. Yeye ni mkuu machoni pa Mungu.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa wa 8 hadi 14 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi huendana na somo hili. Tutatumia Mwongozo wa Somo Zoezi la 2, *"Hisia"* katika darasa la leo.

**4. Maandalizi Mapema Ya Mwalimu**

**A. Chaguo la kuwa na vipindi viwili vya darasa**

Somo hili linaweza kupelekea mjadala wa mambo mengi yanayohusiana na nafasi ya hisia katika maisha ya Mkristo. Pengine utahitaji vipindi viwili ili kushughulikia maelezo ya somo hili, kama ratiba yako inaruhusu. Mara tu baada ya mpango huu wa kufundishia, utakutana na habari zaidi katika Maelezo ya Ziada ya Mwalimu, yanayoweza kutumiwa wakati huu. Tazama ukurasa wa 33 na 34 wa Kitabu hiki Cha Mwalimu.

**B. Picha za kawaida au zinazotumia mashine kwa ajili ya Shughuli Za Mpango Wa Mwalimu Kufundishia #10**

Shughuli #10 katika mpango huu wa mwalimu kufundishia inapendekeza utafute picha ya nyumba za kawaida au zinazotumika kwenye mashine, yenye kuonyesha nyumba hiyo ikiwa katika viwango mbalimbali vya kujengwa. Zitakazokuwa nzuri sana ni picha za msingi wa nyumba, sehemu ya chini, kuta na paa, na nyumba iliyomalizika, na ikiwezekana, picha kubwa ya jiko. Kama hutaweza kupata picha za nyumba inayoendelea kujengwa au iliyokamilika hivi karibuni, nenda kwenye maktaba ya serikali, na utapata vitabu kuhusu jinsi ya kujenga nyumba.

**5. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5-10)**

**A. Chemsha Bongo Kuhusu Hisia**

Toa changamoto ifuatayo mwanzoni mwa kipindi. Tazama ukurasa wa 23 katika kitabu hiki cha mwalimu upate hiyo changamoto. Waambie wanafunzi wako kwamba hayo yote ni maswali yenye majibu binafsi. Hawatapewa alama kwa ajili ya chemsha bongo hii. Kusudi lake ni kuwapa nafasi kufikiri juu ya hisia zao, na nafasi yake katika maisha yao ya kila siku.

Pengine utapenda kutoa nakala ya chemsha bongo hii ili kila mwanafunzi awe na nakala yake. Au unaweza kuichapisha kwenye karatasi inayoweza kutazamwa kwa mtambo maalum.

Baada ya wanafunzi kukamilisha chemsha bongo hiyo, hebu zungumzeni kwa kifupi majibu yao. Ikiwa wanafunzi wana majibu tofauti, wajulishe kwamba ni sawa. Waulize kueleza kwa kifupi ni kwa nini walichagua jibu lao. Jambo moja tunalotaka watu wapate kupitia shughuli hii ni haja ya kutafakari hisia zetu na kuona nafasi yake katika maisha ya Wakristo wapya. Hapo hapo, tunataka kutambua kwamba kila mtu ameumbwa kipekee, na ni wa maalum, hivyo hatuwezi kuitikia mambo yanayotupata kwa namna inayofanana.

**B. Mfano wa mtoto mchanga aliyezaliwa**

Watu wazima wengi pamoja na watoto hujieleza kihisia wanapokuwa karibu na mtoto mchanga aliyezaliwa. Waulize wanafunzi kufikiri juu ya kuzaliwa kwa mtoto. Hebu wajifanye kwamba ni mama, au baba, au daktari, nesi, babu na bibi, au kaka na dada wa mtoto mchanga aliyezaliwa. Unapomwona mtoto kwa mara ya kwanza, ni hisia gani unazoweza kuonyesha? Wape wanafunzi nafasi ya kuwasilisha majibu yao darasani.

Onyesha kwamba watu waliohusika katika kuzaliwa kwa mtoto wanaweza kuhisi tofauti, japo tukio ni hilo hilo moja.

Kuzaliwa kwa mtoto kimwili kunafanana kwa njia nyingi na kuzaliwa kwa Mkristo mpya kiroho. Watoto wengi huanza kulia muda mfupi baada ya kuzaliwa. Majuma na miezi ya kwanza imejaa mambo mengi mapya, na mengine – hasa nepi chafu – si ya kufurahisha sana. Maisha ya mtoto mara nyingi yamejaa kilio, maumivu, kuona kama mambo hayaendi anavyotaka, kuhisi kutengwa, kuhisi baridi sana, au joto sana – yaani, hali mbaya kwa jumla! Mtoto anapata wakati mgumu kuendana na mabadiliko yote ya maisha yake mapya. Wale watu wazima wanaomzunguka wanayaita hayo “kukua”.

Mara nyingi Wakristo wapya hupitia nyakati zinazofanana na hizo – chungu na zenye kuchanganya, wakijaribu kuchukuliana na maisha mapya ya kuwa Mkristo. Hakika si maisha yaliyojaa furaha wakati wote. Leo katika kipindi chetu, tutatazama kwa undani kidogo jinsi hisia zetu zinavyohusika kwa sisi kuwa Wakristo, na ziwe na nafasi gani katika maisha yetu mapya.

## Chemsha Bongo Kuhusu Hisia

Kweli Si Kweli 1. Mkristo aliye karibu sana na Mungu atahisi furaha wakati wote.

Kweli Si Kweli 2. Kuweka hasira yako ndani ni bora kuliko kuionyesha kwa matendo ya nje.

Kweli Si Kweli 3. Mkristo anapohisi msongo wa mawazo, kuna kitu kisichokuwa sawa katika maisha yake ya kiroho (uhusiano wake na Mungu).

Kweli Si Kweli 4. Wakristo wapya wanaweza kudumu kwenye kilele cha “juu” kiroho ambacho mara nyingi huja baada ya wao kuongoka, kama wanatii kwa makini sana sheria za Mungu.

Katika maswali manne yanayofuata, chora mviringo kwenye jibu lenye kueleza vizuri hali yako na hisia zako. Maswali mengi yana jibu sahihi zaidi ya moja.

5. Wakati mtu anaponiumiza au kunikasirisha, ni vigumu kwangu kumwambia mhusika ninavyohisi.

   Ni mimi Ni mimi kidogo Sio mimi kabisa

6. Kwa kawaida, mimi ni mwepesi sana kuonyesha hisia zangu (kwa matendo).

   Ni mimi Ni mimi kidogo Sio mimi kabisa

7. Kwa kawaida mimi huweka hisia zangu ndani, na sizionyeshi wala kuzitoa.

   Ni mimi Ni mimi kidogo Sio mimi kabisa

8. Ni vigumu kwangu kumwambia Mungu jinsi ninavyohisi, wakati ninapoudhiwa au kusongwa kimawazo.

   Ni mimi Ni mimi kidogo Sio mimi kabisa

**6. Marudio ya kujitoa akili na nia**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5-8**

Wanafunzi wengi watapata wakati mgumu kukumbuka yale mambo makuu unayotoa katika maeneo haya matatu ya kujitoa. Kwa vipindi viwili au vitatu vya darasa vinavyofuata, chukuaDakika chache kurudia yale maeneo mawili ya kujitoa yaliyotajwa katika kipindi cha kwanza cha darasani – kujitoa kwa akili na kujitoa kwa nia. Waambie wanafunzi waeleze nini kinahusika katika kila eneo. Tumia hiyo kama daraja au kivuko cha kuingia katika eneo la tatu tutakaloshughulikia kwa leo – kujitoa kwa hisia zetu.

**7. Toa Utangulizi wa Hoja ya C. Kujitolea kwa hisia zako**
**(Dakika 2-3) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8**

Shughuli ya kuchangamsha somo inapaswa kuelekeza usikivu wao kwenye hisia. Yafuatayo ni maswali machache ambayo tunataraji kuyajibu katika kipindi cha leo. (Usijaribu kuyajibu wakati huu. Yatoe kwa darasa ili kuwapa wazo juu ya baadhi ya maswala tunayotarajia kushughulikia leo.)

1. Je, hisia zina nafasi gani katika mtu kuwa Mkristo?
2. Hisia zetu ni muhimu kiasi gani?
3. Je, natakiwa kuhisi tofauti baada ya kuwa Mkristo?
4. Je, natakiwa kuhisi kwamba Mungu yuko maishani mwangu baada ya kuwa Mkristo?

**8. Tambulisha Hoja C-1. Hisia zako zinahusikaje unapokuwa Mkristo?**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 8**

Rejelea ule mfano uliotumiwa katika shughuli ya kuchangamkia somo, jinsi watu mbalimbali wanavyoitikia kihisia kwa jambo au hali fulani moja. Hili ni kweli hata wakati watu wanapofanya uamuzi wa kuwa Wakristo.

Tumia ule mfano wa Suzana ulio katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ukurasa wa 8 na 9. Hakikisha mnazungumzia zile ahadi potofu zitolewazo na baadhi ya Wakristo – kwamba utahisi upendo, furaha na amani toka kwa Mungu mara tu utakapokuwa Mkristo. Hayo yote hayana msingi katika Maandiko. Wakristo wengi huwa na hisia nzuri wanapotoa maisha yao ka Kristo. Hili ni sawa na ni nzuri. Lakini hakuna uhakikisho utolewao katika Maandiko kwamba "tutahisi" tumeokoka mara tu baada ya kumaliza sala ya kukabidhi maisha yetu kwa Kristo.

Kazia kwamba, sawa na jinsi ambavyo mtoto mchanga aliyezaliwa anavyopitia marekebisho mengi magumu katika siku na majuma ya mwanzo baada ya kuzaliwa kwake, ndivyo ilivyo na Wakristo wapya mara nyingi wanavyopitia katika nyakati ngumu za marekebisho. Wamtarajie Roho Mtakatifu kuwaonyesha dhambi, ambayo mara nyingi hupelekea watu kuhisi hatia.

**9. Jadili Hoja C-1-b. Hisia zako hubadilika**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9**

Eleza jinsi ilivyo kawaida kabisa kupitia hisia za kupanda na kushuka. Hiki ni kitu kitakachoendelea hata mtu akishakuwa Mkristo. Ikiwa walihisi kuinuliwa sana kihisia wakati walipofanyika Wakristo, washukuru kwa hilo, lakini wasipoteze matumaini hisia hizo zinapoondoka.

Ikiwa mtu hakupatikana na badiliko lolote kihisia alipokubali kuwa Mkristo, basi atafute uwepo wa Mungu maishani mwake utakaopelekea mabadiliko mazuri.

Haijalishi itikio lao la kiroho lilikuwaje walipoomba sala ya kuwa Wakristo. Wanapaswa kujua kwamba Mungu anataka kuleta upendo, amani na furaha katika maisha yao. Hayo maitikio ya kihisia si jambo kubwa la kutafuta katika uhusiano wako na Mungu. Hizo ni kama faida za ziada, katika kule kudumisha uhusiano binafsi na ulio halisi na Yesu. Tutashughulikia jambo hilo katika sura ya tatu kwenye Mwongozo Wa Mwanafunzi, ijulikanayo kama "Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu Kristo".

**10. Jadili Hoja C-1-c. Hisia zako zishike nafasi ya tatu unapofanywa kuwa Mkristo (Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 9-10**


Ili kuonyesha nafasi ya hisia zetu tunapokuwa Wakristo, rudi hadi kwenye yale maswala mawili yaliyozungumziwa katika somo lililopita. Kwanza kabisa ni kuwa na uelewa mzuri kwamba Biblia inasema nini kuhusu kuwa Mkristo. Pili: Ni lazima ufanye uamuzi ulio dhahiri – kujitolea nia yako kabisa. Hapo ndipo Mungu atakupa imani – nguvu – ya kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza uamuzi wako.
Pia, tunahitaji kukabidhi hisia zetu kwa Kristo, tukitambua kwamba kwa sasa Yeye ndiye Kiongozi wa kweli wa maisha yetu.

Kwenye ukurasa wa 10 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi unakutana na kielelezo cha nyumba, kinacho-onyesha uhusiano ulioka baina ya hayo maeneo matatu.
Yafuatayo ni maelezo zaidi ya kielelezo hicho.

Jinsi unavyohisi unapokuwa Mkristo si muhimu kama kuelewa na kutii kweli zilizomo kwa Biblia, zinazokwambia jinsi unavyoweza kuwa Mkristo.

**A. Kujenga Nyumba Yako**

(Ikiwezekana, tambulisha kielelezo hiki kwa kutumia picha za nyumba. Onyesha ikiwa katika hatua mbalimbali, za kukamilika kwake, kwa kulingana na kielelezo hiki.)




**Michoro:** Ukitaka kujenga nyumba mpya, ni lazima uwe na michoro kabla hujaanza ujenzi. Ni muhimu sana kufuata michoro hiyo unapojenga nyumba yenyewe. Kama hujawahi kujenga nyumba, utahitaji msaada wa mtu anayejua jinsi ya kujenga nyumba.

**Msingi:** Inapofikia kujenga nyumba yako, kitu cha kwanza unachofanya ni kuchimba chini na kuweka msingi imara. Huu msingi ni lazima uwe na nguvu ya kutosha kutegemeza hilo jengo kwa miaka mingi sana.

**Nyumba Yenyewe:** Msingi sahihi ukishawekwa, ndipo unapoanza kujenga nyumba. Usitumie kitu chochote kile au chakavu kuijenga. Unatafuta vifaa bora

unavyoweza kununua, tena, vilivyo sahihi. Unatumia vifaa hivyo ambavyo vimetamkwa kwenye mchoro. Itakuchukua muda kuijenga. Kuta lazima zijengwe, paa liwekwe, madirisha na milango iwekwe pia.

**Joto:** Baada ya nyumba kujengwa, ndipo mahali pa kuwashia moto panapotumiwa kwa mara ya kwanza, na joto linajaa ndani ya nyumba. Itakuwa ujinga kuwasha moto kabla nyumba haijakamilika. Kwa sababu, wakati jiko litakapokuwa linafanya kazi vizuri, joto litajaa nyumba na kuifanya mahali pazuri pa kuishi. Joto haliifanyi nyumba kuwa imara. Nyumba kama imejengwa vizuri, itasimama imara na kuwa na nguvu, lile jiko liwashwe au lisiwashwe.

**B. Kufanyia kazi kielelezo**

Kuwa Mkristo kunaweza kufananishwa na kujenga nyumba. Ukitaka kuwa Mkristo aliyefanikiwa, lazima ufuate mpango wa Mungu. Utahitaji msaada wa Roho Mtakatifu ili kufanyika Mkristo. Yeye ana uzoefu na ujuzi mwingi sana wa kuwasaidia watu "kujenga nyumba zao" (yaani, maisha yao ya Kikristo).

**Msingi:** Kama unataka uwe Mkristo, ni lazima kuweka msingi imara kwanza. Hii sehemu ya nyumba inaweza kulinganishwa na kuelewa na kutii kweli zilizomo katika Biblia, inayokwambia jinsi ya kuwa Mkristo. Kweli hizo ni msingi imara ambao juu yake unaweza kujenga maisha yako ya Kikristo. Yesu ameahidi kwamba kweli hizo hazitabadilika kamwe. Tazama Mathayo 5:18.

Watu wengine wanafikiri kwamba msingi kwa ajili ya maisha yao ya Kikristo unaweza kuwa hisia zao. Hisia zako ni msingi wa hali ya chini sana kwa ajili ya Ukristo wako. Ukijenga maisha yako ya Kikristo juu ya "msingi wa kuhisi", nguvu na uthabiti wa maisha yako ya kiroho zitabadilika kila siku. Kwa siku zile utakazohisi vizuri, utajihisi kwamba wewe ni Mkristo mwenye nguvu. Lakini hizo hisia nzuri zikiondoka, "nyumba" yako itatikisika, na yaweza kuanguka na kuharibika.

Msingi pekee ambao ni imara ni ule Mungu aliotupatia, yaani, Neno Lake – Biblia.

**Jengo Lenyewe:** Unajenga maisha yako ya Kikristo kwa imani. Imani ndiyo nguvu ambayo Mungu anakupa, ili ujenge juu ya msingi imara wa Neno la Mungu. Huwezi kuwa Mkristo aliyefanikiwa wewe binafsi kwa nguvu zako tu. Unahitaji msaada wa Roho Mtakatifu, ambaye ni Kiongozi wako na Mwalimu. Anakupa vifaa unavyohitaji na kukufundisha jinsi ya kujenga maisha yako ya Kikristo.

Watu wengine wanataka kuwa Wakristo na "kuweka msingi stahiki". Wanafuata zile kweli za Biblia na wakawa Wakristo. Lakini, wanakosea kwa kujaribu kujenga na kudumisha maisha yao ya Kikristo kwa hisia. Hisia zako si "kuta zenye nguvu" wala "paa lenye nguvu", wala si "milango mizuri au madirisha". Hisia si "vifaa" ambavyo ramani ya Biblia inataja kwamba vitumike.

Ukitaka kujenga maisha ya Kikristo yenye nguvu, lazima ufuate ramani ya Mungu – nayo inapatikana katika Biblia. Lazima utumie "vifaa" vile Atakavyokwambia Yeye uvitumie, na ni lazima ujenge "nyumba" yako kwa namna ile anayosema Yeye. Mungu ndiye anayepaswa kusimamia.

Ukitumia hisia zako kama "vifaa" kwa ajili ya kujengea "nyumba" yako, inaweza kuwa hatari kuishi humo. Kuna siku kuta zitakuwa na nguvu, siku zingine hazitakuwepo. Ukuaji wako wa Kikristo kila siku lazima ujengwe – si kwa matendo yako na mapenzi yako – bali kwa nguvu na msaada wa Roho Mtakatifu.

**Joto:** Hisia hushika nafasi ya tatu. Hisia zako zinaweza kulinganishwa na joto linalojaa kwa nyumba. Hisia zako ndizo zinazofanya maisha yako ya Kikristo kuwa ya kupendeza zaidi. Ikiwa utaelewa nafasi sahihi ya hisia zako katika maisha yako ya kila siku ya Kikristo, utabakia salama kama Mkristo, hata kama hisia zitakuja au zitaondoka.

Nyumba ni nyumba, hata kama kuna joto au hakuna joto. Ndivyo ilivyo hata kwa kuwa Mkristo. Wewe ni Mkristo kwa sababu uliweka msingi sahihi na kujenga "nyumba" yako kwa msaada na vifaa ambavyo Mungu alikupa. Hisia nzuri (au kuhisi vizuri) hazikufanyi uwe Mkristo. Ikiwa hisia zimeondoka, na ukiwa huhisi kwamba wewe ni Mkristo, na kama huhisi kwamba una Mungu wakati wote, ni sawa tu. "Nyumba" bado inasimama imara.

**11. Jadili Hoja C-2. Ni hisia zipi zinazohusika wewe unapokuwa Mkristo? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 10-11**

Wanafunzi watumie majibu yao kutoka kwa lile Zoezi la 2, Sehemu ya Kwanza katika Mwongozo Wa Somo katika kuzungumzia jambo hili. Wazo kuu tunalotaka kutoa hapa ni kwamba kuna aina mbalimbali za hisia ambazo zinafaa kuhisi kwa hali ya mtu kama Mkristo. Pengine ujisomee Maandiko yaliyotolewa katika Zoezi la 2.

**12. Uzoefu binafsi wa maitikio ya hisia wakati wa wokovu (Dakika 3-5)**

Waruhusu wanafunzi kadhaa washirikishe darasa mambo waliyopitia wakati walipokuwa Wakristo. Waambie maelezo yao yaishie kwa kueleza hisia walizopata wakati huo. Wanaweza kutumia majibu yao kutoka kwa Sehemu ya 2 ya Zoezi la 2 katika Mwongozo Wa Somo.

**13. Tambulisha Hoja ya C-3. "Jifunze jinsi Kristo anavyotaka uonyeshe hisia zako kila siku" (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11**

Mtu akiishakuwa Mkristo, anakabiliana na fursa nyingi za kuonyesha hisia zake. Anaweza kujifunza kukabidhi eneo hili la maisha yake kwa Kristo, au anaweza kuendelea kuitikia kihisia kwa njia anayotaka na kupuuza kile anachosema Kristo. Tunapozungumzia kujitolea hisia zako kwamba ni sehemu ya kuwa Mkristo, hatuzungumzii tu jinsi unavyohisi unapokuwa Mkristo. Inahusu kuweka eneo hili la maisha yako chini ya mamlaka ya Kristo kila siku mpya. Kujitolea kwako wakati wa kuokoka ilikuwa hatua ya kwanza ya kujitolea huku.

Kwa kuzungumzia mada mbalimbali katika sehemu hii ya somo, tunataka mazungumzo yalenge kwenye hayo mabadiliko ya hisia ambayo yanahusiana na kuwa Mkristo, na kudumisha uhusiano wenye nguvu na Kristo. Ukipata muda, unaweza kupanua mazungumzo hayo kwa urahisi.

Wanafunzi wengine wanaweza kuwa wameumia kihisia kutokana na mambo yaliyowapata huko nyuma. Hili ni kweli hasa kwa wale ambao wamenyanyasika kijinsia au kimwili, na wanaotoka katika nyumba zilizokuwa na misukosuko. Tunahitaji kuwa waangalifu sana hapa kwamba tusije tukaonyesha kwamba mazungumzo ya Dakika 15 hapa yatatoa majibu yote wanayohitaji kutatua matatizo yao. Watie moyo kuzungumza na wewe kibinafsi kuhusu mambo magumu yoyote makubwa waliyo nayo katika eneo hili la maisha yao.

**14. Jadili Hoja C-3-a, “Kubali hisia zako ziwe chini ya uongozi wa Yesu Kristo” (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11**

Wengi wetu huhesabu maitikio yetu kihisia kuwa ni sehemu binafsi sana ya maisha yetu: Wewe ni nani uniambie jinsi ninavyopaswa kuhisi? Tunapotoa hisia zetu kwa Kristo, tunasema hivi: “Bwana! Ninakupa uhuru uniambie ninavyopaswa na nisivyopaswa kuitikia kihisia. Ninataka niwe kama nilivyo, lakini ninataka kukupendeza ninapoitikia kwa hisia zangu mazingira yoyote ya kila siku.”

Hii haimaanishi kwamba Kristo atatufanya tuhisi hisia fulani. Hatufanyiki kuwa mashine. Hizo bado ni hisia zetu, nasi tunawajibika kwa njia tunayotikia. Hatuwezi kusema, “Nimetoa hisia zangu kwa Kristo, hivyo, nikikukasirikia, ni kwa sababu Mungu anataka nikutendee hivyo.”

Kazia umuhimu wa kujifunza jinsi ya kutawala hisia zao kwa namna ya ukomavu. Hisia zetu haziwezi kutawala maisha yetu. Kristo lazima awe Bwana katika eneo hili la maisha yetu. Kukabidhi hisia zako kwa Mungu hakumaanishi kukoma kuwa wewe. Kwa kawaida, maana yake ni kwamba itabidi ubadilishe halitabia na mwenendo wako kwa jinsi unavyojieleza na kuonyesha hisia zako. Onyesha kwamba huu utakuwa ni utaratibu endelevu wa ukuaji unaoweza kuchukua majuma mengi, miezi mingi, na hata miaka mingi.

**15. Jadili Hoja C-3-b, “Jifunze kutambua hisia zako kwa usahihi” (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 11-12**

Watu wengi wanapata shida sana kutawala hisia zao. Lakini ukimwuliza mtu huyo alikuwa anahisi vipi kwaDakika Fulani, pengine hata hawezi kusimulia au kueleza anahisi vipi. Kujifunza kutambua kwa usahihi hisia zako ni hatua muhimu sana hapa.

Waulize wanafunzi kuorodhesha hisia mbalimbali. Halafu waambie waeleze mazingira au wakati ambapo wao walihisi hiyo.

Kitabu cha John Powell’s book kiitwacho: *Why Am I Afraid to Tell You Who I Am?*, sura ya 3 na ya 4, kina habari nzuri sana kuhusu hisia. Pengine ni vizuri ushirikishe baadhi ya mawazo yake katika somo hili. Pengine ungependa wanafunzi wako wasome hizo sura.

**16. Jadili Hoja C-3-c, “Jifunze kuwa huru kihisia kwa njia ya maombi” (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 12-13**

Hii ni hatua muhimu sana katika maisha ya kila Mkristo mpya. Kama wataanza kuzungumza na Mungu kuhusu wanavyojisikia, wako kwenye njia sahihi. Watie moyo kusoma Zaburi na kutazama jinsi ambavyo Mfalme Daudi alivyoeleza hisia zake kwa Mungu. Wakiwa wamesongwa na kughafilika, watie moyo kumwambia Mungu wanavyohisi.

Watie moyo kumwomba Mungu ajaze maisha yao na maitikio kihisia ambayo Yeye anataka. Kwa mfano: Wamwombe Mungu awasaidie kuhisi upendo kwa ajili ya mtu wanayepata shida kumpenda. Mwombe Mungu aweke amani kwa mawazo ili kuondoa wasiwasi na hofu ambayo inaingia kwa haraka sana. Mwombe Mungu awawezeshe kuwa na huzuni itakayoondoa hasira wanayohisi kuhusu mtu ambaye amewakosea na kuwatendea yasiyofaa.

**17. Jadili Hoja C-3-d, “Jifunze jinsi ya kuzungumza na wengine kuhusu hisia zako” (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13**

Wengi wetu huwasilisha hisia zetu kwa wengine kupitia kwa jinsi tunavyowaitikia. Waeleze wanafunzi wako kwamba tunataka wajifunze jinsi ya kusema kwa maneno ujumbe wao jinsi wanavyohisi, kwa sauti ya upole. Pengine unaweza kutoa nafasi kwao ya kufanya mazoezi kwa hilo.

Wape mazingira ambayo kwa kawaida wanaweza kuitikia kwa hasira, na uwaulize kuigiza hayo, wakimweleza huyo mwingine jinsi wanavyohisi badala ya kuonyesha hisia hizo kwa maneno ya hasira na matendo. Kitabu cha John Powell kiitwacho *Why Am I Afraid to Tell You Who I Am?*, sura ya 3 na ya 4, hutoa mtazamo mzuri sana juu ya hali hii.

Hebu zungumzeni na wanafunzi wako ni kwa nini ni muhimu kuzungumza na watu wengine juu ya jinsi unavyohisi. Sababu moja ni kuzuia au kutuliza majibizano. Sababu nyingine ni kukuza uhusiano wenye kina, na marafiki au mwanafamilia. Kazia umuhimu wa kujifunza kufanya hivyo na wanafamilia, hasa watoto wako.

Hapa kuna haja ya uwiano. Hatupaswi kuzunguka na “kuacha kila kitu kikining’inia nje”. Kuna nyakati ambapo itikio la ukomavu ni kukaa kimya kutokana na vile tunavyohisi. Kama unahisi kushuka kidogo au kuwa na msongo wa mawazo, huna haja ya kwenda kila mahali huku ukumwambia kila mtu tatizo lako. Lakini, ikiwa huwezi kulishinda mwenyewe, itasaidia sana kuzungumza jambo hilo kwa faradha na rafiki au mwanafamilia.

**18. Jadili Hoja C-3-e, “Jifunze kueleza hisia zako zaidi” (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 13-14**

Tunachotaka watu wapate hapa ni kwamba, Mungu anataka ufurahie ukamilifu wa hisia zote ambazo ameumba na kuziweka ndani yako. Kama Mkristo, una uwezekano mkubwa wa kupata viwango vya kina sana vya amani, furaha, na upendo, kwa msaada wa Kristo.

**19. Jadili Hoja C-3-f, Jihadhari na Wakristo “waliolewa hisia” (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 14**

Kuna tatizo kubwa sana kwa baadhi ya mafundisho wanayopata Wakristo siku hizi. Mkazo mwingi sana umewekwa kwenye “hali ya kuhisi vizuri kutokanan na yale utakayopata kutoka kwa Mungu”. Wanakuahidi upendo, furaha na amani tele. Ikiwa huhisi hivyo maishani mwako, wanaofundisha hivyo wanasema unamruhusu Shetani akuibie vitu hivyo. Wewe watie moyo wanafunzi wako kuchunguza kwa makini sana kinachosemwa na Biblia, si mstari mmoja au miwili iliyoko hapa na pale katika Biblia.

Mungu hatoi ahadi ya “hisia za juu” kila siku kwa Wakristo. Ameahidi kuwa pamoja nawe wakati wote. Na atakusaidia katika nyakati ngumu. Watie moyo kutarajia kuwa vipindi hivyo vya hisia kuwa juu huja na kupita. Hiyo ni sehemu ya kawaida kabisa ya maisha.

2

### 20. Kutendea Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)

Lenga shughuli hii kwa kukubali hisia zako zinazobadilika, na kutozitegemea ili zikuthibitishie kwamba wewe ni Mkristo. Zifuatazo ni kazi-miradi zinazoweza kusaidia ukuaji katika eneo hili la maisha yako.

**A. Omba kuhusu hisia zako**

Kiri juu ya hisia zako kwa Mungu kwa maombi. Amua kumwambia Mungu jinsi unavyohisi kuhusu mazingira magumu unayokabilia nayo. Pia mwambie jinsi unavyohisi juu ya mambo mazuri uliyopitia leo. Ukweli ni kwamba, unaweza kutumia muda kuzungumza na Mungu ukiwa katikati ya wakati mgumu. Kumwambia Mungu jinsi unavyohisi kunaweza kupunguza msongo unaoweza kuwa umeanza kupata nguvu ndani yako.

**B. Kitabu cha taarifa kuhusu hisia zako**

Tunza kitabu kuhusu kumbukumbu zako kwa muda wa juma moja. Jaribu kueleza uhalisia wa hisia zako katika baadhi ya nyakati ngumu ulizopitia siku hiyo, au mchana. Unaweza kutaka kujitathmini mwenyewe kwa kujibu swali hili: Je, niliitikia mazingira husika kwa hisia iliyompendeza Mungu? Vipi kuhusu jinsi nilivyoonyesha hisia yenyewe? Je, ilikuwa ya kumpendeza Mungu?

**C. Kujifunza Biblia kuhusu hisia**

Jifunze Biblia ili upate kujua inasema ni njia zipi bora za kuonyesha hisia zako. Tafuta mawazo ya vitendo kuhusu jinsi unavyoweza kutumia hisia zako kama Mungu anavyotaka.

**D. Makubaliano na rafiki au mtu wa familia**

Fanya makubaliano na mumeo/mkeo au rafiki kwa kuhojiana au kuzungumza kuhusu hisia zinazoonekana kwa kila mmoja. Huku kutoleana taarifa kutatoa nafasi ya kujifunza jinsi ya kuzitambua kwa usahihi hisia za mtu mwingine na jinsi anavyozionyesha. Pia, itawapa nafasi ya kuwa wakweli kuhusu hisia, kwa mtu mnayeaminiana. Kama hilo linatisha sana likifanyika kwa maneno, ana kwa ana, basi ni sawa kabisa kuandika tathmini zenu na kila mmoja akachukua za mwenzake.

**E. Jambo La Kufanyia Utafiti**

Hebu tathmini jambo hili la kufanyiwa utafiti na uamue njia iliyo bora ya kumsaidia mtu huyu apate kuelewa vizuri zaidi jinsi Mungu anavyomtaka aonyeshe hisia zake, na azitumaini kiasi gani.

Hebu badilisha jina katika mfano huu na kuweka la kike ikiwa darasa lako ni la wanawake tu.

Mfano: Edu alifanya uamuzi mbele za watu kumfuata Kristo siku sita tu zilizopita, akamwomba Yesu awe Kiongozi wa maisha yake. Siku mbili za kwanza zilikuwa nzuri sana kwa Edu. Furaha na amani iliyofurika maishani mwake ilikuwa dhahiri kwa wote waliokutana naye.

Lakini jana, dunia yake iliporomoka. Akasikia kwamba mke wake amepanga kumwacha. Anasema hampendi tena. Furaha na amani ya siku chache zilizopita imetoweka kabisa. Hali ya kukata tamaa na kutokuwa na raha imetawala kabisa maisha yake. Edu anakwambia hivi: "Kama Mungu ananipenda kweli, asingeruhusu hayo yatokee kwangu. Kama kuwa Mkristo ndiyo mambo haya, basi sitaki."

Je, ungemwambia Edu kitu gani? Ungetumia mistari gani ya Biblia kumsaidia Edu aone kile ambacho Mungu anafanya maishani mwake? Ungejaribuje kumshawishi Edu aamini kwamba yeye bado ni Mkristo na kwamba Mungu kweli anampenda? Ungempa ushauri gani kuhusu nafasi ya hisia zake katika maisha ya Kikristo?

**21. Kazi Za Kufanya**

A. Mwishoni mwa darasa, toa chemsha bongo juu ya zile kweli 8 unazohitaji kuzijua na kuziamini ili uwe Mkristo. Tazama ukurasa wa 5 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi.

**Hizi ndizo kweli unazohitaji kujua na kuziamini ili uwe Mkristo**

1. Mungu yupo. Waebrania 11:6
2. Biblia ni ya kweli. 2 Timoteo 3:16
3. Nimetenda dhambi kwa kutokutii sheria za Mungu. Warumi 3:23
4. Mungu ananipenda, na alimtuma Yesu Mwanawe wa pekee, aishi na kufa kwa ajili yangu. Yohana 3:16
5. Yesu peke Yake ndiye anayeweza kusamehe dhambi zangu. Matendo 4:12
6. Adhabu ya dhambi ni kifo (kifo cha milele). Warumi 6:23
7. Ni naweza kuokolewa kutokana na adhabu ya dhambi kwa kutubu dhambi zangu kwa Yesu na kumwomba anisamehe. 1 Yohana 1:9
8. Ni naweza kuwa Mkristo kwa kumruhusu Yesu awe Kiongozi wa maisha yangu sasa. Warumi 10:9-10

*Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5*

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 2, *"Hisia"*.

C. Tumia muda mfupi kueleza kwa kifupi Mwongozo Wa Somo Zoezi la 5, *"Andika Hadithi Yako."* Wana muda mrefu wa kufanya kazi-mradi hii, lakini wanahitaji kuanza mara moja. Hakikisha wanaandika hadithi, si taarifa tu yenye kutoa maelezo na habari.

D. Waelekeze wanafunzi kusoma sura ya 2 katika Mwongozo wa Wanafunzi wakijitayarisha kwa kipindi kifuatacho.

2

## 22. Maelezo Ya Ziada

Katika kurasa mbili zinazofuata, kuna maswala mawili yanayoshughulikia hisia. **Je, kweli mtu anaweza kujifunza jinsi ya kuhisi uwepo wa Mungu?** na **Jinsi ya kushughulika na hisia juu ya maisha yako ya kale ya dhambi**.

Ukiwa na muda, unaweza kushughulikia maswala hayo kwa kipindi kimojawapo.

## 23. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu jinsi ya kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizokwenda vizuri?
Ni zipi zilizokuwa ngumu sana kueleweka na wanafunzi wako?
Ni zipi zilizowafaa sana wanafunzi wako?

# Maelezo Zaidi Ya Kumsaidia Mwalimu



## Je, kweli mtu anaweza kujifunza jinsi ya kuhisi uwepo wa Mungu?

Mara nyingi sana Wakristo wapya huchanganyikiwa jinsi Wakristo wa zamani wanavyozungumzia mahusiano yao na Mungu. Wanakwenda kanisani na kumsikia mchungaji akisema, “Wangapi wanasikia uwepo wa Mungu hapa asubuhi ya leo? Mambo ni mazuri hapa!” Sasa, yule Mkristo mpya anatazama huku na huko, akijiuliza anapaswa ahisi vipi.

Hebu watie moyo wao kuwa makini sana juu ya maneno kama hayo. Wafundishe kusimama kwenye ahadi za Mungu katika Biblia. Mungu ameahidi kuwa pamoja nasi wakati tunapokutanika pamoja kumwabudu. Yupo, hata tukihisi hivyo au tusipojihisi hivyo. Hisia si muhimu hata kidogo – cha muhimu ni ukweli kwamba Mungu yupo pamoja nasi au katikati yetu.

Onyesha kwamba watu wengine hujipata wamehusika kihisia kwa urahisi tu katika kundi la watu. Yaani, wanavutwa na “wingi wa watu” au “wanapata midadi” kwa sababu ya watu wengi. Kuna wasemaji wengine ambao ni wataalamu sana katika kuamsha hisia za kundi la watu. Eleza kwamba hilo halipaswi kutafsiriwa kuwa ni “kumhisi Mungu”.

Mfano mwingine unaweza kutumika kusaidia kuweka wazi jambo hili. Unapokuwa nyumbani umeketi na familia yako, je “unahisi” uwepo wa hao wanafamilia wengine? Hebu tuseme kwamba umeketi sebuleni, halafu mtu mwingine anaingia hapo. Unajua kwamba wapo kwa sababu unawaona au kuwasikia. Je, unahisi kuongezeka kwa hisia kwa sababu wameingia chumbani? Kuna wakati unaweza kujisikia hivyo. Ikiwa unajaribu kupumzika na wao wangie wakipiga kelele za kila aina, unaweza mara moja kuhisi hasira ikipanda ndani yako. Au kama wewe ni kijana na rafiki yako wa kike au wa kiume aingie, waweza kuhisi upendo (au mapenzi!) ndani yako.

Lakini, jaribu kufikiri juu ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika leo, na mengi yalikuwa ya kawaida tu. Je, ulihisi badiliko kubwa la kihisia ndani yako kila wakati mtu alipoingia au kutoka chumbani humo? Hapana. Hivyo ndivyo inavyotakiwa iwe – ni SAWA KABISA.

Kwa hiyo, usishangae kwamba hutahisi uwepo wa Mungu kila utakapokuja kanisani. Wakati mwingi unaweza kufanya vitu ambavyo vitarahisisha wewe kuhisi uwepo wa Mungu. Kumwomba, kumfikiria, kusoma Biblia – ni baadhi tu ya mambo yanayoweza kukusaidia kumsikia Yeye na kutambua uwepo Wake.

# Maelezo Zaidi Ya Kumsaidia Mwalimu

2

## Jinsi ya kushughulika na hisia juu ya maisha yako ya kale ya dhambi

Mara nyingi Shetani hujaribu kuwavunja moyo Wakristo wapya kwa kuwashtaki. Atakusaidia kukumbuka jinsi ulivyoshindwa zamani au hata hivi karibuni tu, na kusema, “Kweli ulitenda dhambi. Unatakiwa kuhisi hatia kubwa kwa mambo mabaya yote uliyofanya. Halafu, unajua tena jinsi Mungu alivyo mtakatifu na mkamilifu. Lakini hebu tazama dhambi zako. Umeshindwa vibaya sana na wewe ni mwovu na mwenyedhambi. Hutaweza kamwe kufikia kiwango cha utakatifu wa Mungu.”

Hiyo lawama na kuhukumiwa na Shetani inaweza kumkatisha tamaa Mkristo mpya, na kumfanya aone ni vyema aachane na mambo ya Mungu. Watie moyo wasimame kwenye ahadi za Mungu, hasa 1 Yohana 1:9. Unapoungama dhambi zako, Mungu anakusamehe. Huna haja kuendelea kuungama dhambi hiyo hiyo leo na kesho na kesho kutwa. Kama ulimaanisha ulipotubu mara ya kwanza, imetosha. Mungu atatimiza ahadi Yake kukusamehe.

Shetani atafanya kila anachoweza kukudanganya. “Ikiwa Mungu amekusamehe, kwa nini bado unahisi hatia ya hiyo dhambi? Ni hakika bado unajiona aibu na mwenye hatia kwa ajili ya dhambi hiyo mbaya!” Waambie wanafunzi wakubaliane na Shetani kwamba, kweli walitenda dhambi.

Watie moyo kwa kumwambia Shetani kwamba Mungu alikwishasamehe dhambi hizo, na kwa sasa wanafurahia amani ya kujua kwamba Mungu bado anawapenda. Sasa na waelekeze usikivu wao wote kwa Mungu na kumshukuru kwa upendo Wake na msamaha. Tumia hii kama nafasi ya kumwomba Mungu kuwasaidia wawe na nguvu, na wasianguke kwa dhambi hizo tena. Lakini hata kama watafanya hivyo, wanajua kwamba Mungu atawasamehe kama wataungama kwa moyo wa dhati.

Baadhi ya maumivu kihisia kutokana na maisha yao ya dhambi hapo zamani yanaweza kuhitaji msaada wa mshauri wa Kikristo. Watie moyo wale wenye matatizo makubwa katika siku zao za nyuma watafute msaada kutoka kwa mshauri.

# Somo La 3
## Ushahidi: Biblia Na Roho Mtakatifu



**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Nahitaji kujifunza kumsikiliza Roho Mtakatifu anapozungumza nami. `

**2. Mstari Mkuu: Warumi 8:9 TLR**

Lakini, hamfanyi yale mnayotakiwa kufanya na nafsi zenu za zamani za dhambi. Mnafanya yale ambayo Roho Mtakatifu anawaambia, kama Roho wa Mungu anaishi ndani yenu. Hakuna aliye mali ya Kristo kama hana Roho wa Kristo ndani yake.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa wa 15 hadi 19 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi huendana na somo hili. Tutatumia Mwongozo wa Somo Zoezi la 6, *"Kutafuta Ushahidi"* katika darasa la leo.

**Maandalizi Mapema Ya Mwalimu***

Tafadhali pitia mada namba 4 hadi 8 hapo chini siku chache kabla ya kufundisha somo hili. Utahitaji kufanya maamuzi kadhaa muhimu wakati huu, yatakayoathiri jinsi utakavyopangilia somo hili.

**4. * Uchaguzi wa vipindi viwili vya darasa**

Ikiwa ratiba yako inaruhusu, unaweza kugawa somo hili na kulifundisha kwa vipindi viwili. Somo la kwanza linaweza kushughulikia ushahidi ambao Biblia inao wa kuonyesha kwamba mtu ni Mkristo. Somo la pili linaweza kushughulikia ushahidi ambao Roho Mtakatifu anaotoa, kwamba mtu ni Mkristo. Yafuatayo ni mapendekezo ya Kweli Kuu Za KiBiblia na Mstari Mkuu vinavyoweza kutumiwa na hilo somo juu ya ushahidi wa kiBiblia.

**Kweli Kuu Ya KiBiblia:** Nahitaji kujifunza kutumia Biblia kama chombo kwa ajili ya kukusanya ushahidi unaoonyesha kwamba mimi ni Mkristo.

**Mstari Mkuu:** 2 Timoteo 2:15.

**5.* Mpango Wa Kufundishia Kipindi Kimoja**

Huu mpango wa kufundishia utolewao katika kurasa zinazofuata una mapendekezo ya muda unaohusika katika kufundisha hizo mada mbili (ushahidi kutoka Biblia, na ushahidi wa Roho Mtakatifu) katika kipindi kimoja cha darasa. Ukifundisha hayo katika kipindi kimoja darasani, itakubidi uwe makini sana kutawala jinsi unavyogawa muda wako kwa ajili ya hizo mada mbili.

**6.* Njia mbili za kushughulikia ushahidi wa kiBiblia**

Nusu ya kwanza ya somo hili inalenga ushahidi wa kiBiblia. Kuna namna mbili za kulifundisha somo hili, kutegemeana na ukomavu kiroho wa wanafunzi wako.

**A. Njia Rahisi**

Njia rahisi ni kuitazama Biblia kama chanzo cha maelezo inayotupa sisi habari kuhusu iwapo mtu ni Mkristo au hapana. Tumia muda wa lutosha kuzungumzia mistari hiyo, na kueleza jinsi ambavyo tunaweza kujua ikiwa mistari hiyo ni kweli maishani mwetu.

**B. Nia Yenye Changamoto**

Mtazamo wenye changamoto zaidi kuhusu nusu ya kwanza ya somo hili ni kutafiti jinsi tunavyoweza kuitumia Biblia kama chombo cha kukusanya ushahidi unaoonyesha kwamba mtu ni Mkristo. Elekeza mjadala kwenye haja ya kujifunza Biblia kwa usahihi. Tafuta jinsi tunavyoweza kutafsiri kwa usahihi na kufanyia kazi ahadi za Mungu maishani mwetu na kuona matokeo.

**7.* Tathmini anachojua mwanafunzi kuhusu Roho Mtakatifu**

Kabla hujaanza kufundisha nusu ya pili ya somo hili, yenye kushughulikia ushahidi anaota kwetu Roho Mtakatifu, unahitaji kutathmini kwa makini sana wanachojua wanafunzi wako juu ya Roho Mtakatifu. Ikiwezekana, fahamu hayo yote kabla ya darasa kuanza.

Hakikisha wanaelewa kwamba Roho Mtakatifu ni nafsi, si mzimu au mzuka. Yeye ni Mungu, tena yuko kwenye ngazi moja na Mungu Baba na Mungu Mwana. Wanafunzi wako wanahitaji kuwa na uelewa kiasi fulani juu ya kusudi na huduma ya Roho Mtakatifu siku za leo. Kama hakuna kingine chochote utakachofanikiwa kufanya leo, tungependa wanafunzi waelewe kweli hizo za msingi sana juu ya Roho Mtakatifu.

Huduma na karama za Roho Mtakatifu zinazungumziwa kwa upana zaidi katika somo la *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya* liitwalo *Maisha ya Kikristo yenye mafanikio.*

**8.* Je, ushahidi juu yako unaweza kumfanya asiyekuwa Mkristo aamini?**

Katika kujiandaa kwa ajili ya somo hili, tunahitaji pia kutambua kwa uangalifu sana hali ya moyo ya mtu mwenye mashaka juu ya Mungu na Wakristo. Je, tunaweza kutoa ushaidi ambao hata mwenye mashaka ataona kwamba una thamani halisi? Kama hatuwezi, basi labda hatujafanya kazi nzuri katika kuonyesha hoja zetu. Ni kweli kwamba Roho Mtakatifu lazima afanye kweli hizo kuwa halisi kwa kila mtu, lakini sisi pia tunahitaji kufanya sehemu yetu kwa kuandaa kwa uangalifu sana kesi yenye nguvu kwa ajili ya upande wetu.

## 9. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)

**Mfano wa Kesi Mahakamani**

Hebu waambie wanafunzi watumie mawazo yao unapoelezea mfano huu: Twende pamoja mpaka mahakamani. Kuna kesi inaendelea, na wanasheria wanajitahidi kutetea pande zao katika hiyo kesi, kwa ushahidi wanaotumia. Je, ushahidi ni kitu gani?

Ruhusu wanafunzi kutoa majibu. Pengine utahitaji kuonyesha tofauti kati ya ushahidi, maneno ya kusikia – yaani, habari toka kwa mtu wa pili – na uhakika. Ushahidi husaidia mahakama kufikia uamuzi. Je, ushahidi wenyewe unaaminika? Uthibitisho wa kitu unahitaji ushahidi ulio wazi kabisa kiasi kwamba hakuna maswali yanayobaki mawazoni mwa watu kuhusu ukweli wake.

Baada ya hapo waambie wanafunzi hivi: “Mtu anapokuwa Mkristo, yeye ana ushahidi thabiti kabisa. Ushahidi huu unaonyesha wazi kabisa kwamba mtu huyo ni Mkristo. Kama ungekuwa kwenye kesi, je, ungethibitisha kwamba wewe ni Mkristo? Ni ushahidi gani ungetoa kuthibitisha ukweli wako?”

Ikiwa wanafunzi watajibu swali hili, kubaliana na majibu yao, lakini usiingie katika mjadala mrefu wakati huu. Kama wanafunzi hawataki kujibu kwa maneno swali lako, sema hivi: “Tutatazama baadhi ya ushahidi leo unaoweza kutumiwa kuonyesha kwamba mtu ni Mkristo.”

## 10. Shughuli Ya Vikundi – Kutafuta ushahidi (Dakika 15-25 zitumike kwa shughuli nzima)

### A. Shughuli Ya Kujifunza Biblia Katika Kikundi Kidogo (Dakika 7-10)

Ligawe darasa katika makundi mawili na upange shughuli inayohusu ushahidi wa kiBiblia kwa Kundi A. Lipangie Kundi B shughuli kuhusu jinsi Roho Mtakatifu anavyotoa ushahidi kwamba mtu ni Mkristo. Kama una darasa kubwa, itakuwa vizuri kuligawa katika makundi kadhaa.

Kila kikundi kitazame yale Maandiko yaliyotolewa ukurasa wa 15 hadi 19 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi yanayoendana na shughuli yao. Wape na mistari zaidi ambayo wewe unaona itawasaidia. Toa kwa kila kikundi karatasi kubwa na kalamu aina ya ‘marker pen’. Taarifa zao ziandikwe kwa hiyo karatasi.

**Kundi A** wajibu swali hili: **Ni ushahidi gani unaotolewa na Biblia kuniambia mimi kwamba ni Mkristo?** (Tumia Maandiko yaliyoorodheshwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 5 na 15-17.)

**Kundi B** wajibu swali hili: **Ni ushahidi gani anaonipa Roho Mtakatifu kuonyesha wazi kabisa kwamba mimi ni Mkristo?** (Tumia Maandiko yaliyoorodheshwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 17 hadi 19.)

### B. Taarifa kwa darasa (Dakika 5-10)

Toa nafasi kwa Kundi A watoe taarifa ya mambo waliyogundua kwa darasa zima. Halafu ruhusu darasa wajadiliane kuhusu mada hiyo. Wanafunzi wenye maswali wayaelekeze kwa wanakikundi waliohusika katika hiyo kazi-mradi. Pia unaweza kuliambia darasa lishirikishe majibu waliyotoa kwa swali la 2 katika Zoezi la 6.

Swali hili linawataka waorodheshe mistari miwili ambayo imewasaidia kuelewa hatua za msingi kuhusu jinsi ya kuwa Mkristo.

Toa nafasi kwa kundi B watoe taarifa ya mambo waliyopata baadaye wakati wa darasa, utakapoanza kuzungumza juu ya Roho Mtakatifu. Tazama shughuli #16 iliyoko kwa ukurasa wa 40 katika mpango huu wa kufundishia somo.



**11. Rejelea yale maeneo matatu ya kujitoa (Dakika 5)**

Baada ya Kundi A kumaliza kutoa taarifa yao, na mkiishajadili mambo waliyopata, tumia nafasi hii kufanya marejeleo ya maeneo yale matatu ya msingi kuhusu kujitoa, kama tulivyoyatazama katika vipindi vilivyotangulia. Onyesha uhusiano wa karibu uliopo kati ya ushahidi wa kiBiblia, na kujitoa kwako kiakili wakati wa kuwa Mkristo. Unaweza kutaka kutumia jambo lifuatalo, la kufanyia utafiti, kusaidia wanafunzi wafikiri vizuri juu ya huko kujitoa kwa aina tatu.

## Jambo La Kufanyia Utafiti: Mkristo Mpya, Mwenye Kuamua Mambo Haraka Haraka

Siku chache tu zilizopita, Petro alisikia kwa mara ya kwanza kuhusu mpango wa wokovu. Hakuwahi kuzungumza na Mkristo halisi kabla ya wakati huo kuhusu jambo hilo, kwa hiyo kila kitu kilikuwa kigeni kwake. Alipenda alichosikia, na akaamua kuwa Mkristo. Hiyo ilikuwa kawaida yake Petro – mara nyingi alifanya maamuzi kwa haraka.

Ni siku nne tangu Petro alipoomba sala ya kuwa Mkristo. Tangu wakati huo, amekabiliana na matatizo na shida kuliko kawaida. Anawaza hivi: “Mimi nilidhani Mungu anapaswa kunitengenezea maisha bora. Inaonekana hili jambo la Ukristo si kitu halisi, ni kitu bandia kabisa. Kama kuwa Mkristo kingekuwa kitu halisi, mambo yangekuwa yananiendea vizuri zaidi.”

### Maswali ya kujadiliana:

1. Hebu tumia yale maeneo matatu ya kujitoa tuliyozungumza katika vipindi viwili vya darasa, kutathmini uamuzi wa Petro wa kuwa Mkristo.
2. Je, mtindo wa Petro wa kufanya maamuzi haraka haraka ulikuwa na athari gani kwa kujitoa kwake kiakili kuwa Mkristo?
3. Je, ungempa Petro ushauri gani sasa, ili kumsaidia?

**12. Tafuta jinsi ya kujifunza Biblia**
**(Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 15-16**

Tumesema kwamba Biblia ina kweli zinazokwambia jinsi ya kuwa Mkristo. Tungetaka kusema waziwazi kwamba mistari mingine mingi katika Biblia inaweza kutumiwa kutoa ushahidi kwamba mtu ni Mkristo. Ili hawa Wakristo wapya waweze kuzipata kweli hizo za Biblia na kuzitumia kwa ufanisi, wanahitaji kukuza au kuendeleza njia zinazofaa, za kujifunza Biblia.

Mada hii inashughulikiwa kwa upana sana katika yale *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya*, katika somo liitwalo *Jinsi Ya Kujifunza Biblia.* Ikiwa una muda, zungumza na wanafunzi wako juu ya njia chache tu za msingi za kujifunza Biblia. Hakikisha kwamba wanajua jinsi ya kutumia itifaki ya Biblia ili kutafuta na kupata mistari juu ya mada Fulani.

Waonye kuhusu hatari ya kuondoa mistari ya Biblia katika mantiki yake. Eleza maana yake, na utoe mfano. Tazama ukurasa wa 15-16 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kupata habari zaidi.

Katika kuhitimisha sehemu hii ya somo, onyesha umuhimu wa kujifunza Biblia ili kujua kile ambacho Mungu anasema juu ya mahusiano yetu Naye kama watoto Wake. Ushahidi umekwishatolewa kwetu na Mungu. Ni juu yetu sasa kuupata ushahidi huo na kuufanyia kazi katika maisha yetu.



**13. Jadili Hoja A-2. Ni lazima utii mafundisho yaliyomo katika Biblia (Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 16**

Tunahitaji kuweka wazi kwamba Biblia inatoa ushahidi mwingi kuliko kutaja tu kweli zinazoonyesha jinsi mtu anavyokuwa Mkristo. Kipengele kidogo cha 2 kwenye ukurasa wa 16 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi huonyesha kwamba wakati mtu anapokuwa Mkristo, lazima atii mafundisho ya Biblia. Unapotii mafundisho hayo, unajikusanyia mwenyewe ushahidi binafsi za zaidi kwamba kweli Biblia ni Neno la Mungu. Wengi wetu hatuwezi kutii mafundisho hayo kikamilifu kwa nguvu yetu wenyewe. Ni lazima tupate msaada wa Mungu kufanya hivyo.

Watie moyo wanafunzi kutafuta mistari inayoshughulika na maeneo ya maisha yao ambapo wanataka kukua. Waambie waweke malengo ambayo watayatimiza kwa msaada wa Mungu. Mafanikio hayo yatatoa habari za msingi sana kwa ajili ya ushuhuda binafsi wenye nguvu sana kuhusu jinsi Neno la Mungu lilivyo kweli. Waambie washirikishe mifano hiyo wakati wanapotoa ushuhuda kanisani au wakati wanapowashuhudia watu wasiokuwa Wakristo.

**14. Jadili Hoja A-3. Kweli katika Biblia hazijabadilika (Dakika 3-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 16-17**

Biblia inatoa ushahidi wenye nguvu sana, tena unaoaminika. Tazama ukurasa wa 16-17 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kupata habari zaidi kuhusu hili. Swala hili linashughulikiwa kwa upana zaidi katika yale *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya,* somo liitwalo *Kuitazama Biblia Kwa Haraka,* ambalo ndilo somo linalofuata katika mfululizo huu ikiwa unafuata mtiririko wa kufundisha uliopendekezwa.

**15. Ushahidi unaodai uamuzi (Dakika 2-10)**

Ndugu Josh McDowell ameandika vitabu kadhaa vyenye wingi wa ushahidi kuhusu uhalisia wa Kristo na Biblia. Ifuatayo ni orodha ya baadhi ya vitabu vyake. Unaweza kuwajulisha wanafunzi wako vitabu hivyo na kuwaonyesha jinsi ya kuvitumia kukusanya ushahidi binafsi za ziada juu ya kuwa Mkristo. [Ni vya Kiingereza]

Evidence that Demands a Verdict

More Evidence that Demands a Verdict

More than a Carpenter

Reasons Skeptics Consider Christianity

The Resurrection Factor

Evidence for Faith

**16. Taarifa Ya Kundi B kuhusu Roho Mtakatifu (Dakika 5-10)**

Tambulisha kwa kifupi nusu ya pili ya somo, ukionyesha kwamba Roho Mtakatifu pia anaweza kutoa ushahidi kwamba mtu ni Mkristo. Toa nafasi kwa Kundi B kusema mbele ya darasa walichokipata. Tazama Shughuli #10 kwenye ukurasa wa 37 katika mpango wa somo ili upate maelezo zaidi.

Baada ya wanafunzi kukamilisha taarifa yao, ingia kwa mazungumzo kuhusu dondoo kuu zinazotajwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ukurasa wa 17-19. Ikiwa kundi lilifanya vizuri katika kushughulikia maswala haya, basi endelea na yale ambayo ungetaka kuyazungumzia kwa upana zaidi.

**17. Jadili Hoja B-1. Roho Mtakatifu atakuja na kukaa ndani yako**
**(Dakika 5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 17**

Hili jambo linashughulikiwa vizuri zaidi katika ukurasa wa 17 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi. Kwa faida ya darasa zima, ni vizuri usome na kuzungumzia baadhi ya Maandiko yaliyotajwa kwenye mada hii. Weka wazi wakati Roho Mtakatifu anapokuja na kukaa ndani ya mtu – ni ule wakati wa wokovu. Je, anakaa wapi? Ndani ya roho zetu. Eleza mahali roho yako ilipo. (Na ufurahie muda huo!) Tumia hili swali la mwisho kuingiza darasa kwenye mjadala kuhusu mada kuu inayofuata:
*Kwa nini Roho Mtakatifu anakuja na kukaa ndani yako baada ya wewe kuwa Mkristo?*

**18. Jadili Hoja B-2. Roho Mtakatifu atakuwa Mwalimu wako**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 17-18**

Kwa kifupi zungumzia majukumu ya Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo.

Tulitaja mwanzoni mwa mpango huu wa kufundishia somo kuhusu haja ya kuwa makini juu ya wanafunzi wetu na kupima uelewa wao juu ya Roho Mtakatifu. Kama wanafunzi wako wana uelewa mdogo au hawana kabisa juu ya maswala hayo, hakikisha kwamba unatumia muda wa kutosha kueleza kwa kifupi Roho Mtakatifu ni nani. Hakikisha wanafunzi wako wanaelewa kwamba Yeye ni Mungu.

Unaweza kutaka kuzungumzia kwa kirefu zaidi jibu la swali hili:
***Roho Mtakatifu anakufundishaje?***

Orodhesha majibu yao kwenye ubao. Hatufundishi kama mwalimu anavyofundisha akiwa amesimama mbele ya darasa, wala hatutumii barua maalum. Mara nyingi anatumia Biblia pamoja na watu wanaotuzunguka, naye anasimama karibu nasi ili kutuongoza katika kweli, kwa “sauti” Yake “ndogo, tulivu”.

**19. Roho Mtakatifu husema nasi kwa njia gani?**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 18-19**

Wanafunzi watoe mawazo yao na kuyajadili, jinsi wanavyoweza kumsikiliza Roho Mtakatifu, na jinsi wanavyoweza kujua wakati anapozungumza nao. Unaweza kuweka swali lifuatalo kwenye ubao, kisha uorodheshe majibu yao. Swali hili ni:
***Je, Roho Mtakatifu anazungumzaje na wewe?*** Hapa mnaweza kuzungumza kuhusu majibu waliyotoa kwa swali la 4 na 5 kutoka kwa Zoezi la 6 katika Mwongozo Wa Somo.

**Swali La 4: Roho Mtakatifu anamwambiaje mtu kwamba ni Mkristo?**

**Swali La 5: Unatakiwa kuitikiaje yale unayoambiwa na Roho Mtakatifu?**

Ruhusu tofauti za majibu ya wanafunzi. Sisitiza kwamba Roho Mtakatifu hushuhudia na roho yetu kutuambia kwamba sisi ni watoto wa Mungu. Ni mara chache sana Wakristo husikia Roho Mtakatifu akisema nao kwa sauti, kama watu wanavyowasiliana au kuzungumza. Roho Mtakatifu husema nasi kupitia kwa roho zetu; hayo mawasiliano ni swala la ndani.

Pengine itakuwa vizuri kuzungumzia swali hili pamoja na baadhi ya watumishi wengine hapo mnapofanya huduma, au na mchungaji wako, ili kupata mawazo mengine zaidi jinsi Roho Mtakatifu anavyosema nao.

Mara nyingi Wakristo wapya watakuwa na mashaka kuhusu hali yao halisi, kama ni Wakristo wa kweli au hapana. Mawazo yataingia akilini mwao. Ni vizuri sasa mzungumzie maswali haya kama una muda. Kama huna, taja kwa kifupi tu jambo hilo na kueleza kwamba tutalishughulikia zaidi katika sura ya nne ya somo hili, tunapozungumzia juu ya mashaka.

1. Ninajuaje ni Roho Mtakatifu anazungumza, au kama ni mawazo yangu tu?
2. Je, kuna njia isiyo na makosa kabisa ya kujua wakati Roho Mtakatifu anapozungumza, tofauti na wakati mawazo mengine yanapoingia akilini mwangu, yasiyotokana na Roho Mtakatifu?
3. Ninawezaje kujua wakati Shetani anapotia mawazo kwa akili zangu? (Kumbuka, Shetani atakuja akijifanya ni malaika wa nuru.)

Kwa kujadili maswali haya, tunahitaji kuwasaidia waone kwamba kumsikiliza Mungu ni eneo ambalo kuna nafasi kubwa ya kukua katika miaka ya mbele. Tazama ukurasa wa 19 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi kwa maelezo zaidi juu ya mawazo matano yanaweza kutumiwa kuamua kama ni Roho Mtakatifu anazungumza na wewe.

Sisitiza haja ya kupata uwiano huo katika kushikilia mawazo yetu na kutazama maeneo mengine ya maisha yetu ya Kikristo. Tunayo Biblia, ambayo ni ujumbe dhahiri kabisa kutoka kwa Mungu ambao hauathiriwi na uwezo wetu wa kusikiliza mawazo yetu. Tunaweza kusoma Biblia na kujua kwamba ni Neno la Mungu.

**20. Jadili Hoja B-4. Mtu anawezaje kuwa msikivu zaidi kwa sauti ya Roho Mtakatifu? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 18-19**

Ikiwa una muda, na wanafunzi wamekomaa kiasi cha kutosha kufaidika na mjadala, zungumzia jinsi unavyoweza kuwa na usikivu zaidi kwa sauti ya Roho Mtakatifu. Hakikisha wnaelewa ni kwa nini Roho Mtakatifu huzungumza nasi.

Mara nyingi, Roho Mtakatifu huzungumza nasi kupitia dhamiri zetu. Unaweza kuzungumzia dhamiri ni kitu gani na jinsi dhambi zinavyoiathiri. Onyesha hitaji la sisi kama watoto wa Mungu kujifunza jinsi ya kuwa wasikivu kwa dhamiri yetu.

**21. Kutendea Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)**

Kuna kazi-miradi kadhaa iliyopangwa hapo chini, kwa ajili ya kutendea kazi somo maishani. Chagua moja au zaidi, unayoona inaweza kuwa msaada kwa wanafunzi wako.

**A. Andika karatasi moja kuhusu Roho Mtakatifu**

Wape wanafunzi kazi ya kuandika kiasi cha karatasi moja, wakieleza uhusiano wao na Roho Mtakatifu. Wafikiri vizuri na kujibu maswali yafuatayo katika uandishi wao.

1. Je, Roho Mtakatifu amezungumza na mimi au hapana?
2. Je, Roho Mtakatifu amanifundisha kitu chochote?
   Kama ndiyo, nini mfano mmoja?
   Pia, orodhesha maeneo katika maisha yako ambapo ungependa Yeye akufundishe.
3. Nawezaje kumsikiliza Roho Mtakatifu kwa ukaribu sana?

**B. Jambo La Kufanyia Utafiti Kuhusu Mkristo Mpya**

Taja hili lifuatalo, na uwaambie wanafunzi wajibu maswali yao kwenye karatasi:

Rafiki yako mpya hivi karibuni ameonyesha shauku kubwa ya kutaka kuwa Mkristo. Huyu mtu ameomba na wewe, na kumkaribisha Yesu maishani mwake, na kumtaka amwokoe. Rafiki yako amekuwa akipitia matatizo mazito hivi karibuni. Anakwambia hivi: “Sidhani mimi ni Mkristo. Kwa sababu, kama ningekuwa Mkristo, sidhani Mungu angeniruhusu nipitie haya matatizo yote ninayopitia.” Je, utamtiaje moyo rafiki yako ambaye hana hakika tena ikiwa ni Mkristo au hapana?

Baada ya wanafunzi kuandika majibu yao, unaweza kuzungumzia baadhi ya majibu yao ili yajadiliwe na darasa zima.

**C. Kitabu cha kumbukumbu ya ushuhuda binafsi kwamba ni Mkristo**

Wape wanafunzi changamoto ya kupima ahadi za Mungu na kuona kama zinafanya kazi maishani mwao. Waambie watunze kitabu cha kumbukumbu kuhusu mambo maalum ambayo Mungu amewatendea. Waandike mifano ya pale walipoona Mungu akitimiza ahadi Zake kwao. Unaweza kuwaambia watumie wakati huu kuandika kitu cha kwanza katika kitabu chao hicho.

### D. Orodha ya matatizo yaliyoko sasa

Kazi-mradi hii ya kufanya kazi somo kibinafsi inahusu kujifunza kumtumaini Roho Mtakatifu zaidi katika shughuli zao za kila siku. Waambie waorodheshe matatizo wanayokabiliana nayo juma hili, hasa yale ambayo hawawezi kuyatatua kwa busara wala akili zao au hata nguvu zao wenyewe. Waambie watafute mistari inayohusiana na matatizo hayo, kisha wamwombe Roho Mtakatifu awape hekima kujua mahali pa kuanzia kushambulia kila tatizo.

## 22. Kazi Za Kufanya

A. Mwisho wa kipindi cha darasa, toa chemsha bongo itokanayo na Warumi 8:16.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 3, *“Kujitoa Kwa Ajili Ya Yesu Kristo”*.

C. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 4, *“Mawasilisho Ya Maeneo Matatu Ya Kujitolea”*, leo au baada ya kipindi cha darasa kinachofuata.

D. Wanafunzi wasome Sura ya 2 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kufanya marudio ya mazungumzo ya darasani leo, na kujiandaa kwa ajili ya kipindi.kifuatacho cha darasa.

## 23. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 4
## Ushahidi: Mabadiliko Katika Maisha Yako



**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Ninahitaji kushirikiana na Mungu kufanya mabadiliko katika maisha yangu ya kila siku, yatakayonisaidia kumkaribia Mungu.

**2. Mstari Mkuu: Wafilipi 1:6 TLR**

Nina hakika kwamba Mungu aliyeanzisha kazi njema ndani yenu ataendelea kufanya kazi ndani yenu mpaka siku Yesu Kristo atakapokuja tena.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Ukurasa wa 20-26 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi huendana na somo hili. Mazoezi yafuatazo katika Mwongozo Wa Somo pia yatatumika kwa pamoja na somo hili.

Zoezi la 3, *Kujitoa Kwa Ajili Ya Yesu Kristo*

Zoezi la 4, *Mawasilisho Ya Maeneo Matatu Ya Kujitolea*

Zoezi la 6, *Kutafuta Ushahidi*

Zoezi la 7, *Waulize Wakristo Wengine Ushahidi*

**4. Zoezi la utangulizi wa somo (Dakika 5)**

**A. Hadithi ya kijana wa kiume aliyeingizwa jeshini**

Soma ile hadithi ya kijana wa kiume aliyeingizwa jeshini ambaye hakumwambia mtu yeyote kwa miaka miwili kwamba yeye ni Mkristo. Habari hii inatoka kwa kitabu kiitwacho *The Mind Changers*, kilichoandikwa na Em Griffin (na kuchapishwa na Tyndale House Publishers, mwaka wa 1976), ukurasa wa 207. Imetumiwa kwa kibali maalum. Tafsiri ya kisa hicho inafuata hapa chini.

{Kuna habari tamu lakini chungu juu ya mvulana mmoja kutoka vilimani West Virginia, aliyeingizwa jeshini. Jamaa huyu alikuwa amelelewa katika kanisa dogo, lililofichika, na yeye pamoja na washirika wenzake wote kanisani walikuwa na wasiwasi juu ya mvulana huyo, kwamba atakapokutana na mambo ya dunia atapoteza imani yake. Wakamfanyia ibada ya maombi ya mkesha usiku ule kabla hajaondoka kwenda kambini kwa mara ya kwanza. Yule kijana hakuandika barua nyumbani kwa miaka miwili yote alipokuwa jeshini. Basi siku aliporudi, washirika wote walikusanyika kumwona wakiwa na shauku kubwa. Wakamwuliza, “Mambo yalikuwaje huko? Uliweza kuitunza imani yako?” Kijana akajibu kwa msisimko mkubwa, “Ni hivi jamani: Kweli niliogopa sana. Lakini maombi yenu yalisaidia, na mambo yakaniendea vizuri tu. Nilikuwa jeshini kwa miaka miwili yote na hakuna mtu yeyote aliyegundua kwamba mimi ni Mkristo!”}

Eleza kwa kifupi kwamba leo tutazungumzia juu ya mguso wa maisha yetu mapya katika Kristo kwenye mawazo yetu, hisia, na mwenendo.

**B. Marudio ya yale maeneo matatu ya kujitoa**

Baada ya kushirikisha hiyo hadithi hapo juu, waulize wanafunzi kutathmini kiwango cha kujitoa kwa huyo kijana kwa habari ya mahusiano yake na Mungu. Kisha mwulize mmoja au wawili kati ya wanafunzi, kushirikisha darasa majibu yao waliyotoa kuhusiana na **Zoezi la 4,** ***Mawasilisho Ya Maeneo Matatu Ya Kujitolea***, kutoka kwa Mwongozo Wa Somo. Ni matumaini yetu kwamba wanafunzi wameanza kugundua umuhimu wa kujitoa kwao katika hayo maeneo matatu ya maisha yao.

**5. Kutambulisha mada ya leo ya mabadiliko ya maisha (Dakika 5)**



Kwa ajili ya kuhamia kwa sehemu inayofuata ya somo, onyesha kwamba kujitoa anakofanya mtu wakati anapokuwa Mkristo ni lazima kuguse au kuathiri maisha yake ya kila siku. Leo tutazungumzia mabadiliko yanayotakiwa kuanza kufanyika katika maisha yao baada ya kuwa Wakristo.

Itakuwa vizuri kushirikisha darasa kwa maswali manne yafuatayo. Msijaribu kuyajibu sasa. Katika kipindi chote cha darasa, tutajaribu kushughulikia mada hizo.

- Ni mabadiliko gani yanayotakiwa kutokea maishani mwangu?
- Kwa nini mabadiliko hayo yatokee?
- Hayo mabadiliko yanatoa ushahidi gani kwamba mimi ni Mkristo?
- Nawezaje kufanya mabadiliko hayo yatokee maishani mwangu?

Pengine utengeneze bango kubwa lenye maswali hayo manne, na kuliweka ukutani mbele ya darasa ili lilejelewe wakati wote mtakaokuwa mnajifunza somo la leo.

**6. Jambo La Utafiti kuhusu Zakayo (Dakika 5-10)**

Wanafunzi wasome habari ya Zakayo katika Luka 19:1-10. Kabla ya kumruhusu mwanafunzi mmoja asome Maandiko hayo kwa sauti, waambie waone jinsi Zakayo alivyobadilika baada ya kuwa Mkristo.

Yafuatayo ni maswali ya majadiliano yanayoweza kutumika, baada ya Maandiko kusomwa:

1. Ni nini kilichokuvutia tulipokuwa tunasoma habari hii?
2. Ni mabadiliko gani hasa ambayo Zakayo aliahidi kuyafanya baada ya kuwa Mkristo?

Onyesha kwamba hakuna yeyote kati yetu aliye katika hali kama ya Zakayo. Lakini Mungu anapendezwa anapoona sisi tukifanya mabadiliko hayo yatakayotoa ushahidi wa wazi kwetu na kwa wegnine kwamba kweli tumekuwa Wakristo.

**7. Tayarisha orodha ya mabadiliko (Dakika 5-10)**

Waambie wanafunzi kukupa orodha ya mabadiliko ambayo yametoka maishani mwao tangu walipokuwa Wakristo. Weka orodha hiyo ubaoni au ibandike ukutani. Wanafunzi warejelee majibu yao katika Zoezi la 3, swali la 6 na la 7, pamoja na Zoezi la 6, swali la 8. Msiingie kwa mjadala mrefu juu ya kila wazo linalotajwa. Itengeneze orodha kwa namna ambayo wanafunzi wote wataanza kuelewa mambo halisi ya kimatendo tunayotaka kushughulikia leo.

Zoezi la 3, Swali la 6.
**Ikiwa umekuwa Mkristo, umeyaona mabadiliko yoyote katika maisha yako?**
**Ndiyo Hapana Sina Hakika Ikiwa umeona mabadiliko, ni yapi hayo?**

Zoezi la 3, Swali la 7,
**Je, mabadiliko katika maisha yako yanakufanya kuwa Mkristo?**
**Ndiyo Hapana Sina Hakika Fafanua jibu lako.**

Zoezi la 6, Swali la 8,
**Ni mabadiliko gani uliyoyaona maishani mwako tangu uwe Mkristo?**

**8. Je, nibadilike upesi kiasi gani? (Dakika 5)**

Jambo moja linaloweza kuleta majadiliano marefu ni kuhusu mtu afanye mabadiliko gani upesi na kwa kiasi gani. Kwa mfano: Kama mtu ameandika “kuacha kuvuta sigara” kuwa mojawapo ya mabadiliko, unaweza kutumia hilo kama mfano wa hoja hii.

1. Je, ni lazima uache kuvuta sigara *kabla ya* kuwa Mkristo?
2. Je, inabidi kuacha kuvuta sigara ndani ya siku moja au mbili baada ya kuwa Mkristo?
3. Je, unaweza kuendelea kuvuta sigara kwa miezi au miaka kadhaa baada ya kuwa Mkristo?
4. Je, Mungu anataka tubadilishe tabia fulani wakati gani hasa?

Usihisi kulazimika kutoa jibu la kiBiblia lililo wazi kwa maswali haya, kuhusu jambo la kuvuta sigara. Onyesha kwamba tunachotaka watu wapate ni hiki:

1. Je, Mungu anaamini hili ni badiliko la muhimu sana ninalotakiwa kufanya? Au je, Mungu anajali zaidi kwamba nishughulikie mabadiliko mengine kwanza?
2. Je, Mungu anataka nianze kushughulikia mabadiliko katika eneo hilo la maisha yangu wakati gani?

   Tunahitaji kugundua yale Mungu anayoyapa umuhimu. Tunawezaje kufanya hivyo? Tunaweza kuomba, kusoma Biblia na kutafuta ushauri wa Wakristo waliokomaa, na wa zamani.

Inaonekana kuna vipindi vitatu tofauti vya kutafakari katika kufanya mabadiliko hayo. Kila kipindi kinajadiliwa kwa kirefu zaidi hapo chini.

1. Mabadiliko kabla ya, au wakati wa, wokovu
2. Mabadiliko yanayohitaji kufanyika mara tu baada ya mtu kuwa Mkristo
3. Mabadiliko yanayokuja baadaye katika maisha ya Mkristo

### 9. Mabadiliko kabla ya, au wakati wa, wokovu (Dakika 3-5)

Wakati mwingine mabadiliko yanaonekana kuwa sehemu muhimu ya kuwa Mkristo. Badiliko lisipotokea wakati wa wokovu au hata kabla ya hapo, mtu anaweza kuwa na maswali ikiwa kweli tukio la wokovu ni halisi.

Ifuatayo ni mifano michache ya mabadiliko ambayo hutokea mara kwa mara, kabla ya, au wakati wa kuokoka:

1. Pepo kutolewa kwa mtu aliyepagawa – yule mtu wa Gerasi katika Luka 8:26-39
2. Paulo aliacha kuwatesa Wakristo, Matendo 9:1-22
3. Mtu aliyelewa mihadarati (au, dawa za kulevya). Si lazima waachane na ulevi huo siku hiyo hiyo, lakini kama bado wamelewa na madawa, mtu anaweza kuwa na mashaka kama kweli wanajua wanachokifanya. Tunapozungumza juu ya kujitoa akilini ili kuwa Mkristo, nadhani ni salama kusema kwamba mtu huyo lazima awe katika akili zake timamu, si katika ulevi wa dawa za kulevya.
4. Mtu akiwa amelewa vileo. Kimsingi, dhana ile ile ya mtu aliyelewa mihadarati inahusika hapa. Kuna viwango tofauti vya ulevi, hivyo hatuwezi kuweka msimamo hapa. Lakini hoja kuu ni kwamba, toba za aina hiyo au kiwango hicho hazidumu.

Ikiwa mtu ataomba kuwa Mkristo akiwa mlevi wa madawa au vileo, unapaswa kupanga kuzungumza naye tena juu ya jambo hilo tangu mwanzo hadi mwisho, atakapokuwa ametoka katika ulevi wake. Haikubaliki kujaribu kumsukuma au kumbana atekeleze ile sala aliyoomba akiwa mlevi. Mtie moyo huyo mtu kwa mara nyingine tena kufikiri sana juu ya uhitaji wake wa wokovu, kisha mwombee tena ili kuthibitisha kile walichokiomba saa machache zilizopita, au siku chache zilizopita.

### 10. Mabadiliko yanayohitaji kutokea mara moja baada ya mtu kuwa Mkristo (Dakika 3-5)

Kuna matatizo na tabia ambazo zinahitaji kubadilishwa mara tu mtu anapokuwa Mkristo. Mtu akichelewa zaidi kubadilisha eneo hilo la maisha yake, ndipo uwezekano unavyozidi kuwa mkubwa kwamba tatizo hilo litaharibu maisha mapya aliyopata ndani ya Yesu Kristo. Hayo mabadiliko yanaweza kuwa magumu kuyafanya, lakini huyo mhusika akifanya mapema zaidi, ndivyo atakavyokua kwa upesi kiroho.

Katika Matatizo hayo, kuna yale yanayofikia mahali pa Mungu kusema, “Kama haupo tayari kuachana na eneo hilo la maisha yako, basi unachosema ni kwamba Yesu si Bwana kamili wa maisha yako yote.” Sasa, kama Kristo hawezi kuwa Bwana wa maisha yako yote, basi hawezi kuwa Bwana kabisa. Ifuatayo ni mifano michache tu:

1. Yesu alimwuliza yule kijana tajiri aachane na fedha zake zote na kumfuata. Tazama Mathayo 19:16-30. Hatuwezi kusema kwamba lazima kila mtu aachane na fedha zake ili kumfuata Yesu. Lakini kwa watu wengine, pamoja na huyu mtu wa Mathayo 19, fedha zinaweza kuwa “mungu” katika maisha yao.
2. Zakayo alifanya marejesho kuhusu wizi wake wa siku za nyuma. Luka 19:1-10
3. Mtu anayetumia mihadarati au kileo.
4. Mtu anayejihusisha katika shughuli zilizo kinyume cha sheria (zinazohalifu sheria za nchi yake, ambayo ni kinyume kabisa na amri ya Mungu kwamba tutii mamlaka).
5. Chuki ya ndani sana juu ya mtu fulani au kundi la watu.

**11. Mabadiliko yatakayokuja baadaye katika maisha ya Mkristo (Dakika 3-5)**

Kuna baadhi ya mabadiliko ambayo Mungu hataanza kumhukumu mtu juu yake mpaka baada ya miezi au hata miaka ya kuwa Mkristo. Kadiri mtu anavyoendelea kumfuata na kumtumikia Yesu Kristo, ndivyo naye Roho Mtakatifu atakavyomfundisha. Wakati mwingine Mungu yuko tayari kusubiri muda mrefu kabla ya kuanza kudai mabadiliko. Ifuatayo ni mifano michache:

1. Hali ya ubaguzi aliyokuwa nayo Petro, kuhusu watu Wasiokuwa Wayahudi, kwa habari ya hitaji la kuwahubiria Injili. Tazama Matendo 10:1 hadi Matendo 11:18.
2. Matatizo mengine si dhambi, lakini yanaweza kukuvuta chini kiroho na kukuibia furaha ambayo Mungu anataka uwe nayo – wasiwasi, hasira, kutochukuliana na wanafamilia, kiburi na majivuno, au kutosamehe. Wakati mwingine Mungu anaweza kudai ufanye mabadilio mazuri kimtazamo katika maisha yako, kama vile kuwa mkarimu kwa wengine, kuwa mvumilivu, mwenye kusamehe, na mwenye rehema.

4

Tofauti kati ya fungu la pili na la tatu si sawa kwa kila mmoja. Roho Mtakatifu anaweza kumwonyesha hatia mtu mmoja na kumwambia abadilike mara moja, lakini kwa mwingine anaweza kungojea miezi kadhaa au hata miaka. Ukweli ni kwamba, Roho Mtakatifu anaweza hata asimwonyeshe mtu mwingine hatia kabisa. Si kazi yetu kufanya kazi ya Roho Mtakatifu. Sisi tunahitaji kuwa makini tusilazimishe mitazamo yetu kwa wanafunzi wetu.

**12. Je, nikibadilika, bado nitabakia kuwa “mimi”? (Dakika 5)**

Wakristo wengine wapya wanaweza kupinga mabadiliko kwa sababu wanahisi kama unajaribu kuwalazimisha kuwa mtu mwingine. Mungu hawataki wawe wasanii na kujifanya ni mtu mwingine. Mungu hataki kila Mkristo mpya abadilike na kuwa kama Billy Graham. Sasa basi, ni nafasi gani inayobakia ya “kujitambua mwenyewe” katika utaratibu huu wa kufanya mabadiliko yote haya?

Daktari Gary Collins amefanya kazi nzuri sana ya kushughulikia jambo hili katika kitabu chake kiitwacho *How to be a People Helper*, ukurasa wa 201 hadi 204. Anaonyesha jinsi Kristo anavyotakiwa kuwa katika nafasi ya uongozi kamili wa maisha yako, lakini, anatenda kazi kupitia nafsi yako kuonyesha matunda Yake maishani mwako. Wakati mwingine mtu anaweza kuwa amejifungamanisha na tabia fulani au shughuli fulani. Mfano ni kutawaliwa na mihadarati. Anaweza kujiuliza hivi: “Mimi najua nimetawaliwa sana na mihadarati. Nikiachana na hilo, nini kitabakia maishani kwa ajili yangu?” Onyesha kwamba Mungu anataka umgundue yule “wewe halisi” aliye ndani yako. Anataka uache kujificha na kujidanganya, na ujifunze kuwa mtu mkweli na wa dhati.

**13. Nani anayebadilisha – Mungu au mimi? (Dakika 5-10)**

Jambo lingine gumu kuelewa ni kwamba, ni ipi nafasi ya Mungu na ni nini wajibu wangu katika kuleta hayo mabadiliko yanayohitajika maishani mwangu. Unaweza kuchukua mfano mmoja au miwili na kuzungumzia sehemu ya Mungu ni ipi, na sehemu yako ni ipi. Chora mstari katikati ya ubao au kwenye karatasi ngumu. Upande mmoja uandike *Sehemu ya Mungu* na upande wa pili uandike *Sehemu Yangu.*

Kujaribiwa kufanya dhambi ni tatizo la kawaida, na unaweza kutaka kulitumia katika mfano huu. Maandiko kadhaa yanatoa majibu ya kuweka kila upande. Yakobo 4:7-8 hutaja mambo kadhaa ambayo wewe lazima ufanye, na jambo moja ambalo Mungu atafanya. 1 Wakorintho 10:13 hutoa mawazo zaidi kwa ajili ya pande zote mbili.



**14. Jadili Hoja C. Mabadiliko katika maisha yako (Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 20-26**

Hapa itakubidi upitie yale mabadiliko sita ya msingi yaliyotajwa katika ukurasa wa 20-26 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Jaribu kuonyesha mfano wa kila dondoo kutoka maishani mwako, au wape nafasi wanafunzi watoe mifano ya kila dondoo. Jaribu kueleza ni kwa nini mabadiliko haya yanahitaji kutokea katika maisha ya Mkristo.

Jambo moja linalohusiana na dhambi linapaswa kujadiliwa kwa habari ya badiliko la nne, kwamba ***Utapata majaribu mengi, vishawishi, na matatizo***. Weka wazi tofauti kati ya kutenda dhambi na kuishi katika dhambi. Maandiko mawili: 1 Yohana 1:9 na 1 Yohana 3:5-10 yanazungumzia jambo hilo. Yeye atendaye dhambi kwa makusudi, na kufanya akiwa na hali kwamba “Sijali Mungu anachosema”, yuko katika shida kubwa, hasa ikiwa ataendelea kuwa na hali hiyo mwezi baada ya mwezi. Hii ni tofauti sana na yule mtu anayetenda dhambi katika muda wa udhaifu, kama Petro alivyofanya siku ile Yesu aliposulubiwa. Tunazungumza juu ya tofauti kati ya kushindwa na mtu ambaye wakati wote anatenda dhambi kama tabia yake, na wala hajali au hataki kufanya mabadiliko yoyote.

**15. Igizo kuhusu kesi mahakamani (Dakika 5-10)**

Itafaa kama wanafunzi wataigiza kesi mahakamani. Hebu jifanyeni kwamba Mkristo yuko kwenye kesi. Atoe ushahidi wa kuonyesha wazi kabisa kwamba yeye ni Mkristo. Yule wakili anayeendesha mashtaka ajaribu kuthibitisha kwamba huyo si Mkristo. Malizia sehemu hii ya somo kwa kuwauliza wanafunzi wote, “Kama utapelekwa mahakamani na kushtakiwa kwamba wewe ni Mkristo, utakuwepo ushahidi wa kutosha kukutia hatiani?”

**16. Jadilianeni matokeo ya mapitio ya Zoezi la 7 (Dakika 3-10)**

Ukiwa na muda, wape nafasi wanafunzi wachache kutoa taarifa ya kile walichojifunza walipokuwa wanamalizia Zoezi la 7, *Waulize Wakristo Wengine Ushahidi.*

4

## 17. Kufanyia Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)

### A. Weka mpango kwa ajili ya mabdiliko binafsi

1. Ikiwa wanafunzi hawajafanya hivyo bado, basi wakati huu wape nafasi ya kutayarisha orodha ya maeneo kadhaa ambayo wanahitaji kubadilika.
2. Kila mwanafunzi achague, baada ya maombi, maeneo matatu makuu, wanayohisi kwamba ndiyo yenye kuhitaji mabadiliko muhimu sana, ya kufanyia kazi. Yapewe namba – 1 hadi 3 – na namba 1 iwe ndiyo yenye kipaumbele cha kwanza. Halafu, kila mwanafunzi aandike jambo moja au mawili watakayofanya juma hili katika kutekeleza sehemu yao ya kuleta mabadiliko katika hilo eneo husika maishani. Sisitiza haja ya kutafuta msaada wa Mungu wa kufanya mabadiliko haya.

Yafuatayo ni maswali ya ziada unayoweza kuwapa ili watafakari zaidi na wajifunze:

1. Kwa nini ninahitaji kubadilisha eneo hili la maisha yangu?
2. Mungu anasema nini katika Biblia kuhusu jambo hili?
3. Nini sehemu yangu katika kuleta mabadiliko husika?
4. Mungu ameahidi kufanya nini kunisaidia kubadilika katika eneo hili?
5. Je, badiliko hili litafanya nini katika ukuaji wangu Kikristo?
6. Nifanyeje ili badiliko hili liwe sehemu ya kudumu maishani mwangu?
7. Je, badiliko hili litagusaje mahusiano yangu na marafiki zangu (Wakristo na wasio Wakristo)?

### B. Igizo la fursa ya kushuhudia

Hebu mwanafunzi mmoja ajifanye kwamba anamshuhudia rafiki yake ambaye si Mkristo. Huyo rafiki anauliza, “Ni mabadiliko gani yametokea maishani mwako tangu uwe Mkristo?” Mwanafunzi na amjibu.

### C. Waanzie wapi kufanya mabadiliko?

Ikiwa wanafunzi wako wanapata shida kuamua mahali pa kuanzia kufanya mabadiliko, watie moyo kujaribu mfumo huu:

1. Anza kwa mazingira katika maisha yako ya kila siku inayoleta hali ya kubanwa na usumbufu zaidi.
2. Tambua maeneo ambayo unahitaji kukua, ambayo yameonekana kutokana na mazingira yanayokubana na kukusumbua.
3. Orodhesha mistari ya Biblia yenye kukwambia vitu unavyoweza kufanya ili ukue katika maeneo hayo ya maisha yako.
4. Weka lengo la kitu kimoja au viwili unavyoweza kufanya katika siku chache zijazo ili ukue katika eneo hili la maisha yako.
5. Baada ya kufanya kazi ya kutekeleza lengo lako, fanya tathmini ya matokeo na uone umesaidika kiasi gani. Halafu, weka lengo jipya kwa ajili ya ukuaji zaidi.

**18. Kazi za kufanya**

A. Baada ya darasa, toa ile chemsha bongo ya Yohana 1:12.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 4, *“Mawasilisho Ya Maeneo Matatu Ya Kujitolea”*, ikiwa hukufanya hivyo mwishoni mwa kipindi kilichopita.

C. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 6, *“Kutafuta Ushahidi”*.

D. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 7, *“Waulize Wakristo Wengine Ushahidi”*. Pengine itakubidi kusahihisha hii baadaye ikiwa wanafunzi wako bado hawajapata nafasi ya kuwasiliana na watu wanaowahitaji kwa ajili ya kazi-mradi hii.

E. Waelekeze wanafunzi kusoma sura ya 3 katika Mwongozo wa Wanafunzi wakijitayarisha kwa kipindi kifuatacho.



**19. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa**

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 5
## Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu Kristo



### 1. Kweli Kuu Ya KiBiblia

Nahitaji kugundua njia zenye manufaa za kukuza uhusiano wangu na Yesu, wa binafsi na wa karibu.

### 2. Mstari Mkuu: Waebrania 4:16

Basi, na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

### 3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili

Sura ya 3 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Tutatumia Mwongozo wa Somo Zoezi la 8, *"Kukuza Na Kuendeleza Uhusiano Binafsi Na Yesu"* katika darasa la leo.

### 4. Matayarisho Ya Mwalimu

Inaweza kukusaidia kusoma mipango ya kufundishia kwa ajili ya somo la 5 na la 6, unapojiandaa kwa ajili ya kipindi hiki. Sura ya 3 ya somo hili haiwezi kugawika kwa urahisi nusu kwa nusu, ili utumie vipindi viwili. Mkakati tunaoshauri sisi ni kwamba, ushughulikie dhana nzima ya kukuza uhusiano binafsi na Yesu katika somo la 5. Halafu katika kipindi kinachofuata, rudia dhana zile zile kwa kutumia mifano ya Biblia, hasa kutoka kwa maisha ya Kristo. Jihisi huru kupanga upya mipango hiyo miwili ya masomo ikiwa utapata njia bora zaidi ya kufundisha mambo hayo.

Kama wanafunzi wako wanapta shida kushika vizuri baadhi ya mambo haya, pengine fikiri kutumia vipindi vitatu vya darasa kuhusu Sura ya 3 ya somo hili. Unaweza kutumia vipindi viwili kushughulikia mambo ya msingi yanayotajwa katika mpango namba 5 wa kufundishia somo. Katika kipindi cha tatu unaweza kushughulikia mambo yanayotajwa katika mpango wa namba 6 wa kufundishia somo.

### 5. Zoezi la utangulizi wa somo – Sifa Za Urafiki Mzuri (Dakika 5-10)

Waeleze wanafunzi kwamba leo tunaanza mazungumzo yetu kuhusu jinsi ya kuendeleza na kukuza uhusiano binafsi na Yesu. Lakini, kwa ajili ya shughuli zetu za kuanza darasa, hebu tutazame urafiki tulio nao na watu wengine.

Wanafunzi watayarishe orodha ya sifa kumi au mambo kumi wanayotafuta katika rafiki wa karibu. Hebu wachague zile nne muhimu sana, na kuzipa namba kulingana na umuhimu wake. Baada ya kumaliza orodha yao, wasome zile sifa walizoandika. Wewe andika hizo ubaoni, au kwenye karatasi ngumu, au kwenye bango.

Zungumzia kwa kifupi zile sifa zilizochaguliwa nao kuwa muhimu sana. Tengeneza mazingira ili wawe huru kutaja vipaumbele ambavyo ni tofauti na vilivyochaguliwa na wanafunzi wengine.

6. **Fafanua *uhusiano binafsi* (Dakika 3-5)**

Waulize wanafunzi wako wakupe tafsiri zao za uhusiano binafsi, auwaambie wafafanue nini maana ya kuwa na uhusiano binafsi na mtu mwingine.

Kwa ufupi, eleza tunamaanisha nini wakati tunapozungumza juu ya kukuza au kuendeleza uhusiano binafsi na Yesu. Kimsingi ni kwamba tunazungumza juu ya kukuza na kuendeleza urafiki na Yesu. Tunahitaji kumjua kibinafsi. Leo, tunataka kuzungumzia jinsi hilo linavyowezekana.

Tatizo moja linalotukabili ni hili: Unawezaje kukuza au kuendeleza urafiki na mtu asiyeonekana? Ongeza na hili nalo: Yeye hazungumzi na wewe kwa sauti, na huwezi kumgusa. Hakikisha unaweka wazi hoja kwamba Mungu anaweza kujlukana, na anataka kukuza na kuendeleza urafiki na kila mmoja katika wanafunzi wako.



7. **Jadili Hoja A. Kwa nini kujenga uhusiano binafsi na Yesu?**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 27-28**

Tunahitaji kujibu maswali mengine mawili kabla hatujajibu swali hili: **“Kwa nini nijenge uhusiano binafsi na Yesu?”** Hayo maswali mawili ni haya:

**Je, unaamini Mungu yupo?**

**Je, unaamini kwamba Yesu Kristo ni Mungu?**

Kama baadhi ya wanafunzi wako bado wana maswali juu ya mambo hayo mawili, basi hakikisha kwamba unayaweka wazi kabla hujaendelea kwenye hilo jambo lingine. Wanafunzi wasome Waebrania 11:6, andiko linaloendana na swali la kwanza. Pia, zungumzia baadhi ya Maandiko yanayosema kwamba Yesu ni Mungu.

Halafu, shughulikia yale maswali mawili yanayotajwa katika ukurasa wa 27 na 28 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Majibu ya maswali hayo mawili yanaweka wazi ni kwa nini tunapaswa kukuza uhusiano binafsi na Yesu.

1. **Mungu alikuumba kwa nini?**
2. **Ni nini kinacholeta utoshelevu wa kweli maishani?**

Maneno ya J.I. Packer kutoka kitabu chake kiitwacho *Knowing God*, yapatikanayo kwa ukurasa wa 28 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi, husisitiza kipaumbele tunachotakiwa kuweka ili kumjua Mungu kibinafsi. Vile vile unaweza kutaka kutazama yanayosemwa na kitabu cha Mhubiri juu ya kupata maana halisi ya maisha. Mistari michache ya mwisho ya kitabu hicho huonyesha nini cha muhimu zaidi maishani – ambacho ni kumcha Mungu na kuzitii amri Zake. Hebu linganisha kweli hizo za kiBiblia na ujumbe utolewao na dunia kuhusu kitu kinacholeta maana katika maisha ya mtu.

> Katika kitabu chake kiitwacho Knowing God, J.I. Packer anaonyesha hatari za kumpuuza Mungu. Anasema hivi: “Acha kujali kujifunza juu ya Mungu, nawe utakuwa umejihukumu kujikwaa na kutangatanga maishani ukiwa kama mtu aliyefungwa macho kwa kitambaa, bila ya kuwa na mwelekeo na ufahamu wa kinachokuzunguka. Kwa namna hiyo maisha yako yanakuwa kupoteza muda tu, na mwishowe unaweza kupoteza hata nafsi yako.”
>
> *Yametoka kwenye Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 28*

**8. Jadili Hoja B-1. Usitafute tukio la kiajabuajabu**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 29**

Hili ndilo jambo la kwanza linalotajwa katika Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 29 katika kushughulikia mada hii: **"Ni uhusiano wa aina gani unaoweza kukuza pamoja na Yesu?"** Kama baadhi ya wanafunzi wako wanatoka katika mazingira ya uchawi na ushirikina, bila shaka wana uzoefu wa kuona mapepo au maroho. Wavunje moyo ili wasitafute kuona mambo kama hayo wanapokuja kwa Yesu.

Tunaweza kuwa na urafiki halisi kabisa na Yesu. Zungumzia umuhimu wa Yohana 6:44, ambapo Yesu anasema, "Hakuna mtu yeyote awezaye kuja kwangu mimi (Yesu) kama Baba aliyenituma mimi hatamvuta." (TLR)

**9. Jadili Hoja B-2. Je, Inabidi niache kuwa kama nilivyo?**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 29**

5

Wakristo wengine wapya wanajiona kuwa si kitu. Kila unapowauliza kubadilika na kuachana na jambo fulani, ambalo Mungu anasema ni dhambi, wao wanahisi kama unawaambia waachane na jinsi wao walivyo. Wanasema, "Nitaacha kuwa mimi, ikiwa nitaachana na kitu hicho." Huko ni kutokuelewa uhalisia. Hebu fananisha hali hiyo na urafiki wowote wa karibu na mtu mwingine.

Watu wawili wanapokuwa marafiki wa karibu, bado wanabaki na hali zao. Ni kweli kwamba watarekebisha tabia na mwenendo ii wasikwazane. Lakini, wanafanya hivyo kwa sababu wanapendana kama marafiki, si kwa sababu wanalazimishwa.

**10. Jadili Hoja B-3. Mungu anataka urafiki maalum na wewe, lakini si kwamba mnalingana (Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 30-31**

Je, tunaweza kuwa na urafiki na Yesu wa aina gani? Onyesha kwamba Mungu hafyatui kwa wingi urafiki Wake na watu. Yeye humshughulikia kila mtu kimaalum na kipekee, na anampa kila mmoja usikivu binafsi. Lakini, huu urafii na Mungu haunifanyi mimi kuwa sawa na Mungu. Siwezi kumwekea Mungu madai, ila, Yeye anaweza kuweka madai kwangu au kwako.

Hebu tumia jedwali kueleza viwango vitatu vya uhusiano wetu na Yesu.

1. Yesu ni Mwokozi wako – Yeye anakusamehe dhambi zako
2. Yesu ni Kiongozi wako – lazima atawale maisha yako
3. Yesu anataka kuwa Rafiki yako – anataka uhusiano uliojengwa juu ya upendo

## Awamu Tatu Za Uhusiano Binafsi Na Yesu

| **Maandiko** | **Nafasi au sehemu ya Yesu katika uhusiano huu** | **Alichofanya Yesu** | **Pa Kukutania (Kiunganisho)** | **Nafasi au sehemu yangu katika uhusiano huu** | **Cha kufanya mimi** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 Yohana 1:9<br>1 Yohana 2:1-2<br>Matendo 4:12 | Mwokozi | Alilipia gharama ya adhabu kwa dhambi zangu. Anasamehe dhambi yangu | Dhambi yangu | Mwenye dhambi | Kutubu dhambi zangu.<br>Kutoa maisha yangu kumfuata Yesu. |
| 1 Yohana 2:3<br>1 Petro 2:21<br>Yohana 16:13<br>1 Wakor. 6:19-20 | Bwana<br>Kiongozi<br>Mtumishi | Hutoa uongozi<br>Ni Mwalimu<br>Maisha Yake katika Biblia hutoa mfano wa kuigwa ulioko wazi | Sheria za Mungu na mafundisho kuhusu tabia yangu | Mfuasi<br>Mtumishi<br>Mtumwa | Kujua Sheria Zake<br>Kutii sheria Zake<br>Kufanya mapenzi Yake |
| Yohana 15:12-14<br>Yohana 15:15 | Rafiki | Ananipenda<br>Kushirikiana wazi wazi | Kila shughuli katika siku yangu | Rafiki | Kumpenda<br>Kushirikiana wazi wazi |

*Kutoka: Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31*

5

Labda itakuwa vizuri kutengeneza bango la jedwali hili na kulitundika darasani wakati wa kipindi, unapofundisha juu ya kuendeleza na kukuza uhusiano binafsi na Yesu.

Ile safu ya katikati ijulikanayo kama *Pa Kukutania (Kiunganisho),* ndiio jambo muhimu na kuu la kuzungumzia. Mkazo wa huo uhusiano binafsi na Yesu unahusu mambo ya maisha yanayoguswa katika safu hii. Mtu lazima ashughulike na swala la dhambi kabla hajafanikiwa kabisa kuhamia kwenye ngazi ya pili yenye kushughulikia swala la kutii sheria za Mungu na Kristo akiwa Kiongozi wa maisha ya mtu husika.

Hatuwezi kuruka kiwango hicho cha pili cha uhusiano huu. Hatuwezi kuwa rafiki na Yesu na kupuuza sheria Zake na nafasi Yake ya mamlaka katika maisha yetu. Vivyo hivyo, kama wewe ni rafiki ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa, hiyo haikupi wewe uhuru wa kuvunja sheria kila inapo-onekana inafaa kwako.

Urafiki wetu na Yesu unaweza kuwa halisi na wa kina. Yesu hatatumia kamwe nafasi Yake ya mamlaka (kama watu wengine wanavyofanya) na kusema, “Siwezi kumkaribia sana mtu huyo kwa sababu nafasi yangu ni cheo cha juu sana juu yake.”

Hebu zungumzieni juu ya baadhi ya mifano ambayo Yesu aliitumia kuelezea uhusiano huu. Uhusiano wa baba na mtoto ni picha ya kawaida sana inayotumika katika Biblia. Yesu pia alitoa mfano wa hilo kupitia uhusiano wa mchunga mifugo na kondoo wake. Agano Jipya nalo linafananisha uhusiano wetu na Kristo kama ule wa bwana arusi na bibi arusi wake. Pengine utahitaji vielelezo hivyo kwa kifupi tu hapa, na kuvizungumzia kwa kirefu zaidi katika somo linalofuata.

Hiyo jedwali inaweza pia kutumiwa katika somo la 6 ambapo tunajadili kwa upana zaidi swala la kuwasiliana binafsi kama kitu muhimu katika kukuza na kuendeleza uhusiano wa binafsi na Yesu kwa undani zaidi.

**11. Jadili Hoja C-1. Jifunze juu ya Mungu katika Biblia**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31-32**

Kujifunza juu ya Mungu ni moja ya hatua za kwanza ambazo mtu lazima apige katika kukuza na kuendelea mahusiano na Yesu. Wanafunzi warejee swali la 2 kwenye Zoezi la 8 katika Mwongozo Wa Somo, ambalo linawataka wao waonyeshe wanajua kiasi gani juu ya Yesu, kwa kutumia kipimo kinachoanzia namba 1 hadi 10. Kama wanafunzi wako wanahisi huru kufanya, waambie wasome kwa sauti matokeo ya kujipima kwao. La sivyo, wewe zungukia darasa zima na kusoma kimya kimya kila mwanafunzi alichopata. Hiyo itakuwa kuona kwa kiasi fulani jinsi wanavyotazama ufahamu wao wa Mungu kwa jumla.

Kama unao baadhi ya wanafunzi darasani mwako ambao si Wakristo, basi watie moyo wajifunze maisha ya Kristo. Usiwaharakishe kufanya uamuzi wa kujitoa kwa Kristo hadi wajue Yesu ni nani. Kama wanataka Kristo awe Kiongozi wa maeneo yote katika maisha yao kuanzia sasa hadi kufa kwao, usiwasukume wafanye uamuzi wa haraka na usio na kina. Kadiri watakavyojifunza mengi kuhusu Yesu, ndivyo watakavyoweza kuona kwamba Yeye ni chaguo sahihi.

5

Tumia Yohana 14:9-11 kuonyesha kwamba wale Nafsi Tatu katika Uungu, yaani Mungu baba, Mungu Mwana na Mungu Roho Mtakatifu, hawana haiba zinazotofautiana sana. Wote wana sifa zile zile za msingi. Yesu alisema, “Ukitaka kujua zaidi jinsi Baba anavyohisi kuhusu mambo mbalimbali maishani, tazama jinsi Mimi ninavyohisi juu ya hayo. Wote tunafikiri na kujisikia sawasawa.”

**12. Jadili Hoja C-2. Usidhanie Mungu anafikiri kama wewe**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 32**

Tumia maneno ya Isaya 55:8-9 kuonyesha kweli hii muhimu sana juu ya Mungu. Njia Zake na mawazo Yake ni juu sana kuliko sisi, hivyo, hatupaswi kujaribu kufikiria ili kupata mawazo ya Mungu kuhusu jambo wakati Yeye ameamua kunyamaza kimya. Mungu anaweza kujulikana, lakini haitawezekana kwetu kujua kila kitu kinachoweza kujulikana kuhusu Mungu.

**Isaya 55:8-9**

**8 “Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu,” asema BWANA.**
**9 “Kwa maana, kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.”**

Huu unaweza kuwa wakati mzuri wa kuonyesha kwamba maisha yana maswali mengi sana yasiyokuwa na majibu. Huwezi kungoja hadi upate majibu ya hayo maswali yote ndipo ufanye uamuzi wa kumfuata Kristo na kuwa Mkristo. Baadhi ya mambo hayo itabidi “yasubiri” mpaka wakati wa baadaye, ili uweze kufuatilia yale mambo muhimu zaidi maishani – kujifunza kumpenda Mungu na kumtii.

Huu unaweza kuwa wakati mzuri wa kuwaonya wanafunzi juu ya kumtumia Mungu kama chanzo chao cha habari. “Bwana ameniambia.…” Labda kweli Bwana amemwambia mtu huyo kitu, lakini si hivyo wakati wote. Biblia lazima iwe kipimo chetu ili kuona ikiwa hayo “maneno mapya toka kwa Bwana” kweli yanatoka kwa mwanadamu au kwa Mungu.

**13. Jadili Hoja C-3. Kujua kumhusu Mungu au kumjua Mungu kibinafsi**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 32-33**

Ni rahisi sana kutumia muda mwingi sana hapa, ukizungumzia jambo hili. Lakini nadhani itakuwa vizuri ulishughulikie kwa kifupi tu na usonge mbele kufikia sehemu inayofuata, yenye kushughulikia zile hatua za jinsi ya kukuza na kuendeleza uhusiano na Yesu, wa karibu sana na wa kibinafsi.

Wanafunzi wapate nafasi ya kushirikisha majibu yao kwa swali la 3 kutoka Zoezi la 8 katika Mwongozo Wa Somo. Swali lenyewe linawataka wao kufafanua jinsi mtu anavyoweza kumjua Mungu zaidi kwa msingi wa kile kinachosemwa na Wakolosai 1:9-10. Unaweza kutumia hiyo ili kuonyesha tatizo ambalo baadhi ya Mafarisayo walikuwa nalo katika siku za Yesu. Wao walikuwa wanajua mengi sana kuhusu kilichosemwa na Biblia, lakini hawakuwa na uhusiano wa binafsi na Yesu. Pia, yale Maandiko ya Mathayo 7:21-23 yanafaa hapa.

Wanafunzi wako wanaweza kuwa na ufahamu wa kutosha kielimu na kiroho kujua maneno tofauti ya "kujua" yanayotumiwa katika lugha ya Kiyunani. Kwa Kiswahili neno ni moja tu, lakini katika Kiyunani kilichotumika wakati wa Yesu, kulikuwa na maneno mawili. Neno "oida" linahusu kufahamu vitu – yaani, kujua kuhusu kitu fulani. Lile jingine la Kiyunani ni "ginoski" ambalo mara nyingi linabeba dhana ya kujua kutokana na uzoefu binafsi.

Watie moyo wanafunzi wako kujifunza maana ya maneno kutoka kwa hayo Maandiko. Kitabu cha Itifaki cha Young's Analytical kitawapa kwa upesi sana orodha mbili za mistari inayotumia maneno hayo mawili.

**14. Tambulisha Hoja ya D, Ni zipi hatua za msingi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza uhusiano binafsi na Yesu?**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33**

Utakapokuwa umefika hapa katika kipindi, itakubidi upime ni muda gani uliobaki nao wa kufundisha sehemu hii pamoja na ile shughuli ya kufanyia kazi somo kibinafsi. Kama unaona muda unakwisha, basi pitia juu juu kwa haraka mada hizi na kueleza kwamba tutazishughulikia kwa undani zaidi katika kipindi cha darasa kinachofuata.

Utangulizi wa mada ulioko kwa ukurasa wa 33 wa Mwongozo Wa Mwanafunzi hutoa dondoo chache ambazo unaweza kutamani kuzishughulikia japo kwa kifupi. Watie moyo wanafunzi waone hilo kuwa ni lengo halisi – hata watoto wanaweza kukuza na kuendeleza urafiki na Yesu, wa binafsi na wa kina. Tunaweza tusimwone Yesu kamwe, lakini tunaweza kufikia mahali tunapoweza kusema, "Yesu ni rafiki yangu mkubwa".

Unapozungumzia kila moja kati ya hizo hatua nne za kukuza na kuendeleza uhusiano binafsi na Yesu, unaweza kusaidika sana ikiwa utafafanua kila moja kwa kutumia mfano wa urafiki kati ya watu wawili. Nyingi ya hizo kanuni zinaweza kutumika katika urafiki wowote unaotaka kukuza au kuendeleza.

5

**15. Jadili Hoja D-1. Lazima wote wawili watake huo urafiki**
**(Dakika 3-5) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33-34**

Weka wazi hoja kwamba Mungu hana kusitasita katika shauku Yake ya kujenga urafiki na kila mtu wa darasani mwako. Mungu anatamani kuwa na urafiki wa karibu sana na wale wote ambao bado wanaishi dhambini. Mungu tayari amekwisha jitokeza kuonyesha upendo Wake. Swali halisi ni hili:
***Je, mimi ninataka kukuza urafiki na Mungu wa karibu na wa kina, kwa kiasi gani?***

Mathayo 7:7-11 ni mstari mzuri wa kuzungumzia hapa. Onyesha jinsi ambavyo hatua hii inarejea kwa mambo ya kwanza kabisa tuliyozungumzia kuhusu somo hili – kutoa maisha yetu kwa Yesu Kristo.



**16. Jadili Hoja D-2. Jifunze jinsi ya kuwasiliana na Yesu**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 34**

Kujifunza jinsi ya kuwasiliana ndicho kiini cha kukuza uhusiano binafsi na Bwana Yesu. Sisitiza haja ya kukuza na kudumisha muda wenye maana wa maombi kwa kila siku. Kama wanafunzi wako ni Wakristo wapya sana, ni vizuri utumie muda wa kutosha kuzungumza juu ya mambo ya msingi kuhusu maombi. Jambo hilo linashughulikiwa kwa upana zaidi katika somo katika *Mafunzo ya Vikundi kwa Maisha Mapya,* linaloitwa *Matendo Ya Kikristo.*

Wanafunzi washirikishe darasa majibu yao kwa swali la 4 na la 5 katika Zoezi la 8 ndani ya Mwongozo Wa Somo. Swali la 4 linawataka wao kutathmini nyakati zozote ambazo wamehisi kuwa karibu na Mungu. Swali la 5 linawataka wao wapime jinsi wanavyohisi kuhusu nyakati zao za kuomba. Kama muda unakuishia, labda itafaa uzungumzie Swali la 5 wakati huu na kuacha mazungumzo juu ya swali la 4 hadi wakati wa kipindi kijacho cha darasa.

Sisitiza haja ya kuwasiliana na Mungu kwa njia iliyo wazi na ya ukweli. Watie moyo kuzungumza na Mungu juu ya matukio yote tofauti yanayoendelea katika siku yao. Hawana haja ya kusikia "sauti kutoka mbinguni" kabla ya kufanya chochote leo. Lakini wanahitaji kujifunza tabia ya kumwingiza Mungu kwa mawazo yao mara kwa mara mchana kutwa. Mfano wa Mfarisayo na yule Mtoza ushuru wakiomba huonyesha tofauti kati ya kuomba sala za kibianfsi na kuwasiliana na Mungu kwa uwazi kabisa. Tazama Luka 18:9-14.

**17. Jadili Hoja D-3. Jifunze kukuza imani na kusema kweli kwa uwazi**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 34-35**

Mambo haya mawili yanahusiana kwa karibu, lakini pia kila moja liko peke yake. Onyesha haja ya kuchagua kwa udhati jinsi utakavyoitikia katika maeneo hayo mawili. Unachagua kumwamini mtu. Unachagua kuwa mkweli na wazi kwake.

Mungu ni mkamilifu katika hayo maeneo mawili. Yeye ni mkweli kabisa wakati wote anaposema nasi, wala hatupi sisi sababu yoyote ya kutomwamini. Sisi (si Mungu) tunahitaji kukua katika maeneo hayo mawili. Onyesha nafasi ya utii wetu katika kumwonyesha Mungu kwamba anaweza kutuamini.

**18. Jadili Hoja D-4. Jifunze kumheshimu na kumpenda (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 35**

Biblia inatamka wazi kabisa kwamba Mungu anampenda mwanadamu na kumheshimu sana. Hebu darasa litazame sifa za upendo zitolewazo katika 1 Wakorintho 13:4-8, na kuona ni ngapi zinazoeleza jinsi Mungu anavyotuitikia sisi. Ukiishiwa na muda leo, subiri hadi kipindi kijacho cha darasa ili kutazama 1 Wakorintho sur aya 13.

Onyesha haja yetu sisi kuitikia kwa upendo na heshima. Kiwango tutakachoitikia upendo wa Mungu, ndicho kitakachoamua kina cha uhusiano wetu Naye. Zungumzia juu ya umuhimu wa amri kuu ya Mungu kwetu – kwamba tumpende. Unaweza kutaka kuzungumzia ni kwa nini tunaagizwa kumpenda Yeye. Pia, zungumzia ile mistari inayosema kwamba tukimpenda Mungu, tutamtii. Rejelea tena lile jedwali kwenye ukurasa wa 31 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inayoonyesha vile viwango vitatu vya uhusiano wetu na Yesu. Onyesha jinsi upendo na heshima unavyohusiana na Yesu kuwa Kiongozi wetu.



**19. Kufanyia Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)**

Toa changamoto ya moja kwa moja kwamba wawe wakweli wanapomwambia Mungu ni nini wanataka kufanya juu ya uhusiano wao binafsi na Kristo. Waambie wachukue hatua za vitendo kila siku za kumkaribia Yesu.

**A. Pima uhusiano wako binafsi na Yesu**

Watie moyo wanafunzi kujipima wenyewe kwenye kipimo kinachoanzia 1 hadi 10 kuhusu sifa ya uhusiano wao binafsi na Yesu. (Namba 1 inamaanisha Simjui Yesu kabisa, na namba 10 inamaanisha nina uhusiano wa kina na Yesu wa kina, wa kipekee, na wa binafsi.)

Wanafunzi wakae wawili wawili na kushirikishana majibu yao. Halafu waambie waombeane, ili waweze kukuza na kuendeleza uhusiano na Yesu, ulio wa karibu, wa kina na wa binafsi. Kama huhisi vizuri kwa wanafunzi kukaa wawili wawili na kuombeana, basi waambie waandike sala kwa Mungu baada ya kumaliza kujipima. Waambie wamwambie Mungu kile ambacho wangetaka kuona kinatokea katika uhusiano wao wa binafsi na Yesu katika siku na majuma ya baadaye.

**B. Mahali pa kuanzia ili kufikia uhusiano na Yesu wenye kina na wa binafsi – Zoezi la 10 katika Mwongozo Wa Somo**

Je, mtu anaanzia wapi kukuza na kuendeleza uhusiano na Yesu, ulio karibu na wa binafsi sana? Zoezi la 10 katika Mwongozo Wa Somo linatoa kanuni kadhaa zinazoweza kuwapa wanafunzi wako mawazo fulani ya kufikisha jambo hilo kwenye ngazi ya binafsi.

Waambie wanafunzi watazame Kazi-Mradi hii na kwa kifupi upitie yale maelekezo pamoja nao. Kama una zaidi ya siku moja kabla ya kipindi chako kinachofuata, basi uwatake wakamilishe tathmini angaa ya siku moja tu kwa ajili ya kipindi kinachofuata. Mambo watakayogundua yanaweza kutumika katika mazungumzo jinsi mtu anavyoweza kuimarisha uhusiano wake na Yesu.

5

**20. Kazi za kufanya**

A. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 8, *“Kukuza Na Kuendeleza Uhusiano Binafsi Na Yesu”*.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 7, *“Waulize Wakristo Wengine Ushahidi”,* kama hukuisahihisha baada ya kipindi cha darasa kilichopita.

C. Kagua ili uhakikshe kwamba wanafunzi wako wanaelewa jinsi ya kukamilisha Zoezi la 9 katika Mwongozo Wa Somo, inayoitwa *“Kutia Nguvu Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu”*. Kazi angaa ya siku moja ya shughuli hii inatakiwa kuwa imekamilishwa na kuwa tayari kwa ajili ya kipindi kifuatacho cha darasa.

D. Wanafunzi wasome Sura ya 3 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kufanya marudio ya mazungumzo ya darasani leo, na kujiandaa kwa ajili ya kipindi kifuatacho cha darasa.

**21. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa**

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 6
## Kujenga Urafiki Na Yesu

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Nahitaji kushirikiana na Mungu kufanya mabadiliko katika maisha yangu ya kila siku, yatakayonisaidia kumkaribia Mungu zaidi.

**2. Mstari Mkuu: Wafilipi 1:6 TLR**

Nina hakika kwamba Mungu aliyeanzisha kazi njema ndani yenu ataendelea kufanya kazi ndani yenu mpaka siku Yesu Kristo atakapokuja tena.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 3 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la zifuatazo, kutoka katika Mwongozo Wa Somo, zinaweza kutumiwa na somo hili pia.
Zoezi la 8, *Kukuza Na Kuendeleza Uhusiano Binafsi Na Yesu*
Zoezi la 9, *Kutia Nguvu Uhusiano Wangu Binafsi Na Yesu*
Zoezi la 10, *Kumjua Yesu – Ilivyotokea kwangu binafsi*



**4. Zoezi la utangulizi wa somo – Unakuzaje na kuendeleza urafiki na mtu aliye mbali nawe? (Dakika 5-10)**

**A. Tatizo (wasomee wanafunzi wako)**

Unataka uwe na urafiki na mtu aliye katika nchi nyingine.
Unajua hamtaweza kuonana na mtu huyo, kwa sababu huwezi kusafiri kwenda huko. Utafanyaje ili kukuza na kuendeleza urafiki na mtu huyo?

**B. Shughuli Ya Vikundi Vidogo**

Darasa ligawanyike katika vikundi vidogo vya watu watatu hadi watano.
Wape Dakika nne kutayarisha orodha iliyo na mapendekezo yao. Watoe mpango kazi unaoeleweka. Unaweza pia kuwataka waorodheshe baadhi ya matatizo wanayoweza kukabiliana nayo katika kujaribu kumjua mtu huyu. Waandike mawazo yao.

**C. Wakati wa kutoa taarifa**

Kila kikundi kitoe taarifa kwa darasa kuhusu mawazo yao. Kwa kifupi, zungumzia matatizo ambayo wangekutana nayo kwa kujaribu kuendeleza urafiki kama huo.

Unaweza kulinganisha matatizo hayo na yale tunayokabiliana nayo tunapojaribu kuendeleza urafiki na Yesu. Wengi wetu hatutamwona Yesu mpaka tutakapofika mbinguni, lakini tunaweza kujifunza kuwasiliana Naye sasa. Yafuatayo ni maswali machache tunayotaka kujibu katika kipindi hiki cha darasa:

1. Je, unataka kuwa na uhusiano wa aina gani na Yesu?
2. Unawezaje kumjua Yesu kweli kibinafsi?
3. Je, inachukua muda gani kukuza uhusiano na Yesu, wa karibu na wa binafsi?
4. Naweza kufanya nini juma hili ili kuwa na kina cha uhusiano wangu binafsi na Yesu?

6

**5. Rudia dondoo muhimu kutoka Somo la 5 (Dakika 5-10)**

Rudia ile dondoo inayotajwa kwa ukurasa wa 28 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inayosema (Hoja A-2), **"Ni nini kinacholeta utoshelevu wa kweli maishani?"** Hebu waulize kama wana maswali yoyote juu ya mada mlizoshughulikia katika kipindi cha mwisho darasani. Sisitiza haja ya kujitoa kabisa kwa akili, nia na hisia, wakati unapotafuta kukuza uhusiano binafsi na Yesu.

**6. "Kuwa wamoja" na Yesu (Dakika 5-15)**

Rejelea lile jedwali linaloshughulikia awamu tatu za uhusiano wetu na Yesu. Linapatikana ukurasa wa 31 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

## Awamu Tatu Za Uhusiano Binafsi Na Yesu

| **Maandiko** | **Nafasi au sehemu ya Yesu katika uhusiano huu** | **Alichofanya Yesu** | **Pa Kukutania (Kiunganisho)** | **Nafasi au sehemu yangu katika uhusiano huu** | **Cha kufanya mimi** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 Yohana 1:9<br>1 Yohana 2:1-2<br>Matendo 4:12 | Mwokozi | Alilipia gharama ya adhabu kwa dhambi zangu. Anasamehe dhambi yangu | Dhambi yangu | Mwenye dhambi | Kutubu dhambi zangu.<br>Kutoa maisha yangu kumfuata Yesu. |
| 1 Yohana 2:3<br>1 Petro 2:21<br>Yohana 16:13<br>1 Wakor. 6:19-20 | Bwana<br>Kiongozi<br>Mtumishi | Hutoa uongozi<br>Ni Mwalimu<br>Maisha Yake katika Biblia hutoa mfano wa kuigwa ulioko wazi | Sheria za Mungu na mafundisho kuhusu tabia yangu | Mfuasi<br>Mtumishi<br>Mtumwa | Kujua Sheria Zake<br>Kutii sheria Zake<br>Kufanya mapenzi Yake |
| Yohana 15:12-14<br>Yohana 15:15 | Rafiki | Ananipenda<br>Kushirikiana wazi wazi | Kila shughuli katika siku yangu | Rafiki | Kumpenda<br>Kushirikiana wazi wazi |

*Kutoka: Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31*

Safu ya katikati ya jedwali hilo inaeleza mahali tunapokutania na Yesu katika kila awamu. Unaweza kupanua dhana hiyo zaidi kwa kutoa maelezo yafuatayo:

Yesu aliomba katika Yohana 17:20-21, "Wala si hao tu ninaowaombea, lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. [21] Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma." Sehemu inayobaki ya sala hiyo katika Yohana sura ya 17 inafafanua zaidi dhana hiyo. Yesu anataka sisi tupate aina ile ile ya umoja ambayo Yeye na Baba wanayo katika uhusiano wao. Hilo ndilo lengo letu tunalotaka kulifikia hatimaye.

Cha msingi na cha kwanza kabisa ili uhusiano ukue kati ya watu wawili, ni *kukutana.* (Chora duara mbili zinazogusana kidogo kwa mbali.)

Kadiri hao wawili wanavyokutana zaidi, ndivyo uwezekano unavyozidi kuwa mkubwa wa uhusiano wa karibu. (Chora duara mbili zikiwa zimepishana kidogo kwa mbali.) Kadiri hao wawili wanavyokutana ndivyo wanavyozidi kujuana.

Kadiri mwingiliano kati yao unavyofanyika, ndivyo wanavyokuwa karibu ya kuwa wamoja. (Onyesha mfano wa hilo kwa kuchora miviringo kadhaa, kila wakati ikiingiliana zaidi na zaidi kuliko mara ya kwanza. Ile ya mwisho iwe imeingiliana kabisa, kiasi cha kuwa mmoja uko juu ya mwingine.)

Kadiri unavyokaribia "kuwa wamoja" na mtu mwingine, ndivyo uhusiano wenu wa binafsi unavyozidi kupata kina. Utaratibu wa kuwa wamoja haumaanishi kwamba mmoja katika hao wawili anapoteza utambulisho na ubinafsi wake. Wote wawili wanabaki pekee na wana haiba zao binafsi. Lakini, wanasafiri pamoja maishani, wakiwa na malengo yanayofanana, mambo ya kuthamini yanayofanana, na mambo wanayopenda yanayofanana.Wanapata kujuana kweli kweli – wako wazi katika mawasiliano yao. Hapa, ingiza mstari wa Wakolosai 3:14 na kuonyesha jinsi upendo unavyoleta huo msaada unaohitajika ili kutufanya wamoja na Yesu.

Rudi kwenye lile jedwali (Mwongozo Wa Mwanafunzi, ukurasa wa 31) na kueleza zile ngazi tatu za uhusiano wetu na Yesu. Chora kitu kama pembetatu (piramidi) kwenye lile jedwali, kuanzia juu hadi chini. Tunapomjua Yesu mara ya kwanza, ni kama kuwa juu kileleni pa lile piramidi. Kadiri upendo wetu unavyokua na kupata kina, uhusiano wetu unapata nafasi kubwa zaidi maishani mwetu. Upendo wetu unaoendelea kupanuka wakati wote unatuwezesha kuwa na uhusiano wenye kina na wa binafsi sana na Yesu Kristo.



**7. Jadili Hoja D. Ni zipi hatua za msingi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza uhusiano binafsi na Yesu? (Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33-35**

Kama ulishughulikia jambo hili kwa kina katika kipindi cha mwisho darasani, basi rudia kwa kifupi hizo dondoo nne kutoka ukurasa wa 33-35 ya Mwongozo Wa Mwanafunzi. Ikiwa ulitaja tu kwa kifupi sehemu hii ya somo kabla ya hapo, basi ingia kwa undani na utoe maelezo mengi juu ya jambo hilo wakati huu.
Tazama shughuli #14 hadi 18 katika mpango wa mwalimu wa kufundishia somo la 5, ukurasa wa 57 na 59.

**8. Mifano kutoka maisha ya Kristo**
**(Dakika 10-20) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 33-35**

Ili hoja zote zifikie mahali pa kuweza kutumiwa, itakubidi utazame mahusiano ambayo Yesu alikuwa nayo na watu mbalimbali katika Agano Jipya. Tazama hasa zile hatua nne za msingi zinazohitajika ili kuendeleza na kukuza uhusiano binafsi na Yesu zilizotajwa katika ukurasa wa 33-35 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

**9. Jinsi Biblia inavyoonyesha picha za uhusiano wetu na Mungu (Dakika 5-15)**

Zungumzieni picha mbalimbali zinazotumiwa katika Biblia kueleza uhusiano wetu na Mungu. Uwe huru kuongezea Maandiko mengine au picha zingine zinazotumika katika Biblia.

1. Baba na mtoto; Yohana 1:12, Waebrania 12
2. Mchungaji na kondoo; Yohana 10
3. Bibi arusi na bwana arusi; Mathayo 25
4. Kuku na vifaranga vyake; Mathayo 23:37-39

Tazama ukurasa wa 30 na 31 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi kwa ajili ya habari zaidi juu ya jambo hilo —Hoja B-3: **"Mungu anataka urafiki maalum na wewe, lakini si kwamba mnalingana."** Ikiwa ulishughulikia mada hiyo kwa undani na kwa kina katika somo la 5 (tazama shughuli #10 ukurasa wa 54-55), basi ruka shughuli hiyo, au uitaje tu kwa kifupi kama mtu anayefanya marudio.



**10. Zungumzia Waefeso 3:14-21 (Dakika 5-10)**

Waefeso 3:14-21 ina kweli za kushangaza sana juu ya uhusiano wetu na Mungu. Swali la 6 katika Zoezi la 8 iitwayo *Kukuza Na Kuendeleza Uhusiano Binafsi Na Yesu,* katika Mwongozo Wa Somo, linawataka wanafunzi kuorodhesha mawazo jinsi wanavyoweza kukuza urafiki na Yesu, wenye kina. Waambie washirikishe darasa majibu yao. Unaweza pia kuorodhesha waliyogundua kwenye ubao au utayarishe bango.

**11. Mifano ya kisasa na ya kihistoria ya watu waliotengeneza mahusiano na Yesu ya karibu sana (Dakika 5-15)**

Kama una muda, ni vizuri kuzungumzia watu wachache mbalimbali wa kihistoria darasani, na wa kisasa, ambao walitengeneza uhusiano wa karibu sana na Bwana Yesu. Pengine unaweza kuwahoji Wakristo kadhaa wa zamani katika eneo lako na kuwauliza jinsi ambavyo wamekuza urafiki wa karibu sana na Yesu. Shirikisha mifano hiyo darasani. Pia, unaweza ukarekodi mahojiano hayo ili uweze kufanya darasa lisikilize vipengele ulivyochagua na unavyotaka visikilizwe na darasa.

**12. Taarifa za Zoezi la 9 na Zpozi la 10 (Dakika 5-15)**

Ikiwa wanafunzi wako wamepata muda wa kutosha kuanza kufanya Zoezi la 9 na Zoezi la 10, toa nafasi kwa wachache kushirikisha mifano itokanayo na utafiti wao. Ikiwa wanafunzi wako hawajapata nafasi ya kufanya hivyo, basi unaweza kushirikisha mifano kadhaa kutoka kazi ya wanafunzi kwenye Kazi-Miradi hiyo kutoka kwa vipindi au nyakati zilizopita ulizowahi kufundisha somo hili. \

Kama hii ni mara yako ya kwanza kufundisha somo hili, basi tunza nakala ya kazi zao ili uweze kutumia mifano yao wakati mwingine utakapofundisha somo hili. Hakikisha kwamba wanafunzi wenyewe wanakupa kibali cha kufanya hivyo.

**13. Maonyesho ya vitendo kuhusu upendo kutoka 1 Wakorintho 13:1-8 (Dakika 5-15)**

Kupata njia za vitendo za kuonyesha upendo wetu kwa Mungu ni changamoto mara nyingi. Sifa za upendo zitolewazo katika 1 Wakorintho 13:1-8 ni mahali pazuri pa kuanzia, kwa ajili ya wale wanaotafuta njia za kivitendo za kuonyesha upendo wao kwa Mungu. Kadiri muda unavyoruhusu, pitia kila sifa ya upendo na kuzungumza jinsi tunavyoweza kuionyesha hiyo kwa Mungu.

Mstari wa nne unasema, "Upendo huvumilia." Ni njia zipi tunazoweza kutumia kuonyesha upendo katika uhusiano wetu na Mungu? Labda kuna wengine wanaomba muujiza kutoka kwa Mungu katika maisha yao. Kuonyesha uvumilivu kwa Mungu ni onyesho la upendo. Wakati wowote unapoonyesha uvumilivu katika shughuli zako za kila siku, hilo pia linaweza kuwa onyesho la upendo kwa Mungu.

Ikiwa tutakuwa wavumilivu, na kusudio letu iwe ni kumwonyesha Mungu jinsi tunavyompenda, ataona matendo yetu ya upendo. Yesu alisema katika Mathayo 10:40-42 kwamba, hata kama tutatoa kikombe cha maji baridi kwa mtu kwa jina Lake, Yeye Mwenyewe ataona hilo.

Kuna mambo mawili yanayotajwa hapa katika kitabu cha 1 Yohana, yanayofaa kuingia hapa. Katika 1 Yohana 2:3-11 tunaambiwa juu ya uhusiano ulioko kati ya kumpenda Mungu na kumchukia ndugu yako. 1 Yohana 2:15 huzungumza juu ya kumpenda Mungu au kuipenda dunia – si wote kwa pamoja. Pia unaweza kuzungumzia kuhusu jinsi ambavyo kutii sheria za Mungu ni onyesho la upendo wetu Kwake.

6

**14. Jadili Hoja E. Ni nini matokeo ya kumjua Mungu kibinafsi? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 36-37**

Zungumzia matokeo ya kumjua Mungu kibinafsi. Je, huu urafiki utakuwa na mguso gani katika maisha yako ya kila siku?

**15. Kufanyia Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)**

Mahusiano yote yanaweza kufaidika kwa nafasi kutafutwa ya watu kupumzika kidogo na kufikiri na kufanya tathmini. Mume hutulia na kujiuliza ikiwa uhusiano wake na mke wake ndivyo unavyopaswa kuwa. Mke naye anafanya vivyo hivyo. Sisi pia tunahitaji kufanya hivyo kuhusu uhusiano wetu na Yesu. Mara moja moja tunahitaji kutulia kidogo na kujiuliza ikiwa mambo yako vile yanavyotakiwa kuwa.

Wanafunzi watumie muda sasa kufikiri juu ya uhusiano wao na Yesu. Chagua shughuli moja kati ya hizi zifuatazo, ili kumalizia somo hili.

**A. Tathmini binafsi kwa kutumia picha za kuunganishwa au shairi**

Tumia maswali haya yafuatayo kukusaidia kutathmini uhusiano wako binafsi na Yesu. (Orodhesha maswali hayo kwa ubao, au uyatayarishe mapema kabla ya darasa ili kumgawia kila mwanafunzi.)

1. Je, uhusiano wangu na Yesu unakua na kuongezeka?
2. Je, Yesu anaonekana kuwa mbali sana na asiyekuwa sehemu ya maisha yangu?

3. Je, kweli ninampenda Yesu? Nampenda kiasi gani?
4. Je, ninajaribu kumpenda zaidi?
5. Ninaaweza kufanya nini ili kuboresha uhusiano wangu na Yesu?

Baada ya Dakika chache kupita (ambazo wewe unaona ni muda wa kutosha kufikiri), waambie wanafunzi wachague shughuli moja kati ya hizi zifuatazo:

1. Tengeneza mkusanyiko wa picha, wa michoro, au wa maneno - unaoonyesha jinsi unavyohisi juu ya uhusiano wako na Yesu.
2. Andika shairi linaloeleza jinsi unavyohisi kuhusu uhusiano wako na Yesu.

**B. Tathmini ya mazingira yangu yanayonipa msongo au yanayonifanya nichukie**

Wanafunzi wako watambulishe eneo moja ambapo wamekuwa wakipata msongo, au kukasirika, au kuvurugikiwa. Hawana haja ya kuliambia darasa mambo hayo. Wafikiri tu jinsi mazingira hayo au hali hiyo inavyoweza kuwa nafasi kwao kumkaribia Mungu.

6

Waandike njia moja wanayoweza kutumia kuonyesha upendo wao kwa Mungu kupitia hali hiyo ngumu. Pengine utapenda kutoa mfano kutoka kwa maisha yako mwenyewe kwanza.

Funga darasa kwa maombi ya kujiweka wakfu na kujitoa, kukuza uhusiano na Yesu wa karibu na binafsi.

## 16. Kazi za kufanya

A. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 8, *"Kukuza Na Kuendeleza Uhusiano Binafsi Na Yesu"*, kama hukuwa umeisahihisha baada ya kipindi cha darasa la mwisho.

B. Kagua wanavyoendelea katika kutimiza Zoezi la 5 ya kwenye Mwongozo Wa Somo inayoitwa *"Andika hadithi yako"*. Hakikisha kwamba hawaiweki kando na kusubiri hadi siku moja kabla ya tarehe iliyopangwa kukabidhiwa.

C. Waelekeze wanafunzi kusoma sura ya 4 katika Mwongozo wa Wanafunzi wakijitayarisha kwa kipindi kifuatacho.

## 17. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 7
## Sababu Za Mashaka

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Ninaahitaji kugundua kinachotokea katika maisha yangu ya kila siku, kinachonifanya kuwa na mashaka juu ya mimi kuwa Mkristo.

**2. Mstari Mkuu: Yakobo 1:5-6 TLR**

Ikiwa huna hekima, mwombe Mungu akupe. Wakati wote Yeye yuko tayari kukupa, na hatakwambia umekosea kwa kumwomba. (6) Unapomwomba, ni lazima uwe na imani. Usiwe na mashaka. Yeyote mwenye mashaka ni kama wimbi ambalo linasukumwa na bahari huko na huko.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 4 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Tutatumia Mwongozo wa Somo Zoezi la 11, *"Ni Vipi Kuhusu Mashaka?"* katika darasa la leo.

7

**4. Mwalimu Kupanga Mambo Mapema**

Sura ya nne ya funzo hili inashughulika na mashaka. Kulinganana muda ulio nao, na shauku ya wanafunzi, utahitaji kuamua ikiwa utatumia vipindi viwili vya darasa au vitatu kuhusu mada hiyo. Mipango mitatu ya kufundisha inatolewa hapa chini.

Somo la 7 linashughulikia sababu za mashaka.

Somo la 8 linatoa mfumo kwa ajili ya kutatua matatizo yanayoleta mashaka. Ujuzi wa Tomaso aliyekuwa mwanafunzi wa Yesu, ndicho kiini cha somo hili.

Somo la 9 linatoa mafunzo ya ziada kuhusu jinsi ya kuondoa mashaka na nguvu ya mashaka juu ya maisha ya Mkristo.

**5. Zoezi la utangulizi wa somo: *Kupima Mashaka Yangu, Na Maswali* (Dakika 5-10)**

Tumia ile chemsha bongo inayoitwa ***Kupima Mashaka Yangu, Na Maswali*** ili kuanzisha kipindi cha leo. Utapata nakala ya chemsha bongo hiyo hapo chini. Tengeneza nakala za shughuli hiyo ya tathmini na umpe kila mwanafunzi. Wape Dakika kati ya 3 hadi 5 kujipima wenyewe hapo. Onyesha kwamba maelekezo hayawataki wajipime jinsi wanavyohisi leo juu ya maeneo husika. Wanachotakiwa ni kupima ikiwa wamewahi kupata mashaka au maswali katika maeneo hayo (huko nyuma, au hata wakati huu).

Wakimaliza, pata mrejesho kwa njia kadhaa mbalimbali. Njia moja ni wewe kusoma orodha hatua kwa hatua na kutaka watu wainue mikono kuhusu kila jibu linalowezekana. Njia nyingine ni kumwuliza kila mwanafunzi kushirikisha maeneo kadhaa ambayo yeye amepata mashaka au maswali "mengi". Baada ya wanafunzi wote kufanya hivyo, unaaweza kutoa nafasi kwa kila mmoja kushirikisha eneo moja au mawili (kama yapo) ambayo hawakuwa na mashaka wala maswali "kamwe".

Hapo, tambulisha sura ya 4 ya somo. Eleza mambo mtakayoshughulikia katika somo hili na kile mtakachoshughulikia katika darasa moja au mawili yajayo. Hiyo itawasaidia kuwapa mwelekeo jinsi utakavyoshughulikia mambo hayo.

## Kupima Mashaka Yangu, Na Maswali

Hii ni karatasi ya kujitathmini na kujipima mwenyewe. Kila swali linadai jibu binafsi. Hayatafutwi majibu kwamba “Sawa” au “Si Sawa”. Hutatakiwa kumpa mwalimu karatasi yako.

Soma kila sentensi, kisha ujipime kwa kutumia sentensi hii:
**Katika maisha yangu nimekuwa na mashaka, maswali, au hali ya kutokuwa na uhakika katika maeneo haya.**

Weka alama ya kukubali kwenye kisanduku kinachoeleza vizuri zaidi mambo yalivyokuwa.

| | **Sana** | **Kiasi** | **Sijawahi** |
|---|---|---|---|
| 1. Kwamba Mungu yupo | | | |
| 2. Kwamba Yesu ni Mungu | | | |
| 3. Kwamba kweli kuna Jehanamu | | | |
| 4. Kwamba nikifa nitakwenda Mbinguni | | | |
| 5. Kwamba kanisa letu lina majibu kwa maswali yangu yote ya kiroho na matatizo yangu | | | |
| 6. Kwamba kweli Ukristo unatosheleza leo mahitaji ya vijana na watu wazima | | | |
| 7. Kwamba kweli Mungu anajua ni nani anayenifaa kuoana naye, na kwamba atanionyesha huyo mtu | | | |
| 8. Kwamba mimi ni Mkristo wa kweli | | | |
| 9. Kwamba ninaweza kutii sheria za Mungu na bado nifanikiwe maishani | | | |
| 10. Kwamba kweli Mungu ananijali mimi na mahitaji yangu | | | |
| 11. Kwamba Mungu atajibu maombi yangu | | | |
| 12. Kwamba wengine kanisani kwetu ni Wakristo wa kweli | | | |
| 13. Kwamba Mungu anaridhika na jinsi ninavyoishi kwa sasa | | | |
| 14. Mambo mengine yanayoweza kunisababisha kuwa na mashaka | | | |
| A. | | | |
| B. | | | |
| C. | | | |

**6. Tafsiri ya "Mashaka" (Dakika 3-5)**

Mwanzoni mwa kipindi, chukua muda kuzungumza maana ya neno "mashaka". Waruhusu wanafunzi kujibu maswali yao kwa swali la 2 katika Zoezi la 11 katika Mwongozo Wa Somo, kinachowauliza kuandika maana ya neno "mashaka".

Baadhi ya wanafunzi wanaweza kuhitaji mifano kadhaa ili wapate kuelewa vizuri kile tunachozungumzia. Hapa, tunatumia neno "mashaka" kwa ujumla sana. Kimsingi, tunasema kuhusu maswali yoyote au hali ya kutokuwa na uhakika ambayo mtu anaweza kuwa nayo.

**7. Orodhesha baadhi ya mashaka ambayo Wakristo wapya wanayo (Dakika 5)**

Toa nafasi kwa wanafunzi kushirikisha baadhi ya mashaka ambayo wamekuwa nayo juu ya Mungu na kuhusu kuwa Mkristo. Pengine itasaidia kurejea mambo yaliyoibuka katika shughuli ile ya Kuchangamkia Somo. Unanaweza pia kushirikishana majibu waliyoandika kwenye Zoezi la 11, swali la 5 katika Mwongozo Wa Somo, ambalo liliwauliza nini baadhi ya mashaka na maswali waliyo nayo juu ya Mungu, Biblia, au kuwa Mkristo.

Tunataka kujaribu na kuelekeza mawazo yetu kwa mashaka juu ya Mungu na uhusiano wetu Naye. Lakini, matatizo mengine ambayo kwa kutazama haraka haraka yanaweza kuonekana kama hayahusiki na uhusiano wa mtu na Mungu yanaweza kuwa ndiyo sababu ya moja kwa moja ya kuwa na mashaka kuhusu Mungu na kuhusu uhakika wa wokovu wa mtu.

Kuwa makini usipuuze maswali ambayo wanafunzi watayaibua. Lakini pia uwe tayari kuyaweka mazungumzo kwenye mambo unayotaka kuyashughulikia. Watie moyo hao wanafunzi wenye maswali mengine kukuona baada ya darasa.

Pia, tungetaka kuzuia muda huu usiwe nafasi ya mjadala mkubwa sana kitheolojia kuhusu maswali magumu yenye kutenga madhehebu. Shughulikia hayo kwenye kiwango cha kutendea kazi, na itawasaidia sana watu wote.

Kuna uwezekano wa unafiki kiroho kuingia hapa tunaposhughulikia sura ya 4. Kama ifuatavyo: "Mashaka? Mimi sina mashaka! Hayo ni mambo ya Wakristo dhaifu. Mimi niko kiroho; sipati mashaka kamwe!" Usijiruhusu wewe au Kurusu waafunzi wowote kuondoka wakiwa na hali hiyo. Si wote wanaopambana na mashaka. Lakini wengi wanakabiliana nayo, na inabidi tuchukulie kwa uzito sana amri itolewayo katika Yuda mstari wa 22 (TLR), kwamba, "Wahurumieni wale wanaokuwa na mashaka."

**8. Nini kilichosababisha mashaka kwa yule Kijana Tajiri? (Dakika 10-15)**

Wanafunzi wasome Marko 10:17-22, ambapo kuna habari juu ya kijana tajiri mmoja aliyemwendea Yesu. Yafuatayo ni maswali machache unayoweza kutumia kujadili huu mfano wa kiBiblia:

1. **Je, huyo mtu alitaka Yesu ajibu swali gani?**
{"Mwalimu mwema, nifanye nini nipate uzima wa milele?"}

2. **Yesu alijibuje swali la huyo kijana tajiri?**
{Alimtajia baadhi ya zile Amri Kumi}.

3. **Yule kijana alijibuje habari ya Amri Kumi?**
{"Nimezitii amri hizo zote tangu nikiwa mdogo."}
Nyongeza: Lakini bado anaonekana kuwa na mashaka juu ya kufika mbinguni. Onyesha kwamba Wakristo wengi – na sio wapya tu – hupitia kipindi cha mashaka.

4. **Yesu alionyesha kwamba ni tatizo gani lililokuwa linamfanya mtu huyo kuwa na mashaka bado? Je, Yesu alimpa mtu huyo suluhisho gani?**
{Tatizo lake - fedha}

[Suluhisho la Yesu – "Nenda ukauze vyote ulvyio navyo, uwape maskini hiyo fedha, nawe utakuwa na utajiri mbinguni. Halafu, njoo unifuate."]

5. **Huyo kijana tajiri aliitikiaje ushauri wa Yesu?**
{"Uso wake ulikunjamana, naye akaondoka akiwa na huzuni."}

Onyesha kwamba mtu huyo alikuwa anamwamini Mungu kwa dhati. Alikuwa na hekima alipomwendea Yesu – Mungu Mwenyewe – ili kupata jibu la swali lake. Lakini sehemu ya kusikitisha ya kisa hiki ni kwamba alikataa suluhisho la Yesu. Hapa tunaweza kulenga mazungumzo kwenye sababu ya mashaka yake – tatizo lake lilikuwa fedha. Yawezekana pia alikataa suluhisho la Kristo lililohusu wito kuishi maisha mapya ya umaskini.

Jambo tunalotaka kuweka wazi hapa ni kwamba mashaka si tatizo – bali ni matokeo au dalili za tatizo. Mtu anapokuwa na mashaka, kuna kinachosababisha. Matatizo ya aina mbalimbali yanaweza kusababisha mashaka katika maisha ya Mkristo. Mashaka ya huyo kijana tajiri hayakusababishwa na fedha tu, bali hali ya moyo wake kuhusu fedha zake.

7

**9. Jadili Hoja A. Anayeleta mashaka hayo akilini mwako ni nani?**
**(Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 39-41**

Jambo hili linaweza kuleta kuchanganyikiwa kwa urahisi sana, hivyo, uwe makini kufafanua na kueleza vizuri kila jambo, na kulitolea mifano. Utapata kianzio kizuri cha kuzungumzia juu ya vyanzo mbalimbali vinne vya mashaka katika ukurasa wa 39-41 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

**Shetani:** chanzo rahisi cha mashaka kukitambua, ni Shetani. Onyesha baadhi ya mistari inayomtaja Shetani kuwa ni mwongo na mdanganyifu. Kwa hakika atafanya kila kitu katika uwezo wake ili kuwakatisha tamaa Wakristo wapya. Hebu rudia kutazama ile orodha ya mambo katika chemsha bongo tuliyotumia mwanzoni mwa somo hili na utoe mifano jinsi ambavyo Shetani angeweza kutumia baadhi ya hayo yanayotajwa ili kuleta mashaka katika akili zako.

**Watu wengine:** Mwongozo Wa Mwanafunzi katika ukurasa wa 39-40 huonyesha njia kadhaa mbalimbali za watu wengine kutumika kuleta mashaka katika akili yako. Hebu wanafunzi wachache watoe mifano kutoka maishani mwao kuhusu mashaka ambayo yamekuja kwa sababu ya watu wengine.

**Wewe mwenyewe:** Onyesha kwamba kimsingi, mashaka ni mawazo katika akili zako. Wakati mwingine hayo mawazo yenye mashaka hutoka kwa wengine. Lakini kuna watu wengine wanaojitengenezea mashaka yao wenyewe. Wanakuwa na maswali juu ya Mungu na njia Zake. Wape nafasi wanafunzi watoe mifano binafsi ya hoja hiyo.

Watu wengine watasema kwamba hayo mashaka kwa kweli hutoka kwa Shetani. Pengine ni kweli kwa kipindi fulani. Lakini kuna nyakati ambapo watu hukataa tu kumwamini Mungu na Neno Lake. Wanakuwa wamefanya uamuzi wenyewe. Hivyo ndivyo mambo yalivyotokea kwa Waisraeli baada ya kutoka Misri wakiwa njiani kwenda Nchi ya Ahadi.

**Zaburi 95:8-10 TLR**

**(8) Msiifanye mioyo yenu kuwa migumu, kama Israeli walivyofanya katika nyika, pale Meriba na Masa. (9) Kwa sababu hapo, baba zenu walinitilia shaka, ingawa walikuwa wameona miujiza yangu mingi kabla ya hapo. Uvumilivu wangu ulijaribiwa sana kwa malalamiko yao. (10) "Kwa miaka arobaini niliwatazama kwa hasira" asema Bwana Mungu. "Walikuwa taifa ambalo mawazo yao na mioyo yao ilikuwa mbali nami. Walikataa kukubali sheria zangu."**

**10. Je, Mungu hutia mashaka katika akili yako?**
**(Dakika 5-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 40-41**

Wakristo wengi wanapata wakati mgumu kuamini kwamba Mungu anaweza kutia mashaka katika akili zao. Mfano wa kiBiblia wa yule kijana tajiri kumjia Yesu na maswali yake unafaa hapa, ingawa Biblia haisemi wazi kwamba mambo yalikuwa hivyo. Mwongozo Wa Mwanafunzi kinazungumzia tukio hili na kutoa maelezo ni kwa nini Mungu alete mashaka katika akili za huyu kijana tajiri.



Mara chache Yesu alizungumza kwa ukali sana kwa viongozi wa dini wa siku Zake. Ni salama kudhani kwamba faida moja iliyotokana na maneno Yake makali ilikuwa kupanda mbegu za mashaka katika akili zao. Yeye alikuwa anajaribu kuwashtua kutoka kwenye uongo wao. Yesu alionyesha njia tofauti kabisa ya kupima kiroho ya kweli. Nina hakika alitumaini kwamba wangeanza kuwa na mashaka juu ya jinsi walivyokuwa wanafikiri.

Kuna watu wengine ambao watahisi salama zaidi kusema tendo hili la Mungu ni "kazi ya Roho Mtakatifu kuonyesha hatia". Kwa hakika Yeye hutuonyesha hatia ya dhambi. Hakikisha kwamba unaweka wazi aina za mashaka ambayo Mungu analeta katika akili ya mtu. Mungu hawezi kuleta mashaka juu ya kuwepo Kwake katika akili zao. Ataleta mashaka kwamba je, ni Wakristo kweli au sio? Si kitu kinachowezekana kwamba Mungu afanye hivyo kwa Mkristo wa dhati, anayemaanisha. Lakini, kama huyo mtu atajiona sio, basi ni sawa kutazamia kwamba Mungu ataleta mashaka hayo. Ikiwa Mungu ataona kwamba mtu huyo amepotoka na anaelekea kwenye uharibifu kiroho, basi atajaribu kumjali mtu huyo aone kosa la njia zake.

Uwe makini usikwame kwenye mjadala mzito wa kitheolojia hapa. Jambo kuu la kutambua ni kwamba Shetani si chanzo cha moja kwa moja cha kila mashaka yanayokujia. Tunapotazama namna ya kuondoa mashaka, tutahitaji kumtambua yule anayeleta mashaka katika akili yako. Hii itahusika moja kwa moja na suluhisho ambalo mtu anatumia kuondoa hayo mashaka.

**11. Aina tatu za matatizo ambazo husababisha mashaka**
**(Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 41-42**

Sasa tunataka kutazama kwa ukaribu zaidi matatizo yanayosababisha mashaka. Matatizo hayo yanaweza kuwekwa kwa mafungu matatu:

1. Upungufu wa maarifa
2. Upungufu wa uelewa
3. Upungufu wa tabia

Pitia matatizo yanayozungumzwa katika kipindi hiki cha darasa, na kujadili jinsi mashaka yanavyoweza kusababishwa na upungufu mmojawapo. Kuna matatizo mengine yanayohusisha mapungufu katika maeneo yote matatu. Chukua tena ule mfano wa kiBiblia wa kijana tajiri. Mashaka yake ni kama yalitokana na mapungufu yake katika maarifa. Lakini, baada ya Yesu kumpa suluhisho la wazi kabisa la tatizo lake, huyo kijana tajiri alipata mapungufu katika tabia. Yeye alijua suluhisho, akalielewa vizuri kabisa, lakini akaamua hatafanya.

Sababu moja ya kawaida kabisa ya mashaka inahusiana na majaribu.
Mtu anapokubaliana na jaribu la dhambi, mara nyingi Shetani anakuja kwa wingi wa hukumu na hatia. Mashaka yanaingia kama gharika. Sababu ilikuwa ni tatizo la tabia. Baada ya mhusika kufanya dhambi, mashaka yanakuwa makubwa zaidi kuliko nyakati zile ambazo alifikiri tu juu ya jaribu lenyewe.

7

Ikiwa wanafunzi wako wataanza kufikiri kulingana na makundi hayo matatu, itawasaidia katika kipindi kinachofuata wakati tunapozungumzia suluhisho au ufumbuzi kwa matatizo yanayoleta mashaka husika. Kama wanakabiliwa na tatizo linalofaa eneo la mapungufu ya maarifa, basi tatizo hilo linaweza kutatuliwa kwa kupata habari sahihi. Lakini, kama ni mapungufu katika tabia, basi habari zaidi hazitabadilisha hali husika papo kwa hapo.

**12. Jadili Hoja B-1 – B-10. Matatizo yanayoweza kusababisha mashaka**
**(Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 42-45**

Mwongozo wa wanafunzi unakupa maelezo ya aina 10 za matatizo mabalimabali ambayo yanaweza kusababisha mashaka. Tunaweza kuongeza mengi kwa orodha hii. Hata hivyo, haya ndiyo matatizo ya mara kwa mara amabayo wakiristo wengi hupambana nayo.

Utakapokuwa unajadili matatizo haya kumi, unaweza kuuliza kutoka kwa wale watakaojitolea na ambao wamegudua kwamba mojawapo wa matatizo haya limemsababisha kuwa na mashaka kuhusu kuwa Mkristo. Iwapo wanafunzi wako hawako radhi kutolea wengine mifano yao ya kibinafsi, unaweza katumia hadithi za wanafunzi wa awali au za watu wengine amabao waliangaika na matatizo haya.

Hoja kuu ambayo tunataka wailewe ni kwamba, kuna matatizo mengi mbalimbali ambayo yanaweza kumfanya mtu kuwa na mashaka. Kwa kipindi cha darasa lijalo, tutazungumzia hatua haswa ambazo wanaweza kuchukua ili kushinda matatizo haya yanayosababisha mashaka.

Unaweza kungeza matatizo mengine zaidi ya haya kumi kwa orodha hii iliyotolewa katika mwongozo wa mwanafunzi.

**13. Jadili Hoja C. Utagunduaje kinachosababisha mashaka yako? (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 46**

Mwongozo Wa Mwanafunzi kinatoa mawazo manne ya jinsi unavyoweza kugundua kinachokufanya uwe na mashaka. Tazama ukurasa wa 46 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

Kama una muda katika kipindi hiki, rudia hayo mambo manne. Hii kwa kweli ni sehemu ya utaratibu wa kuyaondoa kabisa mashaka yako. Ukitaka kushinda mashaka yako, ni lazima ugundue tatizo ni nini, linalosababisha shaka husika.

**14. Igizo la mashaka ya Yusufu (Dakika 5–10)**

Wakumbushe wanafunzi kwamba mara kwa mara Wakristo watakabiliana na mashaka katika kipindi cha baadaye maishani mwao, na mara ile ya kwanza wanapokuwa Wakristo. Maisha ya Yusufu katika Agano la Kale yalionyesha maeneo kadhaa magumu ambapo ingekuwa rahisi kwake kuwa na mashaka na Mungu.

Kwa kifupi fanya majumuisho ya matukio maishani mwa Yusufu, na ueleze ni kwa nini Potifa alimtupa gerezani. (Tazama Mwanzo sura ya 37 na 39.) Wanafunzi wawili wacheze mchezo huu. Limetolwa katika kitabu kiitwacho *Turnabout Teaching,* kilichoandikwa na Marlene LeFever, (wachapishaji niDavid C. Cook, ukurasa wa 13.) Haya yametumika kwa kibali maalum.

**Mazingira: Yusufu ameshtakiwa kwa uongo, na ametupwa gerezani.**

Hebu kuwe na igizo la mjadala ambao pengine ulitokea mawazoni mwa Yusufu katika miaka ile ya kukaa gerezani. Mwanafunzi mmoja aigize nafsi ya Yusufu yenye mashaka, na mwingine aigize nafsi ya Yusufu yenye matumaini.

Igizo linaweza kuanza hivi: **NAFSI YENYE MASHAKA**: Lakini Mungu! Nilikufuata. Haya ndiyo malipo ya kukufuata? Sielewi hata kidogo.
**NAFSI YENYE MATUMAINI**: Hapana! Kweli sielewi, lakini nakumbuka kusikia habari za jinsi ulivyomwongoza Ibrahimu katika kipindi na mambo magumu. Hakika utanitendea na mimi hivyo hivyo.

**15. Kufanyia Somo Kazi Maishani (Dakika 5-10)**

Hebu lenga shughuli hii kwa kila mwanafunzi kutambua matatizo katika maisha yake, yanayoweza kuwa yanamletea yeye mashaka. Pia wanaweza kuandika tatizo linalowafanya wahisi kuwa mbali na Mungu.

Ukiwa na nafasi, waambie wanafunzi wako wafikiri juu ya kundi wanaloweza kuweka tatizo hilo.

1. Upungufu wa maarifa
2. Upungufu wa uelewa
3. Upungufu wa tabia

**16. Kazi za kufanya**

A. Mwisho wa kipindi, toa chemsha bongo ya Yakobo 1:5-6.

B. Leo sahihisha Zoezi la 9, 10 na 11 kutoka kwa Mwongozo Wa Somo, au mwishoni mwa kipindi kijacho cha darasa.

C. Wanafunzi wasome sura ya 4 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kurudia mambo tuliyozungumza leo na kujiandaa kwa ajili ya kipindi cha darasa kinachofuata.

**17. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa**

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 8
## Kuondoa Mashaka—Sehemu ya 1

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Naweza kuyaondoa mashaka yangu juu ya kuwa Mkristo nitakapotengeneza mfumo wa kushinda tatizo linalosababisha mashaka haya.

**2. Mstari Mkuu: Wafilipi 1:6 TLR**

Nina hakika kwamba Mungu aliyeanzisha kazi njema ndani yenu ataendelea kufanya kazi ndani yenu mpaka siku Yesu Kristo atakapokuja tena.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura Ya 4 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inaendana na hili somo.

**4. Maandalio Ya Mwalimu**

Panga kutumia sehemu kubwa ya kipindi cha darasa la leo kuzungumzia baadhi ya mifano ya kiBiblia ya watu waliokuwa na mashaka. Usione kwamba ni lazima ujadili kwa kirefu kila mfano katika ile mifano mitatu. Unaweza ukatumia muda wako mwingi kuzungumzia habari za Tomaso, na ukataja hao wengine kwa kifupi, au ukatumia habari zao katika kipindi kinachofuata cha darasa. Watatu wanaotumika katika mpango huu wa somo ni:

A. Tomaso kuwa na mashaka ya yesu kuwa hai; katika Yohana 20:19-31

B. Mashaka ya Petro alipotembea juu ya maji; katika Mathayo 14:22-33

C. Yusufu kuwa na mashaka ya maelezo ya Mariamu kuwa mja mzito; katika Mathayo 1:18-21

Njia nyingine ya kufundisha somo hili ni kuwapangia wanafunzi mapema hizo habari tatu, na kuwaambie waandae taarifa kwa ajili ya darasa zima, ambayo ingehusika na mambo yote unayotaka kuzungumzia katika kipindi hicho cha darasa.

Unaweza kumchagua mwanafunzi mmoja atoe taarifa hiyo, au wote waliomaliza kuchambua hadithi husika watoe michango yao wakati wa kutolewa taarifa husika.

8

**5. Zoezi la utangulizi wa somo: Kujifunza Kutokana Na Maisha (Dakika 5-10)**

Timo amekuwa Mkristo kwa miezi karibu miwili. Alijikuta amekuwa Mkristo kutokana na ushawishi wa Badi, rafiki yake wa zamani tokea shuleni. Timo na Badi sasa wako katika kikundi cha ushirika wa kanisa moja. Badi anapenda sana ushirika husika, naye huhisi vizuri kuhusu kukua katika Ukristo.

Lakini Timo hana msisimko wa kuwa Mkristo kama alivyokuwa nao miezi miwili iliyopita. Kujifunza Biblia na maombi anaona ni mambo yanayochukua muda mwingi, na baadhi ya tabia za zamani alizoacha alipotoa maisha yake kwa Kristo bado zinamvutia. Hii inamfanya awe na wasiwasi kama kweli ni Mkristo. Hajawaambia watu

wa kwao wala marafiki zake juu ya badiliko hili katika maisha yake. Ana uhakika kwamba siri yake haijafichuka kwa sababu hakuna mtu yeyote nyumbani kwao aliyemwambia chochote juu ya mabadiliko yoyote ambayo wameyaona maishani mwake.

Timo anahisi kusongwa mawazo juu ya hayo yote. Wakristo wengine wote katika kikundi cha kanisani wanajua jinsi alivyojitolea kwa Kristo. Lakini yeye anahisi kama yuko chini kwao. Haijui Biblia vizuri sana kama wao. Hawezi kuomba kama wao, na hazungumzi juu ya Bwana kama wao. Timo amepata mashaka sana kama kweli yeye ni Mkristo au hapana.

**Maswali Ya Kujadiliana:**

1. Je, Timo azungumze na Badi kuhusu mashaka yake? Mnaonaje?
2. Je, Badi aseme nini iwapo Timo atamwambia mashaka aliyo nayo?
3. Mnadhani sababu kubwa ya mashaka ya Timo ni nini?
4. Mnadhani ni nini kitatokea ikiwa Timo hatafikia kwenye mzizi wa mashaka yake na kujaribu kuyashinda?

Labda uchapishe funzo hili pamoja na hayo maswali manne ya kujadiliana. Wape wanafunzi wanapoingia darasani. Waambie waandike majibu yao kabla ya kuanza kuzungumzia jambo lenyewe.

### 6. Marudio mafupi ya darasa lako lililopita (Dakika 5)

8

Rudia kwa kifupi baadhi ya mambo makuu mliyozungumza katika kipindi kilichopita cha darasa lako.

- Mashaka ni nini?
- Nani anayeleta mashaka akilini mwako?
- Mashaka si tatizo, bali ni dalili au matokeo ya tatizo.
- Matatizo aina tatu yanaweza kusababisha mashaka:
    1. Upungufu wa maarifa
    2. Upungufu wa uelewa
    3. Upungufu wa tabia

Tutatumia hayo mambo muhimu kutathmini yale mafunzo ya kiBiblia kuhusu uzoefu maishani mwa watu, tutakayotazama katika darasa letu leo.

### 7. Tambulisha jambo la Tomaso (Dakika 5-10)

Wanafunzi wasome kwa sauti habari ya mashaka ya Tomaso kutoka Yohana 20:19-31. Kabla ya kusoma habari yenyewe, waambie wawe macho kuona jinsi Tomaso alivyoshughulikia mashaka yake.

Baada ya kusoma Maandiko, uliza swali hili:
**Ni kitu gani kinachogusa zaidi kuhusu tukio hili?**

Wanafunzi washirikishe darasa mambo waliyopata kutokana na hadithi hii. Je, wanaweza kujitambulisha na Tomaso na mashaka yake?

**8. Nini kilichosababisha mashaka ya Tomaso? (Dakika 5-10)**

Waulize wanafunzi wanadhani kilichokuwa kinasababisha mashaka kwa Tomaso ni kitu gani? Jaribu kuruhusu maoni mbalimbali kuhusu mada hiyo. Jaribu kuwafanya wanafunzi wafikiri zaidi ya kawaida. Tomaso alisema, kwa kuwa yeye binafsi hakuwa amemwona Yesu, alikuwa na mashaka kama kweli yu hai. Lakii je, hilo ndilo lilikuwa sababu ya kweli? Je, Tomaso ana tatizo la kina zaidi na la ndani zaidi? Uwezekano mmoja ni huu – Tomaso anaonyesha tatizo la kutoweza kuwaamini watu wengine, na maneno yao pia.

Waulize wanafunzi wako wanafikiri Tomaso alikuwa na tatizo aina gani. Je, ilikuwa:

1. Upungufu wa maarifa
2. Upungufu wa uelewa
3. Upungufu wa tabia

Waambie wafafanue ni kwa nini wanafikiri tatizo lilikuwa la aina hiyo katika maisha yake. Mimi nadhani lilikuwa tatizo la maarifa tu. Yeye alitaka aina fulani ya maarifa ili kuondoa mashaka yake – maarifa ya kujionea mwenyewe moja kwa moja. Alipoona zile alama za misumari mikononi mwa Yesu na kugusa lile kovu ubavuni mwake, basi angeamini.

Kwa undani zaidi, tatizo lake lilikuwa kutoamini. Hili ni tatizo la kitabia. Unamwonyesha mtu kwamba unamwamini kwa tabia yako. Tomaso angeweza kufanya hivyo kwa kukubali habari aliyopewa na wale wanafunzi wengine waliokwishamwona Yesu.

8

**9. Suluhisho la Tomaso kwa mashaka yake lilikuwa lipi? (Dakika 10-15) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 47-48**

Waambie wanafunzi wagundue kitu Tomaso alichosema kingeondoa mashaka yake. Baada ya kuzungumzia suluhisho lake, tumia muda kutambulisha ule mpango wa hatua tano za kuondoa mashaka. Tazama Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 47-48.

Baada ya kupitia hatua hizo zote za kuondoa mashaka, hebu tathmini matendo ya Tomaso ili kuona alitumia hatua gani kati ya hizo. Ni wazi kabisa kwamba alitumia hatua ya kwanza. Maandiko hayataji kama alitumia hatua ya 2, ya 3 au ya 3. Hakika alikuwa na mpango dhahiri kabisa wa kondoa mashaka yake (hatua ya 5). Je, hiyo ndiyo ilikuwa njia ya Mungu ya kuondoa mashaka yake? Tutaona jibu lake tutakapozungumzia mambo yaliyotokana na shughuli za mipango ya kufundishia namba 10 na 11.

Itakuwa vizuri pia kuona Tomaso alikuwa anamtafuta Yesu amsaidie katika kutatua mashaka yake. Tunahitaji kuona hivyo hivyo. Tukirudia ile mifano mitatu ya matatizo yanayoweza kuleta mashaka, ufumbuzi wa Tomaso ulikuwa ni mzuri sana wa kutumia kupata habari ile aliyotaka. Lakini, ufumbuzi huo usingemaliza hapo hapo tatizo lake la ndani zaidi, la kuwaamini watu.

Tomaso hajakiri kwamba ana tatizo la kuwaamini watu wengine. Kama atakataa kukiri kwamba ana tatizo hili, basi ujue kabisa kwamba atapata matatizo tena katika wakati ujao, kwa habari ya kuwaamini watu wengine. Hebu zungumzeni Tomaso angetakiwa kufanya mabadiliko ya aina gani ili aweze kukuza na kuendeleza hali ya kuwaamini Wakristo wengine zaidi.

**10. Je, Yesu alimsaidiaje Tomaso kuondoa mashaka yake? (Dakika 5-10)**

Waambie wanafunzi wazungumzie majibu ya maswali haya. Ikiwezekana, wathibitishe au kuunganisha kila jibu kwa Maandiko.

1. Je, Yesu alimsaidiaje Tomaso kuondoa mashaka yake?
2. Je, Yesu alikubaliana na mpango wa Tomaso wa kuondoa mashaka yake?
3. Tomaso alimwitikiaje Yesu?
4. Itikio la Tomaso linatuambia nini kuhusu udhati aliokuwa nao kuhusu kuondoa mashaka yake?

Tomaso ni mtu wa kwanza katika Agano Jipya kumwita Yesu "Mungu" moja kwa moja. Tomaso alifanya hivyo kibinafsi kabisa, "Bwana wangu na Mungu wangu." Hakuwa anateseka na wasiwasi juu ya kumfuata Mungu na kumtumikia. Mashaka yake yalikuwa kuhusu iwapo Yesu alikuwa hai au hapana.

**11. Yesu alisema ni kitu gani kilichokuwa kinamfanya Tomaso kuwa na mashaka? (Dakika 5-10)**

Tumekwisha ona kwamba Yesu alitaka sana kumsaidia Tomaso kutatua mashaka yake. Hebu tutazame Yesu alisema nini juu ya kile kilichokuwa kinasababisha mashaka yake. Ona kwamba Yesu hamkemei Tomaso kwa nguvu sana kwa sababu ya mashaka. Lakini katika Yohana 20:29, Yesu kwa utaratibu sana anachimba ili agundue tatizo la ndani zaidi na la kina katika maisha ya Tomaso. Kwa njia nzuri tu, Yesu anaonyesha kwamba njia bora zaidi ni kuamini kuliko kuona ushahidi halisi wakati wote. Yesu hasemi kwamba Tomaso alikosea kutaka kuona ushahidi halisi. Yesu alikuwa tayari, na alipenda sana kutoa ushahidi husika.

8

Lakini, maisha ya imani kama Mkristo yanadai imani ambayo si wakati wote itaungwa mkono na ushahidi halisi. Itakuwaje ikiwa kila Mkristo leo atadai ushahidi ule ule ambao Tomaso alidai? Je, yesu angekuwa tayari kumtokea kibinafsi kila Mkristo mpya ili waweze kugusa yale makovu mikononi Mwake na kutia mkono pale ambapo mkuki ulimtoboa ubavuni Mwake?

Maisha ya Kikristo hutaka tujifunze kumwamini Mungu na kuwaamini Wakristo wengine. Kukosekana kwa imani ndani ya Tomaso kunaonekana kuwa tatizo kubwa zaidi ambalo Yesu alitaka ashughulike nalo. Yaweza kuwa vizuri kutambua kwamba Tomaso hakuwa mwanafunzi pekee aliyekuwa na mashaka ya mambo aliyoambiwa na watu wengine juu ya kufufuka kwa Yesu.

Soma Luka 24:9-12, mahali ambapo panaonyesha kwamba wanafunzi wote walipata mashaka mwanzoni. Hata baada ya wale watu wawili kutoka Emau kuwaambia wanafunzi kwamba walikutana na Yesu, bado wanafunzi walikuwa na mashaka. Baada ya Yesu kuwatokea na kutuliza hofu zao, ndipo waliamini kwamba yu hai. Tazama Luka 24:36-43.

**12. Somo kutoka kisa cha Yesu na Petro kutembea juu ya maji (Dakika 5-20)**

Tutatumia maswali yale yale tuliyotumia na Tomaso ili kuzungumzia mashaka katika maisha ya Petro. Waambie wanafunzi wagundue tatizo lililokuwa linasababisha mashaka, matokeo ya mashaka, na jinsi Yesu alivyomsaidia Petro kuondoa mashaka yake.

1. Soma Mathayo 14:22-33
2. Ni nini kilichokugusa kuhusu hadithi hii?
3. Ni nini kilichokuwa kinamsababisha Petro kuwa na mashaka?
4. Ni nani aliyekuwa analeta mashaka hayo katika akili yake? (yeye mwenyewe)
5. Ni nini matokeo ya mashaka ya Petro?
   - ya papo kwa hapo
   - Je, unafikiri Petro alihis vipi baada ya kurudi ndani ya mtumbwi, na kukabiliana na wanafunzi wengine?
6. Petro alifanya nini ili kuondoa mashaka yake?

(Tatizo lake la kwanza lilikuwa kushughulika na matokeo ya mashaka yake – alikuwa anaogopa kuzama kama Yesu asingemsaidia. Baadaye angepata muda wa kushughulika na matatizo yaliyosababisha mashaka yake – hofu, kutoamini, na kutokuwa na imani.)

7. Yesu alifanya nini kumsaidia Petro?

Je, hili lilimsaidia Petro kuondoa mashaka yake, au huo ulikuwa ni msaada tu wa jinsi ya kushughulikia matokeo ya mashaka yake?

Kama alivyosema na Tomaso, Yesu alimpa Petro ushauri ulio wazi kabisa, tena kwa upole sana, ila kwa uthabiti. Hakumkemea, bali alitamka maneno machache tu kuhusu njia iliyokuwa bora ya kukabiliana na hali ngumu. Tazama Mathayo 14:31.

8

**13. Mashaka ya Yusufu kuhusu mimba ya Mariamu (Dakika 5-15)**

Habari inayosimuliwa katika Mathayo 1:18-25 haitaji moja kwa moja kwamba Yusufu alikuwa na mashaka juu ya kilichotokea kwa Mariamu. Lakini matendo yake yanaonyesha kuweka wazi kwamba hakuamini hadithi yake – kama alimwambia jinsi alivyopata mimba. Yusufu alipanga kuvunja ndoa yao au uchumba wao kwa sababu yeye alijua hahusiki na uja uzito wake.

Maandiko hayasemi kwamba alikabiliana na mashaka. Lakini Mungu alitoa suluhisho kwa mashaka yake, na alimwambia cha kufanya kwa uwazi kabisa. Hakika Yusufu angeweza kupata sababu za kutilia shaka ndoto aliyopewa. Katika hali inayofanana na hiyo, malaika alimtokea Zekaria, akimtangazia kwamba mke wake angepata mwana ambaye wangemwita Yohana. Zekaria alitilia shaka ujumbe wa malaika, naye alipewa “ishara” kwamba huo ujumbe ulikuwa umetoka kwa Mungu kweli. Hakuweza kuzungumza mpaka baada ya kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.

Yusufu alikuwa na tatizo la maarifa. Kama Mariamu alijaribu kueleza jinsi alivyopata mimba, ni rahisi sana kuona ni kwa nini Yusufu alipata wakati mgumu kumwamini. Mungu alimpa Yusufu habari aliyohitaji katika ndoto. Yusufu akaikubali habari hiyo kwa hiari, na matendo yake yanaonyesha hivyo. Tatizo lilikuwa jepesi tu – upungufu wa maarifa. Suluhisho lilikuwa rahisi tu – Mungu alimpa habari iliyohitajika. Tabia ya Yusufu inaonyesha kwamba aliitikia hiyo habari mpya kwa haraka.

Yafuatayo ni maswali machache ambayo unaweza kuyatumia kuzungumzia tukio hili katika maisha ya Yusufu na Mariamu.

1. Ni nini kinachokugusa kuhusu tukio hili?
2. Ni nini kilichosababisha Yusufu kuwa na mashaka na maelezo ya Mariamu? Hebu jiweke kwenye nafasi ya Yusufu. Je, ungemwamini mchumba wako kama angekwambia Mungu ndiye amemfanya kuwa mja mzito?
3. Ni tendo gani ambalo Yusufu aliamua kulifanya lenye kuonyesha kwamba hakuamini maelezo ya Mariamu juu ya kuwa mja mzito?
4. Mungu alimsaidiaje Yusufu kutatua tatizo hilo?
5. Je, Yusufu aliitikiaje ndoto ile? Je, itikio lake linaonyesha kwamba bado alikuwa na mashaka?

### 14. Mungu anawatendeaje wale wenye mashaka? (Dakika 5-10)

8

Hiyo mifano yote ya kiBiblia inatoa picha iliyo wazi jinsi Mungu anavyoshughulika na wale walio na mashaka. Mungu hakupuuzia mashaka yao. Alishughulika moja kwa moja na kila moja. Yeye hakuwakemea sana wala kuwahukumu kwa utovu wao wa imani. Mashaka si “dhambi mbaya kuliko zote” unazoweza kutenda. Uhalisi wa maisha ni huu: watu wengi hukabiliana na mashaka. Katika hii mifano mitatu, wahusika waliamua kuweka mbali mashaka yao na kukubali msaada wa Mungu. Hawakung’ang’ania maswali yao baada ya Mungu kuwapa majibu.

Lakini, lazima tuwe makini tusije tukakataa msaada wa Mungu. Hasira Yake ilielekezwa kwa wale waliokataa kumwamini Yeye na wale walioendelea kuhoja uaminifu na ukweli Wake. Waisraeli waliosafiri toka Misri kwenda Nchi ya Ahadi ya Israeli walikuwa na aina hiyo ya hatia ya kutokuamini. Tazama Zaburi 95:8-10.

### 15. Kufanyia Kazi Somo Maishani (Dakika 5-10)

Wanafunzi wapewe nafasi ya kuandika jambo moja walilo na mashaka nalo, au zaidi. Kabla ya darasa linalofuata, wapitie ule mpango wenye hatua tano utolewao katika ukurasa wa 47-48 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Waandike majibu ya kila hatua, hasa hatua ya 3 na ya 5. Walete majibu yao katika kipindi kinachofuata kwa ajili ya mazungumzo zaidi jinsi ya kuondoa mashaka.

Kama hawana mashaka yoyote kwa sasa, waambie waandike shaka au mashaka waliyowahi kuwa nayo siku zilizopita. Ni nini kilichosababisha? Waliiondoaje hilo shaka?

**16. Kazi Za Kufanya**

A. Leo sahihisha Zoezi la 8 na 9 katika Mwongozo Wa Somo kama hukufanya hivyo katika kipindi kilichopita.

B. Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 5, *"Andika Hadithi Yako"*.

C. Wanafunzi wasome sura ya 4 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi ili kurudia mambo tuliyozungumza leo na kujiandaa kwa ajili ya kipindi cha darasa kinachofuata.

**17. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa**

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 9
## Kuondoa Mashaka—Sehemu ya 2

**1. Kweli Kuu Ya KiBiblia**

Naweza kuondoa mashaka yangu kuhusu kuwa Mkristo nitakapotengeneza mfumo wa kushinda tatizo linaloyasababisha mashaka haya.

**2. Mstari Mkuu: Zaburi 94:19 TLR**

Ee Bwana! Mashaka yanapojaa katika akili yangu, na moyo wangu unapokuwa katika kuvurugikiwa, nitulize na kunipa tumaini jipya pamoja na furaha.

**3. Mafundisho ya mwanafunzi yaliyotumiwa katika somo hili**

Sura ya 4 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi inaendana na somo hili. Zoezi la 12 linaloitwa *"Kuondoa Mashaka"*, katika Mwongozo Wa Somo litatumiwa na somo hili. Muda ukiruhusu, tunaweza pia kutumia Zoezi la 5 linaloitwa *"Andika Hadithi Yako."*

**4. Zoezi la utangulizi wa somo: Nikifa Usiku Wa Leo (Dakika 3-5)**

Anza kipindi cha leo kwa kumwuliza kila mwanafunzi kujibu swali lifuatalo. Usiwatake wajibu kwa sauti mbele ya darasa. Pengine ni vizuri utengeneze nakala ya kipengele hiki na uwape nafasi kila mmoja ajaze peke yake. Waambie mapema kama utakusanya au kama utawaachia majibu yao.

9

Ikiwa utakufa usiku wa leo, una uhakika kwamba utaingia mbinguni? Eleza kwa kifupi sababu ya kuchagua jibu lako.

___1. Ndiyo. Ninahisi salama kabisa katika uhusiano wangu na Mungu, na nina uhakika na imani kubwa kabisa kwamba nitaingia mbinguni.

___2. Wakati mwingine ninakuwa na mashaka kama kweli nitaingia mbinguni au hapana.

___3. Sina hakika hata kidogo kwamba nitaingia mbinguni nikifa usiku wa leo.

___4 Sitaki kufikiri juu ya hilo.

Kwa kawaida, tunataka kipengele hiki cha Kuchangamkia Somo kuwasaidia wanafunzi kufunguka na kujihusisha kwa mazungumzo darasani. Swali hili linaweza kuwa tishio kubwa sana kwa wengine ambao hawana uhakika na uhusiano walio nao na Yesu. Njia moja ya kutuliza au kulainisha hali ngumu inayoweza kutokea ni kueleza jinsi ambavyo wewe ungeweza kujibu swali hilo katika nyakati tofauti maishani mwako. Eleza wakati ambapo ungechagua kila moja katika hayo majibu tofauti, na useme jinsi na kwa nini ulisogea kutoka hatua moja na kwenda kwa nyingine.

Ukiona kwamba itasaidia darasa, unaweza kuuliza ikiwa kuna yeyote ambaye angependa kushirikisha darasa kwa jibu lake. Toa nafasi kwao ili waeleze kwa kifupi ni kwa nini walichagua jibu walilochagua.

**5. Rudia kidogo ule mpango wa hatua 5 za kushinda mashaka (Dakika 5-10) Mwongozo wa Mwanafunzi, ukurasa wa 47-48**

Pitia ule mpango wa hatua 5 wa jinsi ya kuondoa mashaka utolewao katika ukurasa wa 47-48 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Toa mfano mmoja au miwili kutoka kwa maisha yako mwenyewe jinsi wewe umefuata mfumo huo. Hakikisha kuwashirikisha kwa matokeo yake. Je, ufumbuzi ulipata ulifanya kazi kweli? Kwa muda gani? Usiogope kushirikisha kushindwa pamoja na mafanikio.

**6. Zungumzia <u>sababu</u> za mashaka katika Utafiti wa 1 katika Mwongozo wa Somo Zoezi la 12* (Dakika 10-15)**

**Angalizo Maalum:** Andika kwa makini majibu mbalimbali yatakayotolewa na wanafunzi wako katika sehemu hii ya somo. Mawazo yao juu ya mifano hii miwili yanaweza kukusaidia sana utakapofundisha somo hili wakati mwingine.

Toa nafasi kwa wanafunzi mbalimbali kushirikisha majibu yao kwa swali la kwanza la mfano wa 1 katika Zoezi la 12 katika Mwongozo Wa Somo. Jaribu kufanya mjadala uwe endelevu, yaani, hoja moja isimalize mjadala, ili majibu mbalimbali yaweze kutolewa kwa uhuru. Baada ya kujadili majibu yao, tumia Dakika chache kurudia kidogo ule mpango wenye hatua nne juu ya kugundua kinachosababisha mashaka yako. Mpango huo umetolewa kwenye ukurasa wa 46 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Wanafunzi wako wazungumze jinsi ambavyo Pati angeweza kugundua sababu za mashaka yake kwa kutumia mpango huu.

Wanafunzi wako na wajadili jinsi ambavyo Pati angeweza kupata sababu za mashaka yake kwa kutumia mpango huu.

Ukishaamua yale yanayodhaniwa kuwa sababu za mashaka ya Pati, basi amueni matatizo yenyewe yanafaa kuangukia fungu lipi.

1. Upungufu wa maarifa
2. Upungufu wa uelewa
3. Upungufu wa tabia

9

Wanafunzi waunge mkono majibu yao kwa maelezo ya ni kwa nini waliamua hivyo. Kama wanaelwa vizuri sababu za mashaka ya Pati, basi itakuwa rahisi kwao kutoa njia zinazofaa kuondolea mbali mashaka hayo.

**7. Jadilianeni <u>ufumbuzi</u> kwa ajili ya mashaka katika Utafiti wa 1 katika Zoezi la 12 (Dakika 10-15)**

Toa nafasi kwa wanafunzi kushirikisha mawaazo yao kwa ajili ya ufumbuzi wa mashaka ya Pati katika mfano wa 1 katika Zoezi la 12 ya Mwongozo Wa Somo. Pengine majibu yao yataendana na matatizo waliyoorodhesha kwa swali la kwanza katika utafiti ule. Ufumbuzi watakaotoa kwa sehemu kubwa unaweza kuwa malengo ya muda mrefu. Kama ndivyo, waulize kukupa malengo ambayo Pati angeweza kuyaweka katika siku chache zijazo ili kuanza kuondoa matatizo hayo.

Jaribu kuwafanya wafikiri kuhusu matokeo yanayoweza kuletwa na yale malengo mbalimbali wanayopendekeza. Je, ni malengo yanayozingatia uhalisia? Au je, tatizo wamelifanya kuwa la kiroho zaidi?

**8. Zungumzia <u>sababu</u> za mashaka katika Utafiti wa 2 katika Zoezi la 12* (Dakika 10-15)**

Wanafunzi mbalimbali washirikishe majibu waliyotoa kwa swali la kwanza katika Mfano wa Pili katika Zoezi la 12 katika Mwongozo Wa Somo. Jaribu usiache mjadala kuwa na jibu litakaloumaliza ghafla ili majibu mbalimbali yanayowezekana yatolewe kwa uhuru. Hebu wazungumze jinsi Daudi anavyoweza kupata sababu za mashaka yake kwa kutumia ule mpango wa hatua nne upatikanao kwa ukurasa wa 46 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi.

Mkishaamua kwamba sababu zinazoweza kusababisha mashaka kwa Daudi ni zipi, basi amueni matatizo hayo yanaangukia fungu lipi.

1. Upungufu wa maarifa
2. Upungufu wa uelewa
3. Upungufu wa tabia

Wanafunzi waunge mkono majibu yao kwa maelezo ya ni kwa nini walichagua hivyo. Kama wanaelewa vizuri sababu za mashaka ya Daudi, itakuwa rahisi kwao kupata njia zinazofaa za yeye kuondolea mbali mashaka haya.

**9. Zungumzia <u>ufumbuzi</u> wa mashaka katika Utafiti wa 2 katika Zoezi la 12 (Dakika 10-15)**

Wanafunzi washirikishe mawazo yao ya ufumbuzi wa mashaka ya Daudi katika Utafiti wa 2 katika Zoezi la 12 katika Mwongozo Wa Somo. Majibu yao yanaweza kuendana na matatizo waliyoorodhesha kwa kujibu swali la kwanza katika utafiti ule. Tumia mapendekezo yale yale yatolewayo na ule utafiti wa Pati kutathmini ufumbuzi wanaotoa kwa ajili ya mashaka ya Daudi.

9

**10. Zungumzia mashaka waliyo nayo wanafunzi wako (Dakika 10-15)**

Shughuli ya kufanyia kazi somo maishani kwa darasa lililopita iliwataka wanafunzi waandike tathmini ya shaka ambalo walikuwa wanakabiliana nalo maishani mwao. Bila shaka wamekwisha andika tatizo linalosababisha mashaka hayo, na mapendekezo ya ufumbuzi kwa ajili ya kuondoa mashaka hayo. Waombe wanafunzi wa kujitolea wasome mbele ya darasa tatizo lao na ufumbuzi wanaopendekeza. Darasa lifanye tathmini mifano itolewayo na wanafunzi.

1. Je, unafikiri mwanafunzi amefafanua kwa usahihi tatizo linalosababisha mashaka hayo?
2. Je, kuna sababu zingine zinazoweza kuchangia tatizo?
3. Je, mwanafunzi ameweka hatua halisi za kutatua mashaka hayo?
4. Je, malengo husika ni rahisi na yana mwelekeo kiasi cha kuweza kuanza kuyafanyia kazi juma hili?
5. Je, malengo hayo yanapimika?
6. Mungu ana nafasi gani katika utaratibu wa ufumbuzi?
7. Je, mwanafunzi anategemea mengi kupita kiasi toka kwa Mungu, au Mungu anaachwa katika ufumbuzi husika?

Ikiwa una nafasi, ruhusu wanafunzi wachache washirikishe mashaka yao na kupitia utaratibu ule ule wa tathmini. Wakumbushe wanafunzi kufuata ushauri utolewao katika Yuda mstari wa 22 (TLR) "Wahurumieni wale wanaokuwa na mashaka." Hakikisha wanafunzi wanatoa mapendekezo mazuri na ya kusaidia.

**11. Rejelea matatizo yanayosababisha mashaka (Dakika 5-10)**

Inaweza kuwa msaada kama utarudia kidogo yale matatizo kumi yatolewayo kwenye ukurasa wa 42 hadi 45 katika Mwongozo Wa Mwanafunzi. Hayo ni matatizo ya kawaida ambayo mara nyingi huwafanya Wakristo kuwa na mashaka. Zungumza jinsi matatizo hayo yanavyoleta mashaka na jinsi yanavyoweza kutatuliwa.

Unaweza kutamani kushirikisha mifano ya wanafunzi wengine ambao wamepitia darasa hili hapo nyuma, na jinsi walivyoitikia mashaka. Hiyo itasaidia sana kama unao wanafunzi wasiohisi vizuri kushirikisha mifano yao na wanafunzi wengine.

Katika tafiti zote utakazozungumza, sisitiza thamani ya kujifunza Biblia kwa mtu binafsi kuwa ni sehemu moja muhimu sana ya kuondoa mashaka. Siri halisi ni kugundua njia ya Mungu ya kuondoa mashaka – njia Zake ni bora sana kuliko zozote tunazoweza kufikiri sisi. Watie moyo kugundua Mungu anachosema juu ya matatizo yanayosababisha mashaka yao. Waonyeshe jinsi wanavyoweza kufanya hivyo.

**12. Wasaidie wengine wenye mashaka (Dakika 5-10)**

Watie moyo wanafunzi kuwasaidia wengine ambao wanakabiliana na mashaka. Mara nyingi Mkristo mpya anaweza kujitambulisha rahisi sana na makabiliano ambayo Mkristo mwingine mpya anapitia. Ukiwa na muda, unaweza kurudia njia ile Yesu alitumia kushughulika na wale waliokuja Kwake wakiwa na mashaka.

Yule kijana tajiri; katika Luka 18:18-30

Petro akitembea juu ya maji; katika Mathayo 12:22-33

Tomaso akiwa na mashaka kuhusu Yesu kuwa hai; katika Yohana 20:19-31

Pengine ugawe darasa katika makundi matatu, na watazame tena ile mifano ya kiBiblia. Watengeneze orodha ya mawazo yanayosaidia tunayoweza kupata kutokana na jinsi Yesu alivyowasaidia waliokuwa na mashaka. Wanaweza kutayarisha orodha mbili:

1. Mambo ya kusaidia ya kuwafanyia wale wenye mashaka.
2. Mambo ya kutowafanyia wale wenye mashaka.

Kwa hayo maeneo yote matatu tunamwona Yesu akiitikia kwa njia inayofanana. Yeye hapuuzii mashaka yao kuwa hayana maana au si muhimu. Anazungumza na mhusika kwa upole. Yesu haonyeshi hali ya ukuu kwao. Hakuna mahubiri marefu yanayotokana na watu kukiri mashaka yao. Yesu alitoa ushauri mmoja tu rahisi na wa moja kwa moja wa kumaliza mashaka husika.

Wanafunzi wako wajue kwamba si wajibu wao kusuluhisha na kumaliza mashaka ya kila mtu. Hata ingawa hawana ufumbuzi wa tatizo husika, wanaweza kufanya mambo mawili muhimu sana. Kwanza: Wanaweza kuwa wasikilizaji wenye huruma. Mara nyingi mtu anayepambana na mashaka anahitaji hakikisho kwamba

anachokabiliana nacho si mwisho wa dunia. Pili: Wanaweza kumtia mtu moyo. Waambie wakiri hivi: “Mpendwa! Sina ufumbuzi wa tatizo lako, lakini nataka ujue kwamba ninakujali. Nitakuombea. Ninajua unaweza kumtegemea Mungu akusaidie, nami nitafanya kila ninachoweza kukusaidia pia.”

Watie moyo wawe makini na waangalifu kuhusu kujaribu kushughulikia mashaka ambayo Wakristo wengine wanayo. Wavunje moyo wasitoe majibu rahisi rahisi kama “Ombea jambo hilo, na mashaka yako yote yatatoweka.” Kweli, maombi ni sehemu muhimu sana katika utaratibu wa kupata hakiksho la uhusiano wako na Yesu. Lakini majibu ya aina hiyo, ya juu juu na rahisi tu, wakati mwingine yataharibu kuliko kutengeneza. Wakisikiliza kwa makini na kutoa maneno ya dhati ya kutia moyo, wawe na uhakika kwamba msaada wa aina hiyo hakika utamsaidia na kumnufaisha yule anayepambana na mashaka.

**13. Hitimisho (Dakika 5-10)**

Waulize ikiwa wana maswali mengine yoyote kuhusu somo zima. Ukiwa na muda zaidi, unaweza kumkaribisha mwanafunzi mmoja au wanafunzi wawili kulisomea darasa kazi waliyofanya katika **Zoezi la 5** katika Mwongozo Wa Somo, inayoitwa, ***Andika Hadithi Yako***. Ikiwa kazi-miradi hiyo imefanywa kwa usahihi, wanafunzi wataweza kumweleza vizuri mtu mwingine jinsi ya kuwa Mkristo.

**14. Kufanyia Somo Kazi Maishani (Dakika 5-10)**

A. Wahamasishe kuendelea kufanyia kazi malengo maalum ili kushinda matatizo yanayosababisha mashaka maishani mwao.

B. Wanafunzi waungane wawili wawili na kushirikishana angalau njia moja ambayo somo hili limewasaidia kujua kwamba ni Wakristo. Halafu, waombeane.



**15. Kazi Za Kufanya**

Sahihisha katika Mwongozo Wa Somo Zoezi la 12, *“Kuondoa Mashaka”,* na Mazoezi yote ambayo bado hujasahihisha.

**16. Tathmini Ya Mwalimu Baada Ya Darasa**

Tafadhali orodhesha mawazo yako kuhusu kuboresha somo hili.
Je, ni sehemu zipi zilizofaa?
Ni zipi zilizokuwa ngumu kueleweka na wanafunzi?
Ni zipi zilizowasaidia zaidi wanafunzi wako?

# Somo La 10
## Mtihani

**1. Utangulizi**

Fanya utangulizi wa somo litakalofuata.

A. Wape Mwongozo wa Somo au Mazoezi yoyote ambayo yanapaswa kukamilishwa kabla ya kipindi cha kwanza cha kozi ifuatayo utakayofundisha.

B. Waelekeze wanafunzi kufungua ukurasa wa mwisho katika Mwongozo wa Somo Mpya. Wanapaswa kupata nakala safi ya ***Orodha ya Kazi za Darasani.*** Wape tarehe za majaribio ya chemsha bongo, Zoezi, na mtihani.

C. Wape Mwongozo wa Mwanafunzi mpya na uwaambie kurasa watakazosoma kabla ya kipindi kijacho darasani.

**2. Wape mtihani wa Somo hili.**

**3. Ikiwa bado hujafanya hivyo, rudisha chemsha bongo zote na mazoezi ambayo umesahihisha.**

# Mwongozo wa Mwanafunzi

Mwongozo wa Mwanafunzi Haujajumuishwa kwenye hati hii,
lakini unapatikana katika hati tofauti.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Mwanafunzi.

# Mwongozo wa Somo

Haukujumuishwa kwenye hati hii, lakini unapatikana katika hati tofauti.

.

Tafadhali angalia ukurasa wa 5 ya Mwongozo huu Wa Mwalimu kwa habari kuhusu matumizi ya Mwongozo wa Somo.

# Mtihani

# Majibu ya mtihani

# Cheti cha Somo

Tazama ukurasa wa 5 wa mwongozo huu kwa habari zaidi kuhusu matumizi ya mtihani na cheti.

**Jina____________________ Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?**

**Tarehe__________________ Mtihani Wa 5**

**Darasa__________________ ________Alama**

**Maswali Ya Kweli – Si Kweli** (Kila jibu lina thamani ya alama 2)

Maelekezo: Weka alama ya __X__ ikiwa jibu ni kweli.

Weka alama ya __O__ ikiwa jibu si kweli.

1.________Kabla hujajua kwa uhakika kwamba wewe ni Mkristo, lazima uelewe maana ya kuwa Mkristo.

2.________Ukitaka kuwa Mkristo, lazima uwe tayari kumtii Mungu.

3.________Wewe ni Mkristo iwapo unahisi kwamba wewe ni Mkristo.

4.________Wokovu una misingi kwenye ukweli – ukweli ulioandikwa katika Biblia.

5.________Huna haja ya kuwa na imani kwa Mungu ili uwe Mkristo.

6.________Ikiwa umekuwa Mkristo, itakuchukua kama miaka miwili kabla ya kuanza kuona mabadiliko yoyote halisi katika maisha yako na tabia.

7.________Alama moja ya kwanza ya Mkristo wa kweli ni kwamba hatataka kuwashirikisha wengine kwa yale mambo ya Kristo anayofanya maishani mwake.

8.________Ikiwa Kristo anatawala maisha yako, basi maisha yako yanaweza kujaa na kukamilika.

9.________Ukitaka kuhakikisha kwamba wewe ni Mkristo, lazima umwambie Yesu aingie moyoni mwako kila siku, au katika kila ibada kanisani.

10._______Ikiwa unataka kwenda mbinguni, kitu pekee unachotakiwa kufanya ni kuamini tu kwamba Yesu alikuwa mtu mzuri.

11._______Biblia inatuambia jinsi ya kuwa Mkristo.

12._______Roho Mtakatifu atakwambia kama wewe ni Mkristo.

13._______Unapofanyika Mkristo, matatizo yako yote yanaondoka siku hiyo hiyo.

14._______Utakapokuwa Mkristo, Roho Mtakatifu atakusaidia na kukufundisha kuwa Mkristo mwenye nguvu zaidi.

15._______Yesu anataka kuwa rafiki yako mkubwa na bora sana.

16._______Ni lazima umwambie Yesu akusamehe dhambi zako kama unataka kuwa Mkristo.

### Maswali Yenye Majibu Ya Kuchagua

Chagua jibu lililo sahihi na kuweka herufi ya jibu hilo kwenye mstari. (Alama 2)

1.________Kama una mashaka ikiwa wewe ni Mkristo au siyo, unapaswa:

A. uyasahau tu.
B. umpe Mungu mashaka yako.
C. uyapuuze au kuyagandamiza.

### Maswali Ya Majibu Mafupi

1. Andika ORODHA ya kweli zile unazohitajika kujua ili uwe Mkristo. (Hizi ni zile kweli kutoka Biblia.) (Alama 8, kila sehemu ina alama 1)

   1.____________________
   2.____________________
   3.____________________
   4.____________________
   5.____________________
   6.____________________
   7.____________________
   8.____________________

2. Ni sehemu zipi tatu ambazo mtu anaweza kutazama ili kupata ushahidi kwamba yeye ni Mkristo? (Alama 9, kila jibu ni alama 3)

   a.____________________
   b.____________________
   c.____________________

3. Andika yale Maandiko Ya Kukariri na mahali yanapotoka. (Alama 21)

   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________
   ____________________

**Maswali Ya Majibu Mafupi** *Kuendelea*

4. Eleza maana ya kuwa na uhusiano binafsi na Yesu. (Alama 4)

**Nini ushauri wako?**

Wakristo wengi wakati fulani hugundua kwamba wanayo mashaka kwa sababu yao kuwa Wakristo. Unawezaje kuwasaidia watu hawa kutatua matatizo yao na kuwasaidia kuondoa mashaka yao?

1. Samu ni mwanafunzi katika shule ya Teen Challenge. Rafiki yake wa kike si Mkristo. Anataka Samu aachane na mpango wa shule hiyo. Kila wakati anapopigiwa simu na Samu, analia na kumwambia arudi nyumbani. Samu hajui afanye nini juu yake. Anaonekana kuwa ni sehemu ya maisha yake ambayo hajaitoa kwa Yesu Kristo. Hili linamfanya awe na mashaka kama kweli yeye ni Mkristo. Ungempa ushauri gani? (Alama 4)

2. Joe, ambaye amekuwa Mkristo juma lililopita, ana mashaka iwapo yeye bado ni Mkristo. Ana tatizo lingine. Bado anatumia ile lugha "ya zamani" na namna ya kuzungumza ya mtaani. Anahisi kwamba hatakiwi kutumia lugha ya mtaani, kwa kuwa ametambua kwamba kutukanana ni dhambi. Unampa ushauri gani? (Alama 4)

**Ni nini ushauri wako?** *Kuendelea*

3. Juma lililopita Sharon alimpokea Yesu kwa siri ndani ya basi akiwa anakwenda kazini. Ilikuwa ni kitu halisi kabisa kwake. Lakini sasa hivi hana uhakika tena na kitu hicho. (Alama 4)

   a. Tatizo lake ni nini?____________________

   b. Afanyeje juu ya hilo?____________________

4. Jeni anamchukia baba yake kwa sababu ya kumpiga. Amempokea Yesu Kristo binafsi hivi karibuni. Alipomwambia baba yake, baba alimwambia hivi: "Utakuwaje Mkristo na unichukie?" Alifikiri juu ya hilo akajiuliza, "Je, kweli mimi ni Mkristo?" (Alama 4.)

   a. Nini tatizo lake?____________________

   b. Ufumbuzi ni nini?____________________

5. Jose alimwibia baba yake shilingi laki tano na kumi (510,000/-). Sasa kwa kuwa amekuwa Mkristo, anhisi hatia juu ya jambo hilo. Lakini hataki kutengeneza mambo na baba yake. Anaamini kwamba anaweza kuwa Mkristo bandia. Je, afanyeje? (Alama 4)

6. Sasa, kwa kuwa Yohana ni Mkristo, anatambua kwamba ni mtu anayejivunia sana nywele zake zinazofikia kiunoni. Asipofanya kitu juu ya tatizo lake la majivuno, nini kinachoweza kutokea kwa Ukristo wake? (Alama 4)

## Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
### Mtihani Wa 5
### Karatasi ya Majibu

**Ukurasa wa 1**

**Maswali Ya Kweli – Si Kweli**
(Alama 2 kwa kila jibu)

1. X Kweli
2. X Kweli
3. 0 Si Kweli
4. X Kweli
5. 0 Si Kweli
6. 0 Si Kweli
7. 0 Si Kweli
8. X Kweli
9. 0 Si Kweli
10. 0 Si Kweli
11. X Kweli
12. X Kweli
13. 0 Si Kweli
14. X Kweli
15. X Kweli
16. X Kweli

**Ukurasa wa 2**

**Maswali Yenye Majibu Ya Kuchagua**
(Alama 2)

1. B

**Maswali Ya Majibu Mafupi**

1. Alama 8 (Alama 1 kwa kila moja)
    1. Mungu yupo.
    2. Mimi ni mwenye dhambi.
    3. Biblia ni ya kweli.
    4. Mungu ananipenda, na alimtuma Yesu kufa kwa ajili yangu.
    5. Yesu ndiye peke yake awezaye kunisamehe dhambi zangu.
    6. Adhabu ya dhambi ni kifo.
    7. Ninaweza kuokoka kwa kumwomba Yesu anisamehe.
    8. Lazima nimruhusu Yesu awe kiongozi wa maisha yangu.
2. Alama 9 (Alama 3 kila moja)
    1. Biblia
    2. Roho Mtakatifu
    3. Mabadiliko katika maisha yangu
3. Alama 21 (alama 7 kwa kila mstari)
    1. Warumi 8:16
    2. Yohana 1:12
    3. Yakobo 1:5-6

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?
## Mtihani Wa 5
## Karatasi ya Majibu

### Ukurasa wa 3

4. Alama 4 (Zipo njia kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kulitazama swali hili. Unaposahihisha majibu yao, usiwe na msimamo mkali. Zifuatazo ndizo hatua zitolewazo katika Kitabu cha Mwanafunzi kuhusu kukuza na kuendeleza uhusiano binafsi na Yesu.)

    1. Wote wawili lazima watake uhusiano huu.
    2. Jifunze jinsi ya kuwasiliana na Yesu.
    3. Jifunze kukuza uaminifu na ukweli.
    4. Jifunze kumheshimu na kumpenda Yeye.

### Jifunze kumheshimu na kumpenda Yeye
(Majibu yanayopendekezwa kwa ajili ya shughuli zote sita)

1. (Alama 4) Anahitaji kutoa sehemu hii ya maisha yake (rafiki yake wa kike) kwa Mungu.

2. (Alama 4) Anahitaji kuachana na dhambi hiyo.

### Ukurasa wa 4

3. Alama 4 (Jibu lenye sehemu 2)

    A. Anaficha ukweli kwamba amekuwa Mkristo. Sasa ana mashaka ikiwa yeye ni Mkristo kweli.

    B. Awaambie wengine kwamba amempokea Kristo.

4. Alama 4 (Jibu lenye sehemu 2)

    A. Ana uchungu.

    B. Anatakiwa kumsamehe baba yake.

5. (Alama 4) Amwambie baba yake mazingira yenyewe na kumwomba msamaha.

6. (Alama 4) Anaweza kupoteza uhusiano wake na Mungu.

**Hongera**

______________________________________

Amemaliza

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na nimatumaini yetu ya kwamba utaendelea kwa mafanikio
katika masomo yako yajayo.

Wakufunzi _________________________

Tarehe ____________________________

**Hongera**

______________________________________

Amemaliza

# Nawezaje Kujua Mimi Ni Mkristo?

Tunatambua kujitoa kwako katika masomo haya
na nimatumaini yetu ya kwamba utaendelea kwa mafanikio
katika masomo yako yajayo.

Wakufunzi _________________________

Tarehe ____________________________